# Nipashe

Jumanne Julai 16, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579971

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Wataalamu Oxford watua kutibu uloto na saratani

UKURASA 3


Nipashe

TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

JE, WAJUA?

Wanafunzi likizo imekwishamalizika, rejesheni fahamu zenu shuleni

Kwanini matumizi ya maziwa ya ngamia yanaongezeka duniani?

ANGALIZO LA MKAPA LITASAIDIA VYUO VIKUU BINAFSI NCHINI

UKURASA 13

# Askari polisi 54 wafukuzwa kazi

• **Wabainika** kujihusisha na rushwa, ujambazi...*Ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

### TPSF KUTUMIA FURSA YA SADC KUSAKA MASOKO

SEKTA binafsi wamejiandaa kutumia vyema fursa ya maadhimisho ya awamu ya nne ya Wiki ya Maonyesho ya Viwanda...

**UKURASA WA 5**

### MAKAMU RAIS AKEMEA VIZUIZI KWA WALEMAVU

KATIKA kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 kwa kuhakikisha wanawake na wanaume wenye ulemavu wanakuwa...

**UKURASA WA 7**

### SHAHIDI ASIMULIA MAZITO KORTINI KESI MAUAJI DAR

SHAHIDI wa Jamhuri, Sajenti Erasto (53), amedai katika kesi ya mauaji ya Mohammed Bushiri kwamba mwanafamilia...


## Mbaroni tuhuma mauaji Msumbiji

UKURASA 3



UKURASA 2

Rais John Magufuli akiwapungia mkono wananchi waliokuwa katika kivuko cha Busisi mkoani Mwanza wakati akitokea mkoani Geita jana. **PICHA: IKULU**

# JPM atoa neno uchaguzi

**MICHEZO** **KASEJA AFUNGUKA KUREJESHWA STARS** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Polisi 54 wafukuzwa kazi kwa rushwa, ujambazi

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

RAIS John Magufuli amepongeza utendaji mzuri wa Jeshi la Polisi nchini, huku akieleza kuchukizwa na askari wake wachache wasio waadilifu.

Amebainisha kuwa katika kipindi cha miezi sita iliyopita, askari polisi 157 wamechukuliwa hatua kwa kukiuka taratibu za kiutumishi. Kati yao, 54 wamefukuzwa jeshini.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa nyumba 20 za askari polisi zilizojengwa kwenye Mtaa wa Magogo mjini Geita.

Kutokana na kuwapo kwa changamoto hiyo, Rais Magufuli alimtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchni (IGP), Simon Sirro, kuwa mkali kwa wanaokiuka maadili na kuchafua sifa nzuri za jeshi hilo.

Akifafanua zaidi kuhusu changamoto hiyo, Rais Magufuli alisema baadhi ya askari hao wamewajibishwa kutokana na makosa mbalimbali yakiwamo vitendo vya kushiriki katika kutenda uhalifu ukiwamo ujambazi na rushwa.

Alimtaka IGP Sirro kutokubali wachache walioko katika jeshi hilo, kuchafua heshima na sifa ya jeshi hilo ambalo yeye analiamini na wananchi wanalikubali kwa utendaji wake mzuri.

"Ninapongeza kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi kwani vitendo vya uhalifu ukiwamo ujambazi, hata mkoani Geita, vimepungua sana kama ambavyo pia wananchi wana imani na Jeshi la Polisi kwa uadilifu na utendaji wake," alisema.


"Kuna askari wachache tu ambao wamekuwa wakichafua sifa na heshima ya jeshi, hao wasipewe nafasi. Sirro washughulikiwe hao wachache," Rais Magufuli aliagiza.

Alisema wapo baadhi ya askari polisi wasio waadilifu, wanashirikiana na majambazi kufanya uhalifu, kubambikiza kesi wananchi wasio na makosa.

Alisema askari wa aina hiyo lazima washughulikiwe ili kutochafua taswira ya Jeshi la Polisi na kulishusha hadhi mbele ya umma. Mradi wa ujenzi wa nyumba 400 za askari ulianza Aprili 7 jijini Arusha wakati wa maadhimisho ya kumbukumbu ya kifo cha Rais wa kwanza wa Zanzibar, Amani Abeid Karume.

Katika maadhimisho hayo, Rais Magufuli alitoa Sh. bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya askari polisi, mradi ambao ulianza kutekelezwa baada ya fedha hizo kutolewa.

Kabla ya uzinduzi huo wa nyumba 20 jana, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola na IGP Sirro walimweleza Rais Magufuli kuwa askari kutoishi kambini ni changamoto inayoweza kukwamisha utekelezaji wa shughuli za kila siku za jeshi hilo.



Sehemu ya nyumba za askari polisi zilizozinduliwa na Rais John Magufuli mkoani Geita jana. **PICHA: IKULU**

# JPM atoa neno uchaguzi mitaa

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

RAIS John Magufuli amewataka Watanzania kuchagua viongozi bora na wasiotoa rushwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Rais Magufuli alitoa rai hiyo jana alipokuwa anawasalimu wananchi wa Kata ya Nyankumbu mjini Geita baada ya msafara wake kusimama kutokana na umati mkubwa wa watu waliotaka kusikia neno kutoka kwa kiongozi wao huyo.

Alisema wananchi wanapaswa kuutumia uchaguzi huo kuwachagua viongozi bora ambao hawatawashawishi kwa rushwa na watakuwa mstari wa mbele katika vita dhidi ya rushwa.

Rais Magufuli alisema serikali ya awamu ya tano inahitaji viongozi bora, wachapakazi na wanaochukia vitendo vya rushwa.

"Ndugu zangu wananchi, mwaka huu ni kipindi cha uchaguzi wa kuchagua viongozi wa serikali za vijiji, vitongoji na mitaa, chagueni viongozi bora na siyo bora viongozi, chagueni wasiotoa rushwa na wawe viongozi watakaoweza kuzuia rushwa," alisema.

Rais Magufuli pia aliwataka wananchi kutokubali kugawanya na itikadi za kidini na kisiasa, badala yake waendelee kudumisha amani na mshikamano nchini.

## TIB yatuliza wateja wake

**Na Salome Kitomari**

BENKI ya TIB Corporate imewatoa wasiwasi wateja wake nchini kuwa haiko chini ya usimamizi wa benki bali mabadiliko ya uongozi wa juu yaliyofanywa ni ya kawaida.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, Fred Luvanda, wataendelea kutoa huduma kama kawaida kwa ubora na ufanisi wa hali ya juu.

Kabla ya uteuzi huo Luvanda alikuwa Msimamizi wa Sekta ya Fedha, na taarifa iliyotolewa juzi na BoT, ilieleza kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Frank Nyabungege, amesimamishwa kwa kile kilichoelezwa ni mwenendo usioridhisha wa benki hiyo.

"Tunawatoa wasiwasi wateja na wadao wote wa benki ya Biashara TIB na wananchi kwa ujumla, wajue kuwa huduma zinaendelea kama kawaida," alieleza na kuongeza:

"Pia mfahamu kuwa serikali na Benki Kuu inatambua umuhimu wa benki hii, itaendelea kitoa ushirikiano wa karibu ili kuhakikisha benki inazidi kuboresha huduma zake na kukua kwa maendeleo ya nchi yetu."

Aidha, aliitaka menejimenti na wafanyakazi kuendelea kufanyakazi kwa bidii ili kuhakikisha benki inatimiza malengo yake.

TIB Corporate inamilikiwa na serikali, na inatoa huduma zote za kibenki za kibiashara kwa mashirika na taasisi za aina mbalimbali za serikali na binafsi.

Benki hiyo ina matawi saba kwa sasa ya Dar es Salaam matatu, Mwanza, Arusha, Mbeya na Dodoma.

## Wauguzi wakumbushwa wajibu

**Na Romana Mallya**

MHADHIRI Msaidizi kutoka Chuo Kikuu cha St. John's kilichopo Dodoma, Faraja Mpemba, amewakumbusha wauguzi kuwa wanaowahudumia hospitalini ni wateja wao hivyo wanatakiwa kutumia lugha nzuri.

Mpemba aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika maonyesho ya vyuo vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) na kushirikisha vyuo mbalimbali nchini.

Akizungumzia kuhusu lugha zinazotakiwa kutolewa kwa wagonjwa, Mpemba alisema wanapotoa mafunzo vyuoni huwafundisha wanafunzi kuwa wanaowahudumia siyo wagonjwa bali wateja.

"Tunawaita wateja kwa sababu ndiyo wanaotufanya tuwepo kazini, unapomuhudumia mteja wako unatakiwa uwe na lugha ambayo itamfanya siku nyingine akiwa na shida arudi kwako," alisema.

Mpemba alitoa wito kwa watoa huduma za afya wakiwamo wauguzi kuhakikisha wanatumia elimu walizopata vyuoni kuwahudumia wateja wao vizuri.

HABARI KITAIFA



Wanafunzi waliomaliza kidato cha sita ambao wanatarajia kujiunga na vyuo vikuu wakiangalia kozi mbalimbali katika banda la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere katika maonyesho yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu nchini, yanayofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Watano mbaroni mauaji ya Watanzania Msumbiji

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

JESHI la Polisi nchini limesema watu watano wamekamatwa wakituhumiwa kuhusika na mauaji ya Watanzania tisa Msumbiji mwezi uliopita.

Usiku wa kuamkia Juni 28, mwaka huu, Watanzania tisa waliripotiwa kuuawa kwa kupigwa risasi na wengine sita kujeruhiwa Msumbiji baada ya kuvamiwa wakiwa kwenye mashamba yao ya mpunga na watu waliovalia sare zilizodaiwa kufanana na za Jeshi la Msumbiji.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP) Simon Sirro, wakati wa uzinduzi wa nyumba 20 za askari polisi mkoani Geita, alimweleza Rais John Magufuli kuwa hakuna damu ya Mtanzania itakayomwagika bure.

IGP Sirro alibainisha kuwa kati ya watuhumiwa watano waliokamatwa, mmoja amefariki dunia na uchunguzi wa kina bado unaendelea. Alisema Jeshi la Polisi litahakikisha raia wote na mali zao wanalindwa na ndiyo sababu baada ya kupata taarifa za mauaji ya Watanzania Msumbiji, mara moja lilichukua hatua kuwasaka wahusika.

"Hadi sasa, tunawashikilia watuhumiwa watano na mmoja kati yao, ametangulia mbele ya haki... na upelelezi bado unaendelea na wanaendelea kutajana wao kwa wao, hivyo zoezi hilo lipo katika hatua nzuri Mheshimiwa Rais.

"Na imebainika mchezo na mkakati wote wa kupanga njama za mauaji hayo ulifanyika Tanzania," IGP Sirro alisema.

Akizungumzia hatua hiyo, Rais John Magufuli alilipongeza jeshi hilo kwa utendaji wake na kulihakikishia kuwa Watanzania wengi wana imani nalo pamoja na majeshi mengine yalipo nchini.

## TPSF kutumia fursa kusaka masoko

**Na Beatrice Moses**

SEKTA binafsi wamejiandaa kutumia vyema fursa ya maadhimisho ya awamu ya nne ya Wiki ya Maonyesho ya Viwanda yanayokwenda sambamba na mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi wa Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyekiti na mwenyeji wa mkutano huo, ambao utahudhuriwa na Wakuu wa Nchi wa Serikali kutoka nchi 16 na wanachama wa SADC, utatanguliwa na maonyesho hayo.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa Sekta Binafsi

INAENDELEA UK.8

# Madaktari bingwa watoa mafunzo huduma saratani, upandikizaji

**Na Mary Geofrey**

WATAALAMU kutoka Hospitali ya Chuo Kikuu Oxford nchini Uingereza, wameanza kutoa mafunzo kwa madaktari bingwa wa damu, saratani na wauguzi jinsi ya kuhudumia wagonjwa wa saratani na watakaopandikizwa uloto.

Hatua hiyo ni mwendelezo wa maandalizi ya kutoa huduma ya upandikizaji uloto kwa mara ya kwanza nchini, matibabu ambayo yalikuwa hayapatikani kutokana na kutokuwapo wataalamu au ukosefu wa vifaa vya kutolea huduma husika.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Kitengo cha Mafunzo, Ushauri na Utafiti, Dk. Faraja Chiwanga, alisema mafunzo hayo ambayo yameanza kutolewa Muhimbili yanahusisha madaktari bingwa 20 wa magonjwa ya damu na saratani na zaidi ya wauguzi 30.

Alisema Juni, mwaka huu, Muhimbili ilipeleka wataalamu 11 India katika Hospitali ya Apollo kwa kipindi cha mwezi mmoja, ili kujifunza kwa vitendo jinsi ya kufanya upandikizaji wa uloto.

"Uwapo wa huduma hii utasaidia wananchi wengi kutibiwa nchini, kujenga uwezo kwa wataalamu wa ndani na itapunguza mzigo kwa serikali kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa sababu gharama za kufanya upasuaji nchini zitashuka kwa zaidi ya asilimia 50 kwa mgonjwa mmoja," alisema Dk. Chiwanga.

Alisema wagonjwa wenye tatizo hilo walikuwa wakipelekwa nje ya nchi na kutibiwa kwa gharama ya Sh. milioni 200, hivyo kwa MNH mgonjwa atagharimiwa chini ya asilimia 50.

Dk. Chiwanga alisema wataalamu hao ni pamoja na madaktari bingwa watatu wa magonjwa ya damu, wataalamu wa maabara watatu, wahandisi watatu mmoja wa ufundi, ujenzi na vifaa tiba na mtaalamu wa fedha ili kufanya uchambuzi wa gharama halisi za huduma hiyo na mtaalamu wa ununuzi kufanya uchambuzi yakinifu wa dawa na vitendanishi.

Alisema wataalamu hao wanatarajia kurejea nchini mwishoni mwa mwezi huu kwa ajili ya kuanza maandalizi ya mwisho ya kutoa huduma hiyo mwishoni mwa mwaka huu.

"Tayari wauguzi watatu, wataalamu wa saratani ya watoto watatu, mfamasia mmoja na wataalamu wengine wawili wa damu wamepata mafunzo ya huduma hiyo katika Hospitali ya Apollo, India kwa kipindi cha miezi mitatu," Dk. Chiwanga alisema.

### NAMNA YA KUPANDIKIZA

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Prof. Lawrence Maseru, Dk. Chiwanga alisema huduma hiyo hufanyika kwa kupandikiza chembechembe mama za kuzalisha damu ambazo hupatikana kwenye uloto au chembechembe mama kutoka kwenye kitovu cha mtoto mchanga au kondo la nyuma la mama.

"Njia ambayo hutumika mara nyingi ni ile ya upandikizaji wa chembechembe mama za damu (HSCT) kutoka kwenye uloto.

Upandikizaji huu unaanza kwa kumwandaa mgonjwa ambaye chembechembe zake za damu zina tatizo kama saratani, selimundu au wale ambao mifupa yao inashindwa kuzalisha damu," alisema mtaalamu huyo.

Alifafanua kuwa upandikizaji huo hufanyika kwa kuwapa tiba maalum ili kuua chembechembe zote zenye matatizo kisha kupandikiza chembechembe mpya zilizomo kwenye uloto kutoka kwa ndugu mwenye vinasaba vinavyofanana au chembechembe mpya zilizozalishwa kutoka kwa mgonjwa mwenyewe baada ya kupata tiba maalum.

Dk. Chiwanga alisema huduma hiyo ndiyo tiba pekee inayoweza kuponya wagonjwa wenye matatizo hayo.

Kwa mujibu wa takwimu za Muhimbili, wagonjwa takribani 130 hadi 140 wanahitaji huduma ya kupandikizwa uloto kwa mwaka na zaidi ya theluthi mbili ya wagonjwa hao hufariki dunia kwa kukosa huduma hiyo.


BONITE BOTTLERS LIMITED

Advertisements of Employment

1. Microbiologist

**Qualification:**

- Applicant should be a holder of Diploma or Bachelor in Microbiology or relevant qualification from any recognized Institution.

**Key skills & Abilities:**

- Ability to prepare micro lab, do sampling, analysing, interpreting and updating result for all production lines.
- Ability to make analysis of transport related issue and prepare report.
- Able to work independently with minimum supervision.
- Self motivated and flexible person and a good team player.

**Experience :**

Any relevant experience will be added advantage

**Mode of Application:**

All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to the undersigned address, to reach him not later than **23/07/2019.**

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**MOSHI**

21532602

## HABARI KITAIFA

# Kortini tuhuma utakatishaji fedha

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI watatu wa jijini Dar es Salaam wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo wizi na kutakatisha zaidi ya Sh. milioni 507 za kilo 6.244 za dhahabu.

Washtakiwa hao ni mkazi wa Kigamboni, Donald Njonjo (30), wa Tandika, Gamba Muyemba (51) na wa Upanga, Kashif Mohammed (41).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kelvin Mhina.

Wakili wa Serikali Jacqueline Nyantori alidai kuwa washtakiwa wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi yakiwamo mashtaka manne.

Alidai kuwa kati ya Novemba 30, 2017 na Juni, 29, mwaka huu, katika ofisi ya Kamishna wa Madini iliyoko Masaki, Wilaya ya Kinondoni waliiba kilo 6.244 za dhahabu yenye thamani ya Sh. 507,347,000 mali ya serikali ya Tanzania.

Alidai shtaka la pili, linamkabili mshtakiwa wa tatu, Mohammed kwamba Julai 8, mwaka huu, mtaa wa Indira Gandhi, Ilala jijini Dar es Salaam, alikutwa na gramu 2794.5 za dhahabu yenye thamani ya Dola za Marekani 121,155.45 (sawa na Sh.278,714,478.06) baada ya kuiba katika ofisi ya Kamishna wa Madini.

Nyantori alidai katika shtaka la tatu, washtakiwa wote, kati ya Julai Mosi na Novemba 31, mwaka jana Ilala jijini Dar es Salaam, walikutwa wakiwa na madini hayo bila kibali.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa kuwa kati ya Julai Mosi na Novemba 31, mwaka jana, washtakiwa wote kwa pamoja, mahali tofauti, walijihusisha na kuhamisha dhahabu yenye uzito wa kilo 6.244 ikiwa na thamani hiyo huku wakijua imepatikana kwa njia ya wizi.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi mpaka pale Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) atakapotoa kibali.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo kuomba tarehe ya kutajwa kesi hiyo.

Hakimu Mhina alisema kesi hiyo itatajwa Julai 29, mwaka huu na washtakiwa wapelekwe mahabusu.

# Makamu Rais akemea vizuizi kwa walemavu

**Na Dege Masoli,** LUSHOTO

KATIKA kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 kwa kuhakikisha wanawake na wanaume wenye ulemavu wanakuwa sehemu ya uzalishaji katika jamii, serikali imesema Tanzania imechukua hatua madhubuti ya kuondoa changamoto zinazolikabili kundi hilo kwenye maeneo ya elimu na afya.

Imeeleza kuwa hatua hizo zimechukuliwa kutokana na kuwa na sera ya taifa kuhusu ulemavu ya mwaka 2004 na baadaye kutungwa kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010.

Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aliyasema hayo alipofungua mkutano wa siku tatu wa Kongamano la 16 la Chama cha Kimataifa cha Elimu Maalum (IASE). Alisema itafanyia kazi mapendekezo yote yatakayotolewa na wadau na washiriki mbalimbali katika kongamano hilo kwa manufaa na mustakabali wa watu wenye ulemavu.

Mkutano huo umeandaliwa na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Askofu Sebastian Kolowa (Sekomu) kinachomilikiwa na Kanisa la Kiinjili Kilutheri (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini kwa kushirikiana na IASE.

Makamu wa Rais alisema watu wenye ulemavu wanatambuliwa kwa mujibu wa katiba inayotamka bayana kuwa watu wote wako sawa na kila mtu ana haki ya kuheshimiwa.

Alisema Tanzania kwa kuheshimu katiba, imefanya juhudi kuhakikisha watu wenye ulemavu wanalindwa kwenye jamii kutokana na aina ya ulemavu walio nao.

Alisema serikali ya awamu ya tano inatambua haki za walemavu kwenye suala la elimu na imeboresha miundombinu ya shule kwa ajili ya kujifunzia, kuweka mazingira rafiki kutokana na aina ya ulemavu wao, kutoa vifaa saidizi vya kujifunzia na kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wanaotoa elimu kwa makundi maalum.

"Jamii inapaswa kutambua mahitaji na kuondoa vizuizi na matabaka kwa watu wenye ulemavu kwa kuwawekea mazingira wezeshi, kutoa taarifa na changamoto zinazowakabili watu wenye ulemavu," alisema.

"Sisi kama serikali tunakubaliana na kuungana na jumuiya za kimataifa kwa kuchukua hatua na kutekeleza mikakati, sheria na kazi mbalimbali katika kutatua changamoto zinzaowakabili watu wenye ulemavu."

Makamu wa Rais aliushukuru uongozi wa Sekomu kwa kuandaa mkutano huo na kuahidi serikali kuyachukua na kuyafanyia kazi mapendekezo yatakayofikiwa.

Mbali na Makamu wa Raism, mkutano huo pia ulihudhuriwa na Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, maofisa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na washiriki kutoka nchi 23 za mataifa mbalimbali duniani.


**UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED**
**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES**

| S/N | ITEM/TRANSACTION | | |
|---|---|---|---|
| SECTION A | SAVINGS ACCOUNTS | RETAIL | CORPORATE |
| 1 | FREEDOM SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 5,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 2 | GENERAL SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | EMPLOYEE SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Adhoc statement request | TZS 1,000/ PAGE | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | SAVINGS ACCOUNT SALARY | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 5 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| | Closing account | USD 5 | |
| 7 | U-CARE CHILDREN SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| SECTION B | CURRENT ACCOUNTS | | |
| 1 | INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT | | BUSINESS CURRENT ACCOUNT |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 10,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenence fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Closing account | TZS 10,000 | TZS 10,000 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 10% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | DIPLOMAT ACCOUNTS | | |
| | Required minimum opening balance | USD 200 | N/A |
| | Minimum operating balance | USD 100 | N/A |
| | Monthly maintenence fee | NIL | N/A |
| | Cash withdrawal at counter | NIL | N/A |
| | Closing account | NIL | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | NIL | N/A |
| | Outward fund transfers(TTs) | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | N/A |
| | Inward fund transfers(TTs Incoming) | NIL | N/A |
| | FOREX exchange | Favourable rates will be applied | N/A |
| 3 | DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenence fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Closing account | USD 10 | USD 10 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION C | DEPOSIT ACCOUNTS | | |
| 1 | Call Accounts | | Call Accounts |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | Term Deposits | | Term Deposits |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION D | ELECTRONIC BANKING | | |
| 1 | E-Banking | | E-Banking |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | TZS 5000 | TZS 5000 |
| | U - Direct (Reversal of transaction) | TZS 4000 | TZS 4000 |
| | E-statement (self downloaded) | FREE | FREE |
| | POS purchase (Local) | FREE | N/A |
| | POS purchase (International) | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| | ATM reversal | TZS 1,000 per transaction | N/A |
| | Fund transfer/ company load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Card Load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Manual pin change | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per transaction |
| | U-MOBILE(mobile banking-Bank to wallet) | TZS 1,000 (0 - 200,000/=) and TZS 2,000 (200,001 - 400,000/=) | N/A |
| | Card to card transfer | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per tr |
| | Africash | TZS 6000 + 1.5% of the amount sent/USD 4.45 + 1.5% | N/A |
| 2 | Visa Debit Card | | N/A |
| | Issuance fees | TZS 10,000 | |
| | Re-issuance fee | TZS 10,000 | |
| 3 | Visa Perapid Cards | | N/A |
| | Issuance fees for instant card | TZS 12,000 | |
| | Issuance fees for personalized card | TZS 16,000 | |
| | Re-issuance fees | TZS 12,000 | |
| | Online Passcode reset fee | TZS 1,500 | |
| | ATM Pin reset fee | TZS 1,500 | |
| | Loading fee | TZS 1,000 | |
| | Online shopping fee - Local transactions | FREE | N/A |
| | Online shopping fee/Web - Int. transactions | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| 4 | ATM Withdrawals | | N/A |
| | At UBA ATMs (On us) | TZS 500 | |
| | ATM Balance inquiry(Local) | TZS 200 | |
| | ATM Balance inquiry(international) | TZS 1000 | |
| | To other banks ATM (On others/OFF US)Local | TZS 2,500 | |
| | international ATM withdraw | TZS 6000 | |
| SECTION E | ASSET BANKING | | |
| 1 | LOANS | | |
| | Processing fee | negotiable | 2% |
| | Insurance for personal loans | N/A | 1.50% |
| | Legal fees | 0.5% minimum of TZS 300,000 | 0.5% minimum of TZS 300,000 |
| 2 | TEMPORARY OVERDAFT (TODs) | | |
| | Processing fee | 2% | 2% |
| SECTION F | TRADE FINANCE | | |
| 1 | Guarantees | | Guarantees |
| | Facility Commission | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qrt. | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qtr. |
| | Arrangement fees | 2% | 2% |
| | Cash Covered | 0.5% per qtr Min 250 per qtr | 0.5% per qtr Min 250 per qtr |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| | Extension to next quarter | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) |
| | Amount increase | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) |
| 2 | Letters of Credit - Imports | | Letters of Credit - Imports |
| | Issuance commision | 0.5% per quarter. Min USD 150. | 0.5% per quarter. Min USD 150. |
| | Handling Fees | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| 3 | Letters of Credit - Exports | | Letters of Credit - Exports |
| | LC Advising Commission | USD 200 flat | USD 200 flat |
| | Amendment advising commision | USD 100 Flat | USD 100 Flat |
| | Correspondences Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Documents handling and examination fee | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 |
| | Courier charge | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | LC confirmation charges | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) |
| 4 | Letters of Credit Refinancing | | Letters of Credit Refinancing |
| | Interest on refinance | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on refinance | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 5 | Discounting on LC/Invoice/Cheque | | |
| | Interest on discounting | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on discounting | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 6 | Bills Discounting (Bills of exchange including cheques) | | |
| | Interest on discounting | PLR +3%-local; International Lobor+8% | PLR +3%-local; International Lobor+8% |
| 7 | Documentary Collection - Export | | |
| | Handling charge | 0.25% of the invoice min USD 100 flat | 0.25% of the invoice min USD 100 flat |
| | Courier charge | USD 100 | USD 100 |
| | Corespondence commission | USD 50 Per tracer | USD 50 Per tracer |
| 8 | Documentary Collection - Import | | |
| | Handling Commission | 0.25%. Min USD 100 | 0.25%. Min USD 100 |
| | correspondence Swift charge | USD 50 | USD 50 |
| 9 | Outward Bills for Collection (clean collections & TCs) | | |
| | Handling Commision | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent |
| | Dhl charges | usd 75 flat | usd 75 flat |
| | Returned foreign cheques | claimed charges + locally un re-covered charges | claimed charges + locally un re-covered charges |
| 10 | Inward Bills for Collection | | |
| | Handling Commission | USD 50 flat per collection | USD 50 flat per collection |
| | Swift charged | USD 40 flat per collection | USD 40 flat per collection |
| 11 | Local Currency Transactions | | Local Currency Transactions |
| | Outward remittances (TISS) | TZS10,000 PER TRANSACTION | TZS10,000 PER TRANSACTION |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT |
| | Inward Swift Transfers (TISS) | NIL | NIL |
| 12 | Foreign Currency Transactions | | Foreign Currency Transactions |
| | Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 |
| | Telegraphic Overseas Charges/ OURS | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | Inward Swift Transfers | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | International Money Order (IMO) | USD 30 per IMO | USD 30 per IMO |
| | Foreign cheques for collection | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; |
| SECTION G | OTHERS | | |
| 1 | Statements | | Statements |
| | Monthly | FREE | FREE |
| | Adhoc requests | TZS 1,000/ PAGE | TZS 1,000/ PAGE |
| 2 | Cheque Books Issuing | | Cheque Books Issuing |
| | - 25 Leaf | TZS 15,000; USD 10 | N/A |
| | - 50 Leaf | TZS 30,000; USD 20 | N/A |
| | - 100 Leaf | TZS 45,000; USD 30 | TZS 45,000; USD 30 |
| | Counter cheque request | TZS 20,000; USD 10 | TZS 20,000; USD 10 |
| | Cheque Stop payment instructions | leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; | Leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; |
| | Issuance of Manager's cheque | TZS 25,000; USD 20 per item | TZS 25,000; USD 20 per item |
| | Managers cheque cancellation charges | FREE | FREE |
| 3 | Standing order | | Standing order |
| | Standing order set-up | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Standing order maintanance | NIL | NIL |
| | Standing order/Foreign Bank (TT charge) | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 |
| | Amend / Stop standing Order | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Unpaid standing order | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent |
| 4 | Insufficient funds/effects not cleared | | Insufficient funds/effects not cleared |
| | Effects not cleared | **ITEM REMOVED** | **ITEM REMOVED** |
| | Insufficient Funds (Refer to drawer) | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| 5 | Other services/charges | | |
| | Retriving old documents (2-6 months) | TZS 10,000; USD 10 | TZS 10,000; USD 10 |
| | Retriving documents (6 months and above) | TZS 15,000; USD 15 | TZS 5,000; USD 15 |
| | Confirmation/Audit/ Certificate of balance | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent |
| | Status enquiry / Reference Letters | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent per customer request | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent |
| | Manual processing of salaries | TZS 1,000; USD1 or its equivalent | TZS 1,000; USD1 or its equivalent |
| | Closure of Account | TZS10,000 | TZS10,000 |
| | Dormant Account Reactivation | FREE | FREE |
| | Cash handling fee-COINS ONLY | 9% of the Deposit | 9% of the Deposit |
| 6 | Soiled notes | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| 7 | Coins | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| | | | |
| | **approved by:** | | |
| | **Signature:** | | **Signature:** |
| | | | |
| | Flavia Kiyanga | | Chomete Hussein |
| | **Chief Operating Officer** | | **Country Chief Finance Officer** |
| | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** |
| | **Disclaimer: All fees are VAT exclusive.** | | |

215324602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wakurugenzi wasipige chenga kujibu hoja za CAG

**MKUU** wa Mkoa wa Pwani, Everist Ndikilo, amewaka wakurugenzi na wakuu wa idara katika wilaya za mkoa huo kuacha tabia ya kuwakaimisha watumishi kuingia katika mikutano ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Selikari,(CAG) kujibu maswali yanayohusu ofisi zao.

Kauli hiyo ya Ndikilo aliitoa katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, ambacho kiliandaliwa kwa ajili ya kujibu hoja 32 za nje za CAG.

Hiyo ni kauli nzito ambayo inaonyesha kuwa Mkuu wa mkoa huyu yupo makini, kwa kuwa hayupo tayari kuona uzembe, ujanja ujanja unafanywa na watendaji wake.

Tunasema hivyo, kwa kuwa kumekuwapo na matukio kadhaa ya viongozi wenye dhamana katika halmashauri zetu ambao ni wakurugenzi na wakuu wa idara kukaimisha nafasi zao kwa wasaidizi wao, hivyo wakati mwingine kujikuta wanakwenda kujibu hoja mbalimbali za ukaguzi wa CAG, kuhusiana na matumizi ya fedha za walipakodi.

Hakusita kuwaeleza anachotaka ni kuwa wakuu wa idara na wakurugenzi wajibu mambo wanayoyasimamia badala ya kukwepa au kutioichukulia umuhimu mikutano ya kujibu hoja za CAG. Ni wazi kwamba kuwa hoja za CAG zinahitaji majibu sahihi yasiyotia shaka, yawezekana pia zimechangia halmashauri kupata hati chafu.

Hati chafu husababisha maswali mengi ikiwamo ofisi husika kuonekana ina watendaji ambao wanadokoa ama 'wanatafuna' fedha za umma kama vile mchwa.

Ndikilo kuipongeza Halmashauri ya Wilaya Mkuranga kwa kupata hati safi mara tatu mfululizo, akieleza kuwa hatua hiyo inaonyesha jinsi viongozi husika walivyo na ushirikiano mzuri wa kusimamia fedha za maendeleo kiufasaha.

Alisema halmashauri wilaya zote za mkoa wake zimefanikiwa kupata hati safi hali inaonyesha jinsi ilani ya chama tawala (CCM) inatekelezwa katika kusimamia masuala ya maendeleo.

Tunatambua kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Dira ya CAG ni Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za serikali na taasisi za umma.Dhamiri Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma

Pia imekusudiwa kuimarisha ubora wa utoaji huduma kwa kuchangia ubunifu kwa matumizi bora ya rasilimali za umma, pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau wetu kuhusu mapungufu katika uendeshaji wa shughuli zao.

Miaka kadhaa tumekuwa tukishuhudia ripoti ya CAG ikiibua madudu yanayofanywa na baadhi ya halmashauri ambayo yamekuwa yakitokana na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Tunategemea kwamba wakuu wengine wa mikoa wataungana na Ndikilo katika kuwahimiza wakuu wa idara kwenye halmashauri zao kutambua umuhimu wa kutoa ushirikiano wa kufanikisha ripoti ya CAG.

Kwa kufanya hivyo, itasaidia halmashauri kuwa na maendeleo kwa kuwa kila kiongozi atahakikisha anatumia fedha aliyopewa ya idara iwe kwa ajili ya miradi ya huduma au maendeleo inatumika ipasavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Rais Magufuli afanye maamuzi pamba ya wakulima inunuliwe

Na Raphael Kibiriti

**CHANGAMOTO** ya kutonunuliwa kwa pamba ya wakulima nchini ilipofikia kwa hivi sasa, ni dhahiri kwa maoni ya Muungwana kwamba ni Mtanzania namba moja kwa maana ya Rais John Magufuli ndiye ambaye anaweza 'kuokoa jahazi' hili.

Ikiwa inaelekea kuwa takribani mwezi wa tatu sasa toka kuzinduliwa kwa msimu wa ununuzi wa zao la pamba nchini Mei 2 mwaka huu, bado kampuni zilizopitishwa kununua zao hilo kwa sehemu kubwa hazijaanza kufanya hivyo.

Taarifa kutoka maeneo mbalimbali ya mikoa kunakolimwa zao hili zinabainisha kwamba bado wakulima wanaendelea kubaki na pamba yao majumbani mwao, na kwenye maghala ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) ambayo ilikuwa imeshapelekwa tayari.

Hivyo wakulima hawa ambao kwa kweli ni sehemu kubwa ya Watanzania takribani milioni 55 kwa maana ya eneo linalolima zao hili wanaendelea kupaza kilio chao, wakitaka pamba yao inunuliwe.

Wanapaza sauti zao kwa sababu kuwa wengi miongoni mwao kilimo ndiyo maisha yao na pamba ndiyo chanzo chao kikuu cha mapato ya kiuchumi na hivyo ustawi wao kwa ujumla.

Hivyo kuna wale ambao walitegemea kuwa wameuza pamba yao muda mrefu, siku za mwanzo za kuzinduliwa kwa msimu wa ununuzi, lakini hawajafanya hivyo kutokana na wanunuzi kusuasua kununua zao hilo.

Muungwana amezungumzia changamoto hii kwa takribani mwezi sasa, akisisitiza jitihada za makusudi zichukuliwe ili pamba ya wakulima inunuliwe kwa lengo la kuwawezesha kujiletea maendeleo yao.

Maendeleo ambayo mbali na kugharimia mahitaji yao ya msingi kama vile ununuzi wa vyakula, kugharimia mahitaji mbalimbali ya familia zao, yanawawezesha pia kujenga ama kuboresha makazi yao na kununua vyombo vya usafiri.

Kuna sababu mbalimbali zinazoelezwa ni kwa nini ununuzi wa zao hilo unasuasua, baadhi zikiwa ni pamoja na madai kutoka kwa kampuni za ununuzi kwamba bei ya Sh. 1,200 iliyowekwa na serikali ni kubwa.

Ni kubwa kwa maana 'haiwalipi' kufuatana na bei ya zao hilo katika soko la dunia, kwamba bei imeporomoka sana.

Kwamba kutokana na kushuka huko kwa bei katika soko la dunia, hata benki nchini zinasita kuwakopesha wanunuzi wa zao hilo zikihofia kuwa hawataweza kurejesha mikopo na kwa maana hiyo ndiyo huo mchezo wa kusuasua kwa ununuzi wa pamba.

Na ndiyo sababu nikaanza katika Tulonge yangu leo kwamba kuna haja sasa ya Rais Magufuli kufanya kazi yake ya 'kuokoa jahazi' hili la wakulima wa pamba.

Nimembainisha yeye kwa sababu ana historia ya kutatua changamoto za aina hii zinazowakumba wananchi wake na hasa wanyonge kama wakulima hawa wa zao la pamba.

Kwa mfano Novemba mwaka jana, Rais Magufuli aliingilia kati sakata la korosho ambalo linaonekana kufanana na hili la pamba.

Wanunuzi wa korosho nchini walisuasua kununua korosho wakitaka wainunue kwa bei ya chini ya Sh. 3,000 kwa kilo, hali iliyosababisha Rais Magufuli kuamuru serikali inunue korosho kwa wakulima kwa bei ya Sh. 3,300 ambayo ilikuwa na tija kwa wakulima.

Aidha, Desemba mwaka jana, Rais Magufuli alifuta kikokotoo cha mafao baada ya mfanyakazi kustaafu kilichokuwa kimependekezwa katika Kanuni za Sheria ya Mifuko ya Jamii ambacho kilikuwa kinalalamikiwa na wafanyakazi.

Kikokotoo hicho kipya kilikuwa kimeleta mkanganyiko na taharuki miongoni mwa wafanyakazi na hata wengine kukata tamaa.

Hivyo Rais Magufuli akaagiza kanuni ya mafao iliyokuwa ikitumika zamani kabla ya mifuko ya hifadhi kuunganishwa iendelee kutumika.

Ni kwa historia hiyo Muungwana ana maoni kwa Rais Magufuli kuokoa jahazi hili la wakulima, ili pamba yao inunuliwe na hivyo kuboresha ustawi wao.

## HABARI KITAIFA

# Chuo cha Mwalimu Nyerere chasisitiza maadili

**Na Romana Mallya**

CHUO cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere (MNMA) kilichoko Kigamboni jijini Dar es Salaam, kimetumia maonyesho ya vyuo vikuu yanayoendelea jijini kuwasisitizia wadahiliwa wapya vyuo vikuu kuzingatia maadili ili kupata viongozi bora watarajiwa.

Mkuu wa Idara ya Diploma ya Uzamili chuoni hapo, Dk. Philip Dalinga, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maonyesho yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Dk. Dalinga ambaye pia ni Kaimu Mwenyekiti wa maonyesho, alisema MNMA inatoa mafunzo ya aina mbalimbali kuanzia ngazi ya cheti hadi shahada ya umahiri.

"Vijana wanaokuja hapa tunawajulisha kuhusu chuo hiki na mafunzo yanayotolewa lakini pia tunasisitiza sana suala la maadili," alisema.

Pia alisema chuo hicho wakati kikitoa mafunzo ya kozi mbalimbali, msisitizo mkubwa ni maadili ili taifa lipate watendaji waadilifu.

"Tunahitaji vijana wanaomaliza wawe waadilifu. Wanapomaliza masomo yao warudi wakafanye kazi lakini kwa uadilifu, wakawe wafanyabiashara waadilifu na Watanzania waadilifu," alisema.

Pia alisema pamoja na kozi mbalimbali watakazosoma chuoni hapo, watasoma maadili na uongozi, utawala na lugha ya Kichina.

"Tumeanza na lugha ya Kichina kwa sababu ya umuhimu wa lugha hiyo kwa kuwa wenzetu China wamefika mbali katika suala la uchumi, biashara na teknolojia. Pia Watanzania wengi wanakwenda China kwa ajili ya biashara, ndiyo maana tumeamua kufundisha iwe kama nyenzo ya maisha ya biashara na ajira," alisema.



Wanawake wakifua nguo kandokando ya mto kutokana na kukosekana kwa mabomba ya maji safi na salama kwa matumizi katika eneo la Goba, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

## Programu kuwezesha masoko, kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

PROGRAMU ya kuendeleza mifumo ya masoko katika kilimo (AMDT), imeanza kuwajengea uwezo viongozi mbalimbali wa ngazi za wilaya na mikoa ili kuongeza chachu ya kufanya mijadala baina ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Aidha, lengo ni uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara katika maeneo yao.

Utekelezaji wa hatua hii unaanza ukiwa takribani mwezi mmoja tangu Rais John Magufuli, azitake serikali za mitaa kutilia mkazo mabaraza ya biashara kwenye maeneo yao.

Katika mkutano uliofanyika wilaya ya Babati mkoani Manyara na kuwakutanisha wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, wenyeviti wa mabaraza ya biashara wa mikoa ya kutoka wilaya za mikoa ya Singida na Manyara, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, alivitaka vyombo vya kutunga sheria kuwashirikisha wadau wote wa sekta binafsi.

Katika hotuba yake iliyosomwa na Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, alisema ipo haja kwa mamlaka zinazosimamia utungaji wa sheria katika ngazi za wilaya, miji na majiji kuhakikisha zinawashirikisha wadau muhimu, hususani kupitia mabaraza ya biashara.

"Tuna changamoto kubwa sana ya fursa ya ajira, kati ya wahitimu zaidi ya 400,000 wanaohitimu kila mwaka ni asilimia kumi ndio hupata ajira, hivyo tunajukumu kuhakikisha kupitia mabaraza ya biashara tunatengeneza fursa ny-

INAENDELEA UK.8




# Shahidi asimulia mazito mauaji ya Bushiri

**Na Hellen Mwango**

SHAHIDI wa Jamhuri, Sajenti Erasto (53), amedai katika kesi ya mauaji ya Mohammed Bushiri kwamba mwanafamilia, Juma Bushiri, aliwaona washtakiwa wakimtoa nje marehemu (wakati wa uhai wake), huku wakimshushia kipigo na kuondoka naye.

Shahidi huyo alidai kuwa kwa mujibu wa maelezo ya Juma siku ya tukio saa 8:00 usiku alimwona Khalfan Omary, Salum Mwarami na Salum Said maarufu kama Muba wakitoka nyumbani kwao wakiwa na Mohammed.

Ushahidi huo ulisikilizwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji, iliyoketi chini ya Naibu Msajili, Pamela Mazengo.

Alidai kabla ya kupata maelezo hayo, Novemba 11, 2015 alikuwa ofisini kwake Polisi Oysterbay, Mkoa wa Kipolisi Kinondoni.

Alidai aliitwa na bosi wake akakabidhiwa jalada la kesi ya mauaji likiwa na maelekezo ya kuwahoji na kuandika maelezo ya mashahidi pamoja na kufuatilia taarifa ya daktari.

Alidai kuwa kwa kushirikiana na Sajenti Adamu, walifika eneo la tukio Mwananyamala Kisiwani Wilaya ya Kinondoni.

"Nilifanikiwa kupata maelezo ya mashahidi akiwamo Halima Mohammed na Juma Bushiri, ambao wote ni ndugu wa marehemu, Juma alinieleza kwamba Novemba 9,2015 aliwaona washtakiwa Salum, Khalfan na Salum wakimtoa nje ndugu yao huku wakimpiga," alidai Sajenti Erasto.

Akifafanua zaidi shahidi alidai kuwa alielezwa alipotolewa nje alipelekwa umbali wa mita 50 kutoka kwenye makazi yake mahali walipofanyia mauaji.

Alidai kuwa ripoti ya daktari inaonyesha kwamba marehemu aliuawa kwa kupigwa na kitu chenye ncha kali kilichosababisha kupoteza damu nyingi.

Alidai kuwa baada ya kupata maelezo ya mashahidi hao aliandaa jalada na kuliwasilisha kwa mwanasheria wa serikali wa Kanda ya Dar es Salaam kwa maamuzi ya kisheria zaidi.

Wakili wa Utetezi, Ramadhani Maleta, alimhoji shahidi kama ifuatavyo:

**Wakili:** Shahidi ulikuwapo eneo la tukio?

**Shahidi:** Hapana.

**Wakili:** Shahidi ulishuhudia tukio?

**Shahidi:** Hapana, tukio lilikaguliwa na watu wengine.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Novemba 9, 2015, washtakiwa walimuua kwa makusudi Mohammed Bushiri.

HABARI KITAIFA

# Waziri abatilisha marufuku ununuzi dengu

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amebatilisha agizo la kuzuiwa wafanyabiashara mkoani Shinyanga kununua zao la dengu moja kwa moja kwa mkulima.

Alisema agizo lilitolewa ni batili kwa kuwa wizara haina taarifa, na wao ndio wenye mamlaka na kutoa maamuzi, hivyo amefuta agizo hilo na mfanyabiashara ana ruhusiwa kununua zao hilo moja kwa moja kwa mkulima.

Hasunga alitangaza hatua hiyo jana mkoani hapa kwenye ziara yake ya kikazi ya kukagua ununuzi wa zao la pamba.

Alisema amesikitishwa na uwapo wa taarifa ya kupigwa marufuku wafanyabiashara mkoani humo kutonunua dengu kwa mkulima, hivyo kukemea.

"Nalipinga agizo hili la kuzuia wafanyabiashara kununua dengu moja kwa moja kwa mkulima, wakanunue hatutaki masuala kama haya yajitokeze kama ilivyokuwa kwenye pamba," alisema Hasunga.

"Maagizo haya ya kuzuia zao la dengu kununuliwa na wafanyabiashara kwenye wizara yangu ina taarifa, hivyo kuanzia sasa napiga marufuku agizo hilo," aliongeza.

Awali Mbunge wa Viti Maalumu mkoani Shinyanga, Azza Hilali, alitoa kilio cha wakulima wa dengu mkoani humo, kuwa wamekuwa wakienda kuuza zao lao kwenye vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) kama ilivyoagizwa na kuambiwa hakuna fedha bali wakopwe, tofauti na hapo awali walikuwa wakipewa fedha zao papo hapo.

Mwishoni mwa wiki, Ofisa Ushirika Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutoka makao makuu, Benjamin Mwangwala, akiwa kwenye kikao cha wadau wa zao la dengu mkoani Shinyanga, alitoa maelekezo ya serikali kuwa zao la dengu litanunuliwa na wafanyabiashara kwa njia ya mnada kupitia kwenye AMCOS.

Alisema serikali imedhamiria kumnufaisha mkulima na kumuinua kiuchumi, ndio maana imetoa mwongozo kuwa marufuku mfanyabiashara kwenda kununua zao la dengu kwa mkulima moja kwa moja, bali anapaswa akalinunue kupitia AMCOS, ambapo ndio watanunua kutoka kwa mkulima.

"Naomba wafanyabiashara wote ambao hua mnanunua zao hili la dengu mtii maagizo haya ya serikali tofauti na hapo tusije kulaumiana baadaye," alisema na kuongeza:

"Dhamira yetu ni kumnufaisha mkulima, pamoja na nyie muweze kupata bidhaa yenye ubora kwa sababu Amcos zitakuwa zinanunua bidhaa safi na siyo chafu."

"Zao hili pia litakuwa linauzwa na vyama vya msingi vya ushirika kwa njia ya mnada ambapo wafanyabiashara waliopitishwa na serikali kuwa wanunuzi wa dengu, baada ya kukidhi vigezo na masharti, ndio watakuwa wanashindana na mshindi atapewa kibali cha kulipa pesa kukabidhiwa bidhaa yake," aliongeza.

Aidha, alisema baada ya mshindi kulipa pesa na kukabidhiwa bidhaa yake, ndipo AMCOS itaandaa malipo ya kila mkulima (stakabadhi gharani) na kumpatia pesa yake bila ya kupunjwa bei.

Mmoja wa wafanyabiashara wa dengu, Hassani Mboje, alidai kutokubaliana na maagizo hayo ya serikali kwa maelezo kuwa imekuwa ghafla sana.

Alisema ni bora wangepewa muda kwa kuwa walikuwa wameshakopa fedha benki kwa ajili ya kununua dengu kwa mkulima na kubainisha kuwa wataingia hasara.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Shinyanga (SHIRECU), Richard Luhende, alisema msimu wa ununuzi wa dengu mkoani humo ulitarajiwa kuanza jana, na kubainisha bei elekezi ni shilingi 800 kwa kilo moja, na kwamba siku ya mnada ikifika wafanyabiashara watakuwa wanatangaziwa.



Watuhumiwa wanne akiwamo wakili wa kujitegemea, Dk. Ringo Tenga, wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusomewa mashtaka ya uhujumu uchumi na kuingilia miundombinu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TPSF kutumia fursa kusaka masoko

INATOKA UK. 3

(TPSF), Godfrey Simbeye, alisema kuwa wanatarajia kuwa na washiriki 500 kutoka sekta binafsi.

"Kuna bidhaa ambazo zimepewa kipaumbele katika ushiriki wa maonyesho hayo ikiwamo dawa, saruji, plastiki na vifaa vya kilimo," alisema Simbeye.

Alisema wanashukuru ushirikiano mzuri uliopo kati yao na serikali, kwa kuwa hata katika kamati ya maandalizi wamo wanachama kadhaa wa TPSF.

"Hatua hiyo inatia moyo nasi tumejipanga kuitumia vyema katika kuangalia masoko mapya ya bidhaa zetu zinazozalishwa nchini, ili tutanue soko kwa nchi nyingine wanachama wa SADC," alisema.

Maonyesho hayo yamepangwa kufanyika katika ukumbi wa Mlimani City Julai 22 hadi 26, 2019, ambapo pia yatahusisha na wafanyabiashara na wajasiriamali wa nchini na wengine kutoka katika nchi wanachama.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Abdul Chacha, akizungumzia kuhusu Wiki ya Viwanda na Biashara inatokana na maazimio ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika tarehe 29 Aprili 2015 mjini Harare, Zimbabwe.

"Wiki ya Viwanda inatokana na mkakati wa viwanda ambao uliidhinishwa na wakuu wa nchi na serikali wa SADC mjini Harare, Zimbabwe," alisema.

Akizungumza kwenye warsha ya waandishi wa habari ya kuwajengea uwezo wa kuandika habari za SADC, Chacha alisema kuwa mkakati wa viwanda wa SADC una lengo la kuongeza kasi ya kuimarisha ushirikiano na ushindani wa kiuchumi kutoka katika nchi zisizokuwa wanachama wa SADC.

Alisema mkakati wa viwanda wa SADC 2015- 2063 umegawanywa katika awamu kuu mbili; awamu ya kwanza 2015 -30 na awamu ya pili 2030-2063.

Mkakati huo umejikita katika maeneo makuu matatu ambayo aliyataja kuwa ni viwanda ushindaji na mtangamano wa kikanda na kila eneo kati ya yaliyotajwa, utekelezaji wake umependekezwa katika mpango mkakati wa viwanda wa SADC.

Awali mratibu wa vyombo vya habari kitaifa SADC, Zamaradi Kawawa Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Maelezo, alisema maonyesho hayo yatafungua fursa zaidi za kibiashara.

Zamaradi aliwataka waandishi wa habari kutumia vyombo vyao kuwapasha habari wafanyabiashara, wajasiriamali na wananchi kwa ujumla kutumia nafasi hizo vyema.

# Programu kuwezesha masoko, kilimo

INATOKA UK. 7

nyingi ili kundi hili liweze kujiajiri," alisema Mnyeti.

Alisema licha ya hali ya uchumi nchini kuimarika, kuna tofauti kubwa sana ya kipato kati ya kundi la maskini na wale waliojaliwa kupata kipato.

Mkuu wa wilaya ya Hanang, Joseph Mkirikiti, alisema malengo ya serikali yatimie ni lazima watendaji wa serikali na hususani katika ngazi za wilaya kutekeleza wajibu wao kwa kuhakikisha wanamsaidia Rais.

"Inasikitisha sana wengi wetu hatufanyi vile Rais anavyotaka tufanye na badala yake tumekuwa watu wa matamko tu na kuweka mbele vyeo vyetu hali ambayo imezorotesha mahusiano yetu na sekta binafsi," alisema.

Mkirikiti ameongeza kuwa ni jambo la ajabu na kusikitisha pale matatizo ambayo yangeweza kutatuliwa katika ngazi ya wilaya yanamfikia kiongozi mkuu wa nchi kwa ajili ya kutafutiwa ufumbuzi.

Naye Naibu Katibu Mtendaji wa Baraza la Biashara la Taifa, Oliver Vengula, alisema kwa sasa baraza hilo limetoa mwongozo mpya ambao ndio utakaokuwa ukitumika katika kuendesha mabaraza.

"Majuzi tumemuona akikutana na wafanyabiashara nchini kujadiliana nao namna bora ya kuboresha mazingira ya biashara, na kama mtakuwa mmegundua sehemu kubwa ya mambo yaliyojadiliwa au kulalamikiwa mengi yanatuhusu sisi watendaji wa huku chini, hatukutekeleza wajibu wetu, tubadilike," alisema.

Mwenyekiti wake wa Kamati ya Ufundi wa Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Kilimo nchini (AMDT), Mike Laizer, alisema malengo ya warsha hiyo yalikuwa kuwajengea uwezo watendaji hao wa sekta ya umma pamoja kutambua vikwazo vinavyoikabili sekta ya umma katika kutekeleza majukumu yake.

"AMDT imelenga kuboresha mifumo mbalimbali ya kimasoko ili iweze kumsaidia mkulima na husussani mkulima wa mazao ya alizeti, mahindi na mikunde, tumelenga kuwa na mazingira wezeshi kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa kuwa na mazingira rafiki ya kibiashara baina ya pande husika," alisema Laizer.

Naye Mtaalamu wa Kuendeleza Mifumo ya Masoko wa AMDT, Tertula Swai, alisema mpango wa kuwakutanisha watendaji hao wakuu kutoka katika wilaya tofauti nchini umelenga kuwajengea uwezo na kuweka mifumo endelevu ya mabaraza ya biashara katika kutatua kero mbalimbali.

# Bwawa kumaliza magonjwa mlipuko

**Na Jumbe Ismailly,** ITIGI

KUKAMILIKA kwa ukarabati wa bwawa lililopo kwenye pori la Akiba la Rungwa-Kizigo- Muhesi katika Kata ya Rungwa wilayani Manyoni, mkoani Singida na ujenzi wa skimu ya umwagiliaji ya Kijiji cha Itagata, Kata ya Mgandu, kutasaidia kupunguza magonjwa ya milipuko.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi kwa Naibu Katibu Mkuu CCM, Rodrick Mpogoro, Mwenyekiti Halmashauri ya Itigi, Ally Minja, alisema halmashauri hiyo imepokea zaidi ya shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya ukarabati wa bwawa lililopo katika pori la Akiba la Rungwa – Kizigo - Muhesi Kata ya Rungwa na ujenzi wa skimu ya umwagiliaji katika kijiji cha Itagata, kata ya Mgandu.

"Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu CCM tumeweza kupata fedha kwa ajili ya ukarabati wa bwawa la Rungwa, kutoka hapa kwenda kwenye kata ya Rungwa ni kama kilomita 200," alisema na kuongeza:

"Bahati nzuri Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa na kamati yake ya siasa wiki mbili zilizopita walifika kuona utekelezaji huo."

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, shughuli za ukarabati huo zimekwenda vizuri kwani maji yamejaa na mradi huo walipokea kutoka Serikali Kuu shilingi milioni 830 kwa ajili ya ukarabati wa bwawa hilo ambalo shughuli hiyo ya ukarabati imekamilika.

Aidha, Minja alisema kuwa bwawa limetengenezwa kimkakati kwani bwawa hilo lipo katika pori la Akiba la Hifadhi ya Rungwa, Kizigo Muhesi, kwa hivyo upatikanaji wa maji hayo umeweza pia kuvutia wanyama kubaki kwenye maeneo hayo.

Matumizi mengine ya maji hayo ni kwa ajili ya binadamu kwa kuyapampu kuyapeleka kwenye Mji wa Rungwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu na kwamba kabla ya kukamilika kwa mradi huo, mji huo ulikuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa majisafi na salama.

# Marekani yakomboa maelfu adha ya maji

**Na George Tarimo,** IRINGA

ZAIDI ya wananchi 5,000 wa kijiji na kata ya Mgama mkoani Iringa wameondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma ya maji baada ya kijiji hicho kujenga tangi kubwa la kuhifadhia maji.

Hayo yalibainishwa na mwenyekiti wa jumuiya ya watumia maji kata ya Mgama, Seleman Kilawa, wakati akieleza changamoto ya maji katika kijiji hicho kwenye ziara ya Kaimu Balozi wa Marekani, Dk. Inmi Patterson.

Baada ya kutaabika muda mrefu wananchi hao wameamua kutumia nguvu kazi zao kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la (WARIDI) wameamua kujenga tangi la maji ambalo wameeleza litamaliza changamoto ya maji katika kata hiyo na vijiji vya jirani.

Kilawa alisema kabla ya ujenzi wananchi hasa kinamama walikuwa wakitembea umbali mrefu na usiku wa manane kufutata maji.

**Awali wananchi hawa walikuwa wakitumia tangi la maji ambalo lilijengwa kwa mbao, lilikuwa likipoteza maji mengi sana.**

"Kinamama wengi ndoa zao zilikuwa shakani wanaamka usiku wa manane kufuata maji tena umbali mrefu na wanarudi, na ndoo moja kichwani wakiwa wamechoka, lakini pia wanashindwa kufanya shughuli nyingine za maendeleo kutokana na kuwa wamechoka," alisema Kilawa.

Ujenzi wa tangi la maji umetekelezwa kwa hisani ya watu wa Marekani kwa kushirikiana na wananchi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.


Francis Mtitu, mwakilishi wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (Usaid), alisema WARIDI imeamua kutoa msaada huo kwa lengo la kumaliza changamoto ya maji kijijini hapo ambapo awali wananchi hao walikuwa wakitumia mfumo wa maji uliojengwa zaidi ya miaka 40 iliyopita, haukukidhi upatikanaji wa maji ya kutosha.

"Awali wananchi hawa walikuwa wakitumia tangi la maji ambalo lilijengwa kwa mbao, lilikuwa likipoteza maji mengi sana," alisema Mtitu.

Mtitu alisema mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 260 hadi kukamilika kwake.

Dk. Patterson alisema serikali ya Marekani imeridhishwa na misaada inayoiletea Tanzania kwa ajili ya kutatua changamoto mbalimbali, na ndio maana inaendelea kufadhili miradi mingi ya maendeleo.

Alisema serikali ya Marekani inafahamu changamoto ya maji mkoani Iringa na imeamua kutoa Dola milioni 50 kwa ajili ya kujenga miradi yote inayotelekezwa na WARIDI mkoani hapa.



Daktari wa mifugo kutoka Shirika la Haki na Ustawi wa Wanyama Tanzania (TAPO), Master George, akitoa chanjo kwa punda ili kuwakinga na magonjwa. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Taasisi yawezesha wakulima wadogo, wanawake, vijana

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya kuendeleza mifumo ya kimasoko katika kilimo iliyo chini ya Serikali za Dernmak, Ireland na Sweden kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania, imeanza kuwasaidia wakulima wadogo, vijana na wanawake ili kuongeza fursa katika mnyororo wa thamani wa mazao matatu.

Tasisi hiyo imeanza kuyasaidia makundi hayo kwenye mazao ya alizeti, mahindi, maharage na mbaazi ili waongeze mnyororo wa thamani kuanzia uzalishaji, usindikaji na masoko ndani na nje ya nchi.

Akizungumza katika maonyesho ya kilimo biashara wilayani Kilosa mkoani Morogoro, Meneja Usimamizi, Maarifa na Mawasilino wa Taasisi hiyo, Al-aman Mutarubukwa, alisema mradi huo umelenga kuwafikia wakulima 500,000.

Alisema wana miradi 11 iliyopo katika mikoa 15, na kwamba miradi mitatu inahusisha zao la mahindi katika mikoa minane iliyopo nchini ili kuongeza thamani ya nafaka.

Akizungumzia kuhusu alizeti, mbaazi na maharage, alisema miradi hiyo ipo katika mikoa ya kusini ikihusisha Mtwara, Lindi, Manyara, Mbeya, Njombe, Iringa, Dodoma na Singida na makundi hayo yameanza kunufaika.

Mutarubukwa alisema mpango huo umelenga kubadilisha mifumo ya usambazaji na mifumo bora ya mbegu bora ya alizeti ambapo kwa miaka mitatu iliyopita hakukuwa na mbegu bora sokoni.

Alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na kampuni ya uzalishaji mbegu ya alizeti ya ndani na nje wameingiza mbegu chotara zilizoboreshwa na kuwasambazia wakulima ambao wameongeza uzalishaji wenye tija.

"Kwa miaka miwili iliyopita wakulima walikuwa wakitumia mbegu zilizozoeleka na kutoa mavuno kidogo wastani wa gunia tatu kwa hekali, lakini baada kuleta mbegu za chotara mavuno yameongezeka katika hekali moja mavuno yamefikia wastani wa gunia 15-18."

Mutarubukwa, alisema kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Ilonga wilayani Kilosa, wameboresha mbegu ya rekodi ya alizeti na kuongeza uzalishaji kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya viwanda vya kutengeneza mafuta ya kula.

Mmoja wa wakulima wa alizeti wilayani Kilosa ambaye alishiriki katika maonyesho ya kilimo biashara, Halfan Mtetema, alisema kupitia uzalishaji wa mbegu ya rekodi iliyoboreshwa na watafiti wa TARI Ilonga, wameongeza uzalishaji wa alizeti mara nne zaidi ya uzalishaji wa mwanzo walikuwa wakipata gunia saba kwa hekari.

Mkulima wa mahindi na mpunga, Leticia Semwenda, alisema kupitia maonyesho hayo na uhamasishaji wa kilimo cha alizeti msimu ujao anategemea kuanza kilimo hicho kwa kuwa kimeonyesha ni zao lenye faida kubwa kiuchumi.

Naye Mratibu wa alizeti nchini, Frank Reuben, alisema mkakati wa TARI ni kutoa matokeo ya utafiti mpya wa mbegu za alizeti itakayokuwa na ubora kuliko mbegu yoyote iliyopo sokoni kwa sasa.

# Majaliwa: Pamba yote itakuwa imenunuliwa ifikapo Julai 30

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema hadi kufikia Julai 30, mwaka huu, pamba yote iliyoko katika mikoa mbalimbali nchini inayolima zao hilo itakuwa imeshanunuliwa na wakulima wote kulipwa fedha zao.

Kauli hiyo ilitolewa jana, na Waziri Mkuu alipozungumza kwa nyakati tofauti na wananchi wa vijiji vya Mbutu na Mwabakima wakati akiwa katika ziara yake ya kikazi katika Wilaya ya Igunga mkoani Tabora.

Alisema serikali imeamua kuingilia kati suala la ununuzi wa zao la pamba kutokana na kusuasua kwa soko lake kwa kutoa dhamana ili kuwawezesha wanunuzi kukopeshwa fedha na benki mbalimbali kwa ajili ya kununulia pamba kutoka kwa wakulima.

Hivyo, aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya katika maeneo yote yanayolima zao hilo wawasimamie ipasavyo wanunuzi wote ili kuhakikisha fedha zitakazopatikana zinakwenda kutumika kwa ajili ya kununulia pamba na si vinginevyo, ambapo kibali cha dhamana kinatarajia kutoka leo.

**Kuhusu suala la maghala tunatambua tatizo hilo na tutahakikisha tunayaboresha ili pamba iweze kuhifadhiwa katika mazingira bora.**

Amesema kumekuwa na kusuasua kwa ununuzi wa zao hilo tangu kuanza kwa msimu wa mwaka huu, jambo ambalo serikali haiwezi kulifumbia macho suala hilo, hivyo jana alikutana na kufanya mazungumzo na wadau wa zao hilo wakiwamo wanunuzi na wamekubaliana kununua pamba yote.

"Tunatambua adha mliyoipata tangu kuanza kwa msimu wa mwaka huu na hayo ni mapito tu. Nawasihi muwe na amani kwani serikali yenu inafuatilia suala hili na Rais John Magufuli anataka kuona pamba yote inatoka kwa wakulima ili kuwawezesha kupata tija."

Kadhalika, Waziri Mkuu aliwasihi wakulima wa pamba na wakulima wa mazao mengine nchini wahakikishe mara baada ya kuuza mazao yao wanatenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kununulia pembejeo watakazozitumia katika msimu ujao.

Awali, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema serikali itahakikisha inaendelea kutafuta masoko ya mazao hayo ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha wakulima kuwa na uhakika wa masoko kwa mazao yao na hivyo kujiongezea tija.

Pia, waziri huyo amesema mbali na kutafuta masoko, serikali imedhamiria kufufua viwanda mbalimbali vya nguo hapa nchini ili kuwawezesha wakulima wa zao la pamba kuwa na soko la uhakika. "Kuhusu suala la maghala tunatambua tatizo hilo na tutahakikisha tunayaboresha ili pamba iweze kuhifadhiwa katika mazingira bora."




Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 kupitia promosheni ya SOKA la AFRIKA, ambapo Omary Ahmed Bwenda (kulia), mfanyabiashara na mkazi wa jijini Dar es Salaam aliibuka kuwa mshindi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wapewa neno utunzaji rasilimali maji

**Na Frank Monyo**

OFISA wa Maji Bonde la Wami Ruvu, Simon Ngonyani, amesema changamoto kubwa iliyopo sasa nchini ni upatikanaji wa maji ambayo ndio 'injini' ya maendeleo kuelekea Tanzania ya viwanda, hivyo wadau wa maendeleo pamoja na serikali wanapaswa kuunga mkono juhudi za utunzaji wa rasilimali za maji.

Ushauri huo aliutoa mwishoni mwa wiki katika mkutano wa saba wa mwaka wa Bodi za Maji za Mabonde nchini uliofanyika Kigoma.

Ngonyani alisema changamoto kubwa kwa bodi ya maji ya Bonde la Wami/Ruvu ni uwapo wa ongezeko la viwanda katika ukanda wa bonde hilo ambao kwa namna moja ama nyingine ni watumiaji wakubwa wa maji, hivyo basi ni lazima kufanyike jitihada za kutosha kuhakikisha vyanzo vinalindwa na maji yanakuwapo.

Alisema kutokana na maji kuwa kidogo, siku za usoni kutakuwa na changamoto ya ugawaji wa maji kwa sababu watumiaji ni wengi, na maji ni kidogo, hivyo wamejipanga kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa kwa ufasaha ili kukabiliana na hali hiyo hapo baadaye.

"Embu tujiulize maswali haya; maji yapo wapi? Swali la pili; je, kwa haya maji yaliopo ni endeleavu...yataendelea kuwapo na kutosheleza mahitaji?... Swali la tatu; Je, maji yaliopo yana ubora? Tukipata majibu ya haya maswali tutaona tunatakiwa kuchukua jitihada za makusudi katika kuongeza nguvu katika utunzaji wa vyanzo vya maji," alisema.

Aliongeza kuwa kwa hali ya maji iliyopo sasa hakuna budi wakulima wakubwa na wadogo wakaachana na umwagiliaji wa mafuriko "floods Irrigation" kwani hayo ni matumizi mabaya ya maji. "Juzi tulienda kwenye kiwanda cha Sukari cha Mtibwa tulikuta wanatumia floods Irrigation kumwagilia mashamba yao ya miwa tulikuta maji mengi sana hadi yanatisha lakini tulizungumza nao na kuwaelimisha jinsi ya kutumia maji vizuri kwani wapo wenzao wa kiwanda cha sukari Bagamoyo wanatumia umwagiliaji wa matone "Drip Irrigation" kwa maana hiyo tukitumia maji kwa ufanisi yanaweza yakatosha," alisema Ngonyani.

Aliongeza kuwa hakuna namna ambavyo serikali ikajitoa katika kusimamia rasilimali za maji kwa maana ya rasilimali kwa kuwa mabonde yanatakiwa kuwezeshwa na sio kutegemea mapato yake pekee au wadau wa maendeleo.

Alisema serikali inatakiwa kuongeza nguvu katika mabonde ili maji yaendelee kuwapo ili kesho ya Dar es Salaam iendelee kuwapo kwani kuna wakati Mto Ruvu ukipata "mafua" pampu za kusukuma maji za Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) zinaungua.

"Njia pekee ya kukabiliana na hali hiyo ni kujenga lile bwawa la Kidunda lililopo mkoani Morogoro na endapo tusipofanya hivyo tutakuwa tumegonga mwamba," alisema.

# Wito kutunza sokwe mtu

**Na Magreth Magosso,** KIGOMA

CHANGAMOTO ya uharibifu wa misitu unaofanywa na baadhi ya wananchi wa vijiji vilivyopo karibu na Hifadhi ya Taifa ya Gombe Wilaya ya Kigoma, inahatarisha kutoweka kwa wanyama adhimu aina ya sokwe mtu 90, waishio kwenye hifadhi hiyo.

Hayo yalibainishwa jana wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Sokwe Mtu Duniani, yaliyoshirikisha Serikali na Taasisi ya Jane Goodall (JGI) kupitia mradi wa Roots and Shoots, katika kuelimisha jamii juu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa maslahi mapana ya viumbe hai.

Mkurugenzi wa Sayansi za Uhifadhi wa Mradi wa Roots and Shoots, Shadrack Kamenya, alisema sokwe mtu wapo hatarini kutoweka katika hifadhi hiyo kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoathiri misitu na mapori, ikiwamo hifadhi ya Gombe.

"Sokwe mtu anategemea misitu kwa ajili ya makazi, chakula hasa mizizi na matunda kwa asilimia 85, kitendo cha jamii kuvamia maeneo ya misitu na mapori ya hifadhi ni chachu ya wanyama hawa wenye asilimia 99 ya vinasaba vya ufahamu kama binadamu kutoweka," alisisitiza.

Alieleza kuwa athari ya uharibifu wa misitu ni pamoja na kuwakimbiza wanyama hao katika hifadhi hiyo kwa kuwa sokwe mtu wanaishi katika jumuiya za koo zao (familia) na kila koo ina uongozi wake, na hawaingiliani katika himaya zao, hivyo kitendo cha kuvamia maeneo ya misitu kinawaathiri kukosa makazi na chakula.

Alizitaja sababu ya kuanzishwa kwa siku maalum ya sokwe ni pamoja na kumuenzi mtafiti kutoka Uingereza wa JGI baada ya kubaini madhira wanayokumbana nayo katika msitu huo na kuanza kutafiti mwaka 1968 na mwaka 1978 shughuli za kitalii ilianza rasmi kwenye hifadhi hiyo, hali iliyomsukuma mtafiti huyo, Dk. Jane Goodall, kuiweka Julai 14 kila mwaka iwe maalum kumwadhimisha sokwe mtu.

**Sokwe mtu anategemea misitu kwa ajili ya makazi, chakula hasa mizizi na matunda kwa asilimia 85, kitendo cha jamii kuvamia maeneo ya misitu na mapori ya hifadhi ni chachu ya wanyama hawa wenye asilimia 99 ya vinasaba vya ufahamu kama binadamu kutoweka.**

# Maadhimisho fuvu la binadamu yaiva

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya ugunduzi wa fuvu la binadamu wa kale anayejulikana kama Zinjanthropus Boisei yatakayofanyika Julai 22, eneo la Olduvai ndani ya Hifadhi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Akizungumza jana jijini hapa, Mwenyekiti wa Maandalizi hayo, Prof. Audax Mabula, alisema sherehe hizo awali zilipangwa kufanyika kesho lakini sasa zimesogezwa mbele hadi tarehe hizo.

Prof. Mabula alisema pia kuna mabadiliko ya terehe ya warsha iliyokuwa inaandaliwa kufanyika leo na badala yake itafanyika Julai 20 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa Arusha (AICC).

**Fuvu hilo lenye umri wa miaka milioni 1.75 iliyopita liligunduliwa Julai 17, 1959 na wataalamu wa akiolojia, Dk. Louis Leakey na mke wake Dk. Mary Leakey.**

Alisema mabadiliko hayo hayatahusu ofa maalum ya kutembelea makumbusho ya Olduvai na maonyesho maalum sehemu mbalimbali nchini yenye urithi wa utamaduni yataendelea kama ilivyopangwa kuanzia kesho hadi Julai 22.

Lengo la maonyesho hayo, alisema ni kuendeleza utafiti, uhifadhi, utalii na matumizi bora na sahihi ya urithi wa utamaduni.

Pia alisema fuvu hilo lenye umri wa miaka milioni 1.75 iliyopita liligunduliwa Julai 17, 1959 na wataalamu wa akiolojia, Dk.Louis Leakey na mke wake Dk. Mary Leakey.

Alisema lengo lingine la madhimisho hayo ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa urithi wa asili na utamaduni, kuendeleza utafiti, uhifadhi endelevu, matumizi bora na sahihi ya urithi wa utamaduni na kuendeleza utalii nchini na duniani.

Prof. Mabula alisema maadhimisho hayo yanafanyika kwa ushirikiano wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Makumbusho ya Taifa, Idara ya Mambo ya Kale na Idara ya Akiolojia na Urithi wa Utamaduni, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Alisema siku ya maadhimisho hayo kutakuwa na uzinduzi rasmi wa Makumusho ya Dk. Leakey ambayo familia yake ilikuwa ikiishi na kufanya shughuli zake za kitafiti maeneo ya Ngorongoro mwaka 1930.

Alisema hiyo ni fursa kwa wananchi, wanafunzi na watalii kupata fursa ya kujionea makumbusho iliyosheni vitu vilivyotumiwa na binadamu wa kale na familia ya Dk. Leakey alivyotumia wakati huo wa utafiti.

Naye Meneja wa Mambo Kale wa Mamlaka hiyo, (NCAA) Mhandisi Joseph Mwankunda alisema ugunduzi wa fuvu hilo, ulisaidia kubadilisha uelewa wa wanasayansi kuhusu mchango wa bara la Afrika katika historia na chimbuko la binadamu duniani.

Alisema masalia ya Zinjanthropus Boisei na masalia mengine ya binadamu wa kale, zana zao za mawe na masalia ya mifupa ya wanyama waliyokuta bonde la Olduvai miaka milioni 2.0 iliyopita, vinathibitisha dunia kuwa Tanzania ndio nchi pekee yenye taarifa bora na sahihi kuhusu chimbuko la binadamu na utamaduni wake, chakula na namna ya kupata chakula hicho katika kipindi hicho.

Pia watu watajionea nyumba, meza, vyombo, camera, vitanda,gari na vifaa mbalimbali alivyotumia katika utafiti wake ambavyo vitakuwa sehemu ya makumbusho hayo, maana ni tofauti na vifaa vya sasa wanavyotumia watafiti.

## Bashiru afungua milango kusaidia matawi CCM

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, ametoa mabati 200 kwa matawi ya CCM ya Naisinyai na Songambele wilayani Simanjiro kwa ajili ya kujenga ofisi mpya.

Akizungumza na wanachama wa matawi hayo, Dk. Bashiru alisema mabati hayo 200 yanatolewa kupitia mfuko wa kuendeleza chama wa mwenyekiti wao, Rais John Magufuli.

Dk. Bashiru alisema uhai wa chama hicho unategemea wanachama walioko kwenye matawi na mashina, hivyo wanayaunga mkono ili kuendelea kuifanya CCM iwe karibu zaidi na wananchi.

"Lakini nawapongeza baadhi ya wadau wa maendeleo wa mji mdogo wa Mirerani, ambao ni wana CCM, Paul Mollel na Siria Mepukori kwa kila mmoja kuchangia Sh. 500,000 ya ujenzi wa tawi la CCM Songambele na Diwani wa Loiborsiret, Ezekiel Lesenga (Mardad), aliyejitolea mifuko 20 ya saruji kwa tawi la Songambele," alisema.

Dk. Bashiru alimpongeza pia Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, aliyejitolea mifuko 100 ya saruji ya tawi la Songambele na Mbunge wa Simanjiro, James Ole Millya, aliyetoa mifuko 40 kwenye tawi la Naisinyai na mifuko 20 katika tawi la Songambele.

Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Yefred Myenzi, ambaye alisema binafsi anachangia mifuko 10 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa tawi la CCM Songambele.

Mbunge wa Simanjiro, Millya, alisema amewatafutia wadau na amewachangia kwa kuwa matawi yote ni yake, Naisinyai yote ni CCM japo hapo Songambele diwani ni wa Chadema.

Kada wa chama hicho, Siria Mepukori, alisema yeye ni mdau wa maendeleo na aliamua kumuunga mkono Dk. Bashiru kwa Sh. 500,000 ili kufanikisha ujenzi wa tawi la Songambele.

Kada mwingine, Paul Mollel, alisema amechangia Sh. 500,000 kwenye ofisi hiyo ya Songambele ili kumuunga mkono Katibu Mkuu wa CCM, ambaye ana lengo zuri la kuhakikisha matawi yanajengwa.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Arusha, Loata Sanare, akizungumza na wazee waliowakilisha makundi ya wafugaji, wanawake, watumishi walioachishwa kazi katika Hifadhi ya Ngorongoro. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Mwenyekiti UVCCM alia uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MWENYEKITI mpya wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Arusha, Omary Lumato, amesema katika uongozi wake atahakikisha anawaunganisha vijana wote, ili kuiwezesha CCM kushinda kwa kishindo katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Aidha alisema atashirikiana na wagombea wenzake Suleman Msuya na Novat Filemon ambao kura zao hazikutosha katika uchaguzi huo.

Lumato alisema hayo mwishoni mwa wiki, mara baada ya kutangazwa kuwa mshindi katika nafasi hiyo na kuahidi kuwaunganisha vijana wa Mkoa wa Arusha, ili CCM iendelee kushika dola.

"Ninawashukuru vijana wenzangu kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwenyekiti wenu. Ninawaahidi kuwa nitahakikisha vijana wote wa mkoa huu wanakuwa kitu kimoja tofauti na walivyo hivi sasa kwa maslahi ya chama chetu,"alisema.

Pia alisema atahakikisha ajira za muda mfupi na muda mrefu zinazotolewa wakati wa utekelezaji wa miradi mbalimbali mkoani hapa, huku kipaumbele kikiwa vijana.

"Najua vijana wengi mnakabiliwa na ukosefu wa ajira, naomba niwahakikishie kuwa nitatumia uwezo wangu wote kuhakikisha kuwa fursa zote za ajira, zinazojitokeza mkoani hapa kipaumbele mnapata ninyi kwa kuwa sisi ndiyo wenye serikali," alisema.

Awali, Katibu wa UVCCM Mkoa wa Arusha, Jamal Khimji, aliwataka vijana kutoshawishiwa kuchagua kiongozi na kwamba kila mtu ana demokrasia ya kuchagua kiongozi ambaye anaona anafaa kuongoza jumuiya hiyo.

"Wagombea wote ambao majina yao yamerudi wana sifa za kuongoza, ila nafasi ni moja tuu hivyo tambueni kuwa hakuna ambaye hatoshi kuwa mwenyekiti katika majina haya matatu," alisema.





# Mchakato uchaguzi wamwibua Malecela

Na Paul William, SAME

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara na Waziri Mkuu mstaafu, John Malecela, amewataka vijana wa chama hicho kuunga mkono kwa vitendo juhudi zinazofanywa na Rais John Magufuli.

Pia amewataka kuhakikisha CCM inaendelea kushika dola pamoja na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Malecela alisema hayo jana alipozungumza na wanachama wa CCM katika kata ya Ndungu, Jimbo la Same Mashariki na kusisitiza kuwa vijana ndio nguvu kazi ya chama na taifa.

**Serikali ya awamu ya tano imeonyesha dhamira yake ya dhati ya kupambana na matatizo ya wananchi pamoja na kuwaletea maendeleo.**

Alisema serikali ya awamu ya tano imeonyesha dhamira yake ya dhati ya kupambana na matatizo ya wananchi pamoja na kuwaletea maendeleo na kuwataka vijana kuunga mkono juhudi hizo.

"Vijana chama kinawategemea sana katika kuhakikisha kinaendelea kushika dola, hivyo hampaswi kulala. Tokeni na kueneza yale yote mazuri yaliyokwisha kufanywa na serikali ya CCM ili kuwaondolea imani ambayo wamekuwa wakiaminishwa na wapinzani kuwa CCM haijafanya chochote," alisema Malecela.

Waziri mkuu huyo mstaafu alisema mwaka huu kuna uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba na kuwataka vijana wa Jimbo la Same Mashariki na mkoa wa Kilimanjaro kwa ujumla kuwa mfano bora wa kuigwa kwa kukipambania chama kushinda viti vyote vya uongozi.

Aidha, aliwaomba Wanaccm kuwa wamoja katika kipindi hiki cha uchaguzi na kuepuka kugawanyika na kuwa makundi kwa kuwa kufanya hivyo kutakigharimu chama.



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Civil Social Protection Foundation (CSP), Nemence Iriya, akizungumza na waandishi wa habari juu ya mikakati ya kupambana na ukeketaji mkoani Manyara, mjini Babati juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Siha wakumbushwa kutumia EFD

Na Paul William, SIHA

WAFANYABIASHARA wilayani Siha mkoani Kilimanjaro wametakiwa kuhakikisha wananunua mashine za risiti za kielektroniki (EFD), ili kuondoa malalamiko dhidi ya Mamlaka ya Mapato (TRA) kuhusu kodi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Meneja wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, wakati akizungumza na wafanyabiashara wilayani hapo.

Alisema ni muhimu kwa wafanyabiashara wote kumiliki mashine hizo za kutolea risiti pamoja na kuzitumia hali ambayo itawezesha ulipaji wa kodi halali kwa huduma wanayoitoa.

"Natambua wako baadhi ya wafanyabiashara wanamiliki mashine hizi, lakini wamekuwa hawazitumii na badala yake wamezifungia ndani, hivyo nitumie nafasi hii kuwaomba mzitumie mashine hizo ili kulipa kodi halali kulingana na mauzo yenu," alisema.

Pia alisema serikali kwa sasa imepunguza viwango vya kulipa kodi kwa wafanyabiashara wadogo ambao hulipa kodi kutokana na mauzo yao na kwamba wafanyabiashara waliokuwa wanalipa kodi ya Sh. 100,000 kwa mwaka, sasa wanalipa Sh. 100,000 katika muda huo.

Aliongeza kuwa wale ambao ndio wanaanza biashara kwa mara ya kwanza watakadiriwa kodi na kupewa namba ya mlipakodi, lakini hawatalipa kodi hadi baada ya miezi sita lengo likiwa ni kuwapa fursa ya kujiandaa vizuri kufanya biashara.

Meneja huyo alisema serikali imepunguza kodi kwa kiwango kikubwa ili kuwawezesha wananchi wa hali ya chini kumudu kulipa kiwango cha kodi kilichowekwa.

Akizungumzia mwitikio wa wafanyabiashara katika mkoa wa Kilimanjaro kulipa kodi, Mwangosi alisema mwitikio ni mkubwa huku pia akitumia nafasi hiyo kuwataka wale ambao hawajalipa kodi zikiwamo kodi za majengo kutekeleza takwa hilo bila kusukumwa.

Naye mfanyabiashara Eliza Cheo alitumia nafasi hiyo kuishukuru serikali kwa kuweka kiwango kidogo cha kodi ambacho kila mwananchi anaweza kukimudu.

Kwa upande wake Juma Uwiso alisema zamani wafanyabiashara walikuwa wakiwaogopa maofisa wa TRA na wakati mwingine kuwakimbia kwa kuwa kodi ilikuwa kubwa na walikuwa wanaimudu kwa shida, lakini sasa hivi wanaweza kuimudu bila tatizo.

# Viziwi wataka wakalimani serikalini

Na Mary Mosha, HAI

BAADHI ya watu wenye ulemavu wa kusikia mkoani Kilimanjaro, wameiomba serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kuangalia namna ya kuajiri wakalimani katika kila kitengo ili kutoa msaada pindi wanapofika katika taasisi hizo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki katika kongamano la uhamasishaji wa matumizi ya lugha ya alama kwa watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama na Mratibu wa Chama cha Viziwi Tanzania (Chavita) Wilaya ya Hai, Pulcheria Aloyce.

Alisema watu wenye ulemavu wa kusikia (viziwi ) wanakabiliwa na changamoto wanapofikia katika taasisi hizo kwa kuwa bila kuwapo kwa mkalimani, wanakosa haki zao kwa kushindwa kujieleza na kupatikana kwa ushahidi sahihi.

"Tunaiomba serikali kuangalia namna ya kuajiri mkalimani wa lugha za alama katika vyombo vya ulinzi na usalama ili kupata tafsiri mara wanapofika katika vituo hivyo. Pia wakati wa utoaji wa ajira tunaomba wawakumbuke watu wenye ulemavu ili kuwapo kupatikana mkalimani mmoja katika kila halmashauri ili kurahisisha mawasiliano," alisema.

Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, aliyewakilisha na Ofisa Tarafa wa Masama, Nsajigwa Ndagile, alisema watu wenye ulemavu ni binadamu kama walivyo wengine na wanahitaji kupewa huduma zote kama walivyo raia wengine wote wa Tanzania.

"Kwa sasa tutaishauri serikali kuangalia namna ya kuweka ajira za wakalimani katika kila wilaya, lakini kwa sasa tunawaomba mwendelee kutoa mafunzo ya alama ili watendaji wa idara mbalimbali kuendelee kupata mafunzo ya alama kwa lengo la kuwahudumia watu wenye ulemavu," alisema Ndagile.

Mmoja wa washiriki, Inspekta wa Polisi Zacharia Shabo, alisema mafunzo hayo yatawasaidia baadhi ya askari kufahamu lugha za alama zitakazosaidia kuwahudumia watu wenye ulemavu wanapofika katika kituo cha polisi.

"Ni kweli wapo baadhi ya walemavu ambao wakifika katika kituo cha polisi unaanza kubuni, ili kuwapa huduma lakini kwa baadhi ya askari wetu kupata mafunzo kunaweza kusaidia mawasiliano kuwa rahisi zaidi," alisema.

Naiman Akyoo ni Mkaguzi Msaidizi wa Magereza kutoka Gereza la Karanga, aliiambia Nipashe kuwa licha ya kazi yao kuwahifadhi wahalifu, kuna changamoto ya mawasiliano, hivyo mafunzo hayo yataleta mabadiliko.

Naye Hakimu wa Mahakama ya Bomang'ombe, Regina Samweli, alisema watu wenye ulemavu wamekuwa wakifika kutoa ushahidi katika mahakama hiyo na kuwataka waandike hali ambayo imekuwa ngumu kwao.

"Ambacho tumebaini kuwa watu hawa hawapendi kuambiwa waandike na kutokana na kukosa wakalimani, tunapata shida kuwaelewa na wakati mwingine tunatumia nguvu kubwa ili kubaini nini alichotamani kukisema. Mafunzo haya ya alama yatatusaidia kufanya kazi kwa uhakika bila kubaki na shaka," alisema Hakimu Regina.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 16, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

## JE, WAJUA?



Ukurasa 18

## Kwanini matumizi ya maziwa ya ngamia yanaongezeka duniani?

Ukurasa 15



## Wanafunzi likizo imekwishamalizika, rejesheni fahamu zenu shuleni



# ANGALIZO LA MKAPA LITASAIDIA VYUO VIKUU BINAFSI NCHINI

Ukurasa 16

# ELIMU KUTOKA POLISI

## FAHAMU ELIMU ILIYOTOLEWA NA JESHI LA POLISI KATIKA VIWANJA VYA SABASABA



Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Suzan Kaganda (wa pili kulia). Aliyevaa sare za Jeshi la Polisi ni Msemaji wa Jeshi la Polisi (SACP), David Misime na kushoto ni DCP Ahmada Khamisi. **PICHA: JESHI LA POLISI**

JESHI la Polisi nchini ni miongoni mwa taasisi za serikali ambazo zinatambua umuhimu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu huduma mbalimbali wanazozitoa pamoja na masuala ya ulinzi na usalama ili wananchi nao waone kuwa wana wajibu wa kutimiza katika suala zima la kuimarisha usalama wa raia na mali zao.

Katika Maonesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa yaliyofanyika Dar es salaam yenye kauli mbiu 'Usindikaji wa mazao ya kilimo kwa maendeleo ya viwanda' Jeshi la Polisi kwa kutambua suala la maendeleo ya nchi lilishiriki maonesho haya kwa kauli mbiu yake kuwa ulinzi na usalama ni ni nguzo ya maendeleo ya nchi kwa maana ya kuwa bila kuimarisha ulinzi na usalama hakuna maendeleo yoyote yatakayopatikana.

Jeshi la Polisi nchini, linatambua maendeleo yoyote ili yaweze kufikiwa ni lazima kuwapo na ulinzi, usalama na utulivu.

Jeshi la Polisi nalo liliweka banda lake katika viwanja vya Sabasaba lengo likiwa kutoa elimu kwa wananchi wanaofika katika viwanja vya Sabasaba juu ya kazi mbalimbali zinazofanywa na Jeshi la Polisi.

Mratibu wa utoaji elimu wa Jeshi la Polisi katika Maonyesho ya Sabasaba ambaye ni Msemaji wa Jeshi la Polisi, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), David Misime alibainisha elimu iliyotolewa na jeshi kuhusu namna wananchi wanavyoweza kushirikiana na polisi katika kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi, kampuni za ulinzi binafsi, elimu ya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

> Katika banda la Jeshi la Polisi mwaka huu kulikuwa na elimu ya ukaguzi wa matukio ya uhalifu na kwa kutumia gari maalumu linalotumiwa na wataalamu wa uchunguzi wa kisayansi katika maeneo ambayo uhalifu umetokea.

Vilevile, elimu ya dawa za kulevya na madhara yake na walionyeshwa sampuli mbalimbali za dawa za kulevya ikiwamo mmea wa bangi, namna ya kupata hati ya tabia njema pale mtu anapotakiwa awasilishe ili aajiriwe au asafiri kwenda nje ya nchi, elimu kuhusiana na makosa ya kimtandao (Cyber Crimes).

Aidha, wananchi walipata elimu ya sheria mpya ya kumiliki silaha na utaratibu unaotakiwa kufuatwa kwa anayehitaji kumiliki silaha.

Katika banda la polisi wananchi walipata elimu ya namna wanavyoweza kuwasilisha malalamiko yao kwa uongozi wa Jeshi la Polisi wanapokuwa hawajaridhika na huduma ya polisi.

Mbali na hayo, wananchi pia walipata elimu ya namna ya kupata mali iliyopotea (Loss report) na huduma hiyo pia inapatikana ndani ya banda la Polisi.

Katika banda la Jeshi la Polisi mwaka huu kulikuwa na elimu ya ukaguzi wa matukio ya uhalifu na kwa kutumia gari maalufu linalotumiwa na wataalamu wa uchunguzi wa kisayansi katika maeneo ambayo uhalifu umetokea.

Kwa kutambua umuhimu wa elimu ya usalama wa raia na mali zao, viongozi mbalimbali wa kitaifa walipongeza utoaji wa elimu ya usalama wa raia na mali zao akiwemo Rais Mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete alipofika katika banda la Polisi na kupongeza hatua ambayo Jeshi limechukua ya kuwaelimisha wananchi kuhusiana na masuala ya ulinzi na usalama.

***Imetolewa na :-***
***Kitengo cha Uhusiano,***
***Makao Makuu ya Jeshi la Polisi,***
***Dar es salaam,***
***habariphq@gmail.com***

# TUJIFUNZE KISWAHILI



**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

## Kiswahili kinavyopelekwa arijojo

'ARIJOJO' ni uendaji usio na mwelekeo mwafaka kwa kukosa kuongozwa au kupangiliwa vizuri; enda ovyo; hali ya kupotea. Ndivyo lugha yetu ya taifa – Kiswahili - isivyokuwa na thamani miongoni mwetu!

Ndo maana wahenga walisema "Titi la mama li tamu, jingine halishi hamu." Maana yake titi la mama huwa tamu, jingine halimalizi tamaa au hamu ya maziwa. Ni methali ya kutumiwa kupigia mfano kitu ambacho mtu ana asili nacho na anakithamini. Mbona hatutaki kuthamini lugha ya Kiswahili ambayo ndiyo lugha rasmi ya taifa?

'Mazungumzo' ni maongezi baina ya watu wawili au zaidi; ubadilishanaji wa mawazo baina ya watu, nchi au taasisi kuhusu jambo. 'Uandishi, pia uandikaji ni shughuli inayohusu masuala ya kuandika kama vile habari, magazeti au kitabu; namna au ujuzi wa kuandika. 'Uandikishaji' ni uwekaji wa taarifa za mtu au kitu katika orodha au daftari maalumu kwa kuandika maelezo yake.

Ilivyo sasa (kipindi cha wakati uliopo), waandishi, hasa wa michezo, hushindwa kuandika mtiririko mzuri wa sentensi (tungo yenye kiima na kiarifa na inayojitosheleza kimaana). Kadhalika mara nyingi huandika maneno ya mitaani yasiyo na ufasaha wa Kiswahili na upotoshwaji mwingi wa Kiswahili hivyo sentensi kutoeleweka!

Maneno ya kuzungumza: "Ee bwanae, ngoja nikupashe yaliyotokea mtaani kwetu leo" au "Umesikia yaliyotokea mtaani kwetu leo?" ama "Umekalia nini?" mwingine atajibu: (ashaakum) tamko la kuomba radhi kabla ya kusema neno la karaha: "matako." Haya yote ni maneno ya mazungumzo kwa hiyo hayastahiki kuandikwa gazetini wala kusomwa kwenye runinga au redio. "Kama hujui, klabu hizo kongwe hutenga bajeti zao za kila mwaka ikiwamo usajili na Simba kwa miaka miwili iliyopita ilikuwa ikitenga bajeti kubwa kuliko ile ya Yanga ikitajwa kuwa ni Sh1.3 bilioni huku watani wao wasajili kwa kuungaunga."

Ingeandikwa: " ... ikitajwa kuwa shilingi bilioni 1.3" badala ya Sh1.3 bilioni kama ilivyoandikwa. Kadhalika "huku watani wao wasajili ..." Neno la mwisho (wasajili) halikukamilika. Kwa hiyo sentensi haieleweki kwa kutokuwa na mtiririko mzuri.

Mwandishi anapoandika gazetini au kutangaza kwenye runinga ama redioni hufanya hivyo kuwajuza wasomaji wa magazeti, watazamaji wa runinga na wasikilizaji wa redio. Kinachotakiwa ni mwandishi kuwaeleza wasomaji, watazamaji na wasikilizaji kile kilichotokea badala ya kuweka maneno ya kuuliza. Mwandishi anapoandika au kuuliza "kama hujui ..." ni kosa kwani yeye ndiye aliyeona au kusikia kilichotokea/yaliyotokea hivyo anapaswa kuwajuza wasomaji/watazamaji/wasikilizaji hali halisi ilivyokuwa. Huyo anayeambiwa "Kama hujui ..." ni kweli hajui ndo maana ananunua gazeti, anaangalia runinga au anasikiliza redio ali ajue kilichotokea.

"Kwa misimu miwili, mashabiki wa Yanga wamejikuta wakinuna, hii ni kutokana na chama lao kutoka kapa Ligi Kuu Bara na michuano mingine." Maneno nitakayoyatolea maana halisi ni 'wamejikuta', 'chama lao' na 'kapa'.

Maana ya 'jikuta' ni kuwa mahali bila kukusudia, kuwa katika hali fulani bila kujua. 'Chama' ni kikundi cha watu wenye itikadi au lengo moja, kundi lenye kufuata kaida au silka fulani zenye kuegema dini, siasa, misimamo ya jamii, uchumi au jambo lingine lenye maazimio maalumu.

'Kapa' ni -topata kitu au alama zozote katika mchezo; shindwa kupata hata fungu moja. Si kweli kuwa Yanga haikupata alama zozote kwenye Ligi Kuu ya misimu miwili iliyopita. Waandishi wasitumie maneno ya mitaani au wasiyojua maana yake kwa undani.

Aidha maana nyingine ya 'kapa' ni urefu wa kutoka bega moja hadi lingine wakati wa kupima nguo. Pia ni vazi kama koti lakini fupi lisilo na mikono; kizibao//kizibau. Kadhalika eneo la pwani lenye tope ambapo mikoko husitawi. "Yanga iliyumba tangu Yusuf Manji, aliyekuwa Mwenyekiti wao kujiuzulu na kukosa pesa za kufanya usajili wa kufuru kama zamani, lakini hali kwa sasa imebadilika na inaonekana mabosi wa Yanga wanakula sahani moja na bilionea wa Simba Mohamed 'Mo' Dewji."

Maana halisi ya 'kufuru' ni kitendo cha kusema au kutenda jambo lililo kinyume na dini; kitendo cha kumkana Mungu. Tamko au tendo lililo kinyume na dini au kumkanusha Mungu. Mwandishi anapoandika " ...usajili wa kufuru ..." ana maana ya 'usajili wa kumkana Mungu' au ana maana gani?

Kuandika au kusema 'chama lao' badala ya 'chama chao' ni kosa ingawa magazeti ya michezo huandika 'chama lao' kila mara. Badala ya kuandika 'chama lao' iandikwe 'chama chao, klabu yao' au 'timu yao.'

"Pacha wa Kagere mzuka kama" ni kichwa cha habari ya gazeti la michezo. Kwanza kichwa chenyewe hakikukamilika na kwa hiyo hakina maana yoyote kwa wasomaji. Pili 'mzuka' nimelitolea ufafanuzi mara nyingi sana kwenye safu hii kumbe natwanga maji kwenye kinu! Niandikaje ili nieleweke au wenzangu hudhani mimi ndiye nisiyeelewa?

Jamani! (tamko la kuwataka watu wasikilize. Tamko la kuonesha hisia ya kukerwa), 'mzuka' ni kiumbe kisichoonekana ila hudhaniwa kuwa kinaishi na huweza kumtokea mtu; pepo. Sijui kwa nini waandishi wa habari za michezo hupenda mno kulitumia neno hilo!

"KADAMSHI Koku wa kapuni, ye na Manula tu!" Kama mwandishi anaandika habari au makala kwa kutumia maneno yasiyoeleweka, anafanya kazi bure. Nimeshindwa kupata maana ya 'kadamshi.' Nitumiapo maneno ninayohisi hayaeleweki vizuri, huyatolea maana yake. Kwa mfano, 'kesa' ni kitendo cha kuondoka wingu la mvua. Kwa maana hii, wasomaji hujua maana ya neno nililotumia.

Methali: Jawabu wakatiwe, na wakatiwe si zani.

***marobarnabas@yahoo.com***
***0784 334 096***

## NA MWALIMU REUBENI LUMBAGALA

# Wanafunzi likizo imekwishamalizika, rejesheni fahamu zenu shuleni



Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Ipembe, Nyerere, Unyankindi na Singidani katika Manispaa ya Singida.**PICHA: MTANDAO**

LIKIZO kwa muktadha wa shule ni muda wa mapumziko wanaopewa walimu na wanafunzi, baada ya kusoma kwa kipindi fulani ili kujiandaa kwa kipindi kingine cha masomo.

Ijumaa ya tarehe 7 Juni 2019, shule za msingi na sekondari hapa nchini zilifungwa kwa muda wa mwezi mmoja kwa ajili ya likizo ya nusu muhula.

Na Jumatatu wiki iliyopita, yaani Julai 8, shule zote za msingi na sekondari nchini zilifunguliwa ili kuanza muhula wa pili na wa mwisho kwa mwaka wa masomo 2019.

Likizo ni haki ya wanafunzi na walimu ili kupumzisha bongo, baada ya kusoma kwa muda mrefu.

Mwezi mmoja wa likizo umekuwa ni wakati mzuri kwa baadhi ya wanafunzi kuendelea kuhudhuria masomo ya ziada (tuition) na kujisomea.

Lakini wapo wengine pia ambao hawakubahatika kusoma masomo ya ziada, walibaki nyumbani kusaidia kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupumzika.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanafunzi huacha kujishughulisha kujisomea katika muda wote wa likizo na hivyo kujikuta wakisahau maarifa mengi waliyofundishwa na walimu wao kabla ya kufunga shule, kutokana na kushindwa kujisomea.

Makala haya haiwalaumu wanafunzi hao waliotumia muda wa likizo kupumzika kwani kupumzika ni jambo la msingi kwa afya ya ubongo.

Angalizo ambalo Kalamu ya Mwalimu inaitoa kwa wanafunzi ni kuwa, muda wa kupumzika umekwisha na sasa wamerejea shule kuanza masomo kwa mara nyingine tena.

Hivyo warejee katika ratiba zao za kujisomea kama ilivyokuwa kabla ya kufunga shule.

Yapo mambo kadhaa ambayo wanafunzi wanapaswa kuyatekeleza baada ya kufungua shule, ikiwa ni pamoja na kuamka mapema.

Mwanafunzi anapaswa kuamka mapema kwenda shule kujifunza.

Nasema hivyo kwa sababu kipindi cha likizo, baadhi ya wanafunzi hutumia muda mwingi kulala kutokana na uhuru uliopo kipindi cha likizo.

Kwa sababu ya hali hii, wanapaswa kuachana na tabia ya kulala muda mrefu kwani sasa shule zimefunguliwa.

Katika muktadha huu, wanapaswa kuwahi kuamka na kufanya maandalizi ya kwenda shule ili kuepuka adhabu za kuchelewa kufika shule kwa wakati.

**MALENGO**

Lakini lingine la msingi ni kuwa na malengo na mikakati ya kufanya vizuri kwa muhula wa masomo aliouanza.

Lazima mwanafunzi ajiwekee malengo ambayo anataka ayafikie kwenye muhula mpya aliouanza mwezi huu.

Mikakati ya kufikia ufaulu wa juu ni lazima iwekwe ili iwe na hamasa kwa mwanafunzi kujifunza na kusoma kwa bidii.

Mwanafunzi anapaswa kuyafanyia kazi yale maoni ya walimu wake wa masomo waliyoyatoa katika Ripoti ya Maendeleo ya Mwanafunzi (=E2=80=9C) na Ripoti iliyotolewa na walimu siku ya kufunga shule (=E2=80=9D).

Ripoti hiyo huonyesha alama na wastani aliopata kwa masomo yote pamoja na nafasi aliyoshika kitaaluma.

> Angalizo ambalo Kalamu ya Mwalimu inaitoa kwa wanafunzi ni kuwa, muda wa kupumzika umekwisha na sasa wamerejea shule kuanza masomo kwa mara nyingine tena.

Mwanafunzi aliyefanya vizuri au vibaya ana wajibu wa kusoma kwa bidii ili kupata alama za juu katika masomo yake.

**RATIBA YA KUJISOMEA**

Lingine la muhimu ni la kuendeleza ratiba za kujisomea kwa bidii.

Mwanafunzi makini huwa na ratiba ya kumuongoza ili aweze kujiandaa vyema kimasomo na hatimaye kufanya vizuri katika masomo yake.

Hivyo basi, kwa wanafunzi ambao hawakuwa wakiendeleza ratiba za kujisomea wakati wa likizo, wanapaswa kuanza rasmi kujisomea kwa bidii kwani shule zimefunguliwa na mada za kujifunza darasani zitaongezeka kutokana na kuanza muhula mpya wa masomo.

Kwa mwanafunzi ambaye hakuwa na ratiba ya kumuongoza kujisomea anapaswa kuandaa ratiba yake na kuanza kuitekeleza kwa vitendo.

Na hiyo ni katika kujiweka kwenye nafasi nzuri za kufanya vyema katika masomo yake ili kusonga mbele zaidi kitaaluma na kimaisha.

**NIDHAMU**

Vilevile kuzingatia nidhamu, utii wa sheria na kanuni za shule.

Nidhamu ni jambo la msingi sana kwa wanafunzi ili waweze kuishi kwa amani shuleni na kuepuka adhabu zisizo za lazima.

Likizo inaweza ikawa imewasababishia wanafunzi kuishi nje ya nidhamu na utii wa sheria za shule. Wanafunzi hawapaswi kuishi maisha ya holela baada ya shule kufunguliwa.

> Kwa mwanafunzi ambaye hakuwa na ratiba ya kumuongoza kujisomea anapaswa kuandaa ratiba yake na kuanza kuitekeleza kwa vitendo.

Nidhamu inapaswa kuendelea kama kawaida na kwa kiwango kinachotakiwa.

Aidha, zipo sheria na kanuni zinazoongoza shule, ambazo wanafunzi wanapaswa kuzitekeleza.

Baada ya kufungua shule, upo umuhimu wa wanafunzi kuzisoma tena sheria na kanuni za shule ili kujikumbusha wajibu wao wawapo shuleni na hata nje ya shule.

Kwa kufanya hivyo, wanafunzi hawataingia katika migogoro na walimu wao kwa kuvunja kanuni, sheria za shule na kuwa na nidhamu isiyofaa.

Wanafunzi waendelee kuzingatia yale yote wanayoelekezwa na walimu na wazazi wao ili kufanikiwa kitaaluma na kimaisha pia.

Wanafunzi washirikiane katika kujisomea na kuelekezana mambo yenye faida kwa maisha yao ya sasa na ya baadaye.

Likizo imekwishapita na mambo yake, sasa ni wakati wa kusoma tu.

Nawatakia wanafunzi wote muhula mpya wa masomo. Waongeze bidii katika kujisomea huku wakimtanguliza Mungu katika masomo yao, hakika watafanikiwa. Tafakari.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoa wa Dodoma.

***Maoni: (+255) 764 666349.***

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Angalizo la Mkapa litasaidia vyuo vikuu binafsi nchini

RAIS mstaafu Benjamin Mkapa hivi karibuni ametoa rai kuwa serikali isivione vyuo vikuu binafsi, vikiwemo vya mashirika makubwa ya kidini au kidhehebu, kama washindani na kujenga hisia fulani ya uadui, na badala yake waone kama wenza, washirika kuendeleza elimu ya juu nchini.

Ni rai ambayo ilihitaji kupata msemaji wa ngazi ya juu kijamii, ambaye hawezi kupuuzwa na walioshika madaraka kuhusu suala lolote linalomkera au anatoa wazo la kutaka marekebisho.

Hakuna majibu au maelezo ambayo yametolewa serikalini kuhusu rai hiyo, ila kwa hakika itakuwa na matokeo chanya.

Katika hatua ambazo zimechukuliwa na wizara haikusemwa waziwazi kuwa zinalenga kupunguza idadi ya vyuo binafsi, lakini ilionekana wazi kuwa suala la viwango limechukuliwa kwa uzito usio wa kawaida, tena si kwa kuelekeza marekebisho bali kufunga kabisa.

Hatua kama hiyo inazuia kuboresha kwani vyuo vinaboreshwa kwa kuweka mikakati ndani ya mpangilio wa kutoa huduma na kupata ada, wakati ambapo chuo kikifungwa maana yake ni kuwa juhudi za kutafuta mtaji wa awali kufungua chuo zianzishwe upya.

Ni hatua inayokatisha moyo wadau wa elimu ya juu, na ni kama serikali kujikana yenyewe, kwa leseni.

Hapo ndipo suala la msingi lilipo, kwa kufunga vyuo siyo suala la kuzorota kwa huduma, kwani hiyo inaweza kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Vyuo Vikuu (TCU) ikisaidiana na Bodi ya Wadhamini ya chuo husika.

Hakuna bodi inayoweza kupuuzia utafiti na ripoti ya kina ya tume hiyo kuhusu huduma zake kwani chuo binafsi kina kazi ngumu zaidi ya kujenga imani kwa wananchi, watumiaji kuliko chuo cha serikali, au kwa lugha tuliyozoea, chuo cha umma.

Sababu ni kuwa zikitoka kwa mfano taarifa katika vyombo vya habari ambazo si njema kwa chuo cha serikali, watawala wizarani watakikingia kifua, n.k.

Ina maana kuwa kufunga vyuo siyo kugundua ubovu au mapungufu bali kubadilisha kanuni kwa kutoa tafsiri hasi ya jinsi kanuni zilivyotumika, halafu tofauti kati ya tafsiri ya awali na tafsiri mpya inakuwa ni bili anapelekewa mteja.

Atahitaji shilingi milioni 300 azitoe ghafla bin vu kurekebisha hali ilivyo, jambo ambalo hataweza na mtawala akijua hivyo, anatoa ilani ya kufunga chuo kwa kutumia vigezo hivyo, ila inaonekana kana kwamba chuo kimekiuka kanuni wakati hali halisi ni kuwa zimetafsiriwa upya.

Ndiyo hapo wadau wanalalamika kwa rais mstaafu kuwa hawana mtetezi, waliowatumainia wamekuwa washari.

Mabadiliko ya mwelekeo wa maofisa wa serikali (watawala katika mamlaka husika) kuhusu vyuo vikuu ambayo rais mstaafu anayataka hayatofautiani na mabadiliko ambayo Rais Dk. John Magufuli amekuwa akiitaka Mamlaka ya Mapato (TRA) kuzingatia.

Ni kuacha tabia ya kuwaona wafanyabiashara, yaani wale ambao ndiyo wahusika wake katika shughuli zake za kila siku, kama maadui - yaani kundi kubwa la wakwepa kodi.

Waanze kuwaona wafanyabiashara kama washirika kitaifa katika jukumu kubwa la uwekezaji na kutengeneza ajira, kwani kuzorotesha biashara na kutazamia serikali iunde ajira ni ndoto.

Ndicho kimsingi anachokitaka rais mstaafu na kinacholiliwa na wadau katika sekta binafsi ya elimu kwa jumla na elimu ya juu ambako kuna ushindani mkali wa kiitikadi kati ya wapenda maendeleo na mabadiliko kuelekea dunia ya kisasa, utandawazi, na wahafidhina wanaoona kuwa nchi imepoteza dira.

Ni katika eneo hilo ambako kuingia madarakani kwa awamu ya tano na hatua zilizochukuliwa mwanzo wa utawala huu zilileta matumaini kwa wahafidhina kuwa sasa nchi inarudi pale inapotakiwa kuwa, yaani kufuata nyayo za Mwalimu Nyerere, Ujamaa na Kujitegemea. Vyuo vikuu binafsi si ujanja tu, kutajirika?

Yako maeneo mengine ya kiitikadi ambayo siyo ya suala la kujitajirisha, kwani suala hilo haligusi vyuo vikuu vinavyomilikiwa na mashirika ya dini, hasa makanisa lakini ukiangalia kwa karibu unakuta kuna changamoto lukuki za kiitikadi katika eneo hilo vile vile.

Ni suala la aina ya hisia inayojengwa katika maeneo hayo, hali ambayo inakumbushia kubomolewa kwa makundi huru ya kiraia kati ya mwaka 1964 na 1968 katika mwenendo wa kujenga 'demokrasia ya chama kimoja.'

Ilikuwa ni kuondoa vianzio vya upinzani kwa TANU, siyo tu kwa sababu TANU ilitaka kutawala milele lakini viashiria vya machafuko kuhusu sera, hasa viwango vya malipo kwa watumishi wa serikali, matakwa ya maofisa wa jeshi au polisi -kuacha minong'ono ya nani kapewa cheo na kwanini.

Mwalimu akaona hapo kuna bomu la kutegwa.

Kutokana na kuondolewa kwa vihatarishi vya aina hii kwani nchi imekomaa na ina wingi wa wataalamu na imechanganyika kiasi kwamba ajenda za mwaka 1965 na vihatarishi vya amani hazina uhusiano na hali ya sasa, ndiyo linakuja suala la uhafidhina.

Ni kujenga woga kuhusu sekta binafsi, kuona kama njia ya kuuacha Utanzania (hoja aliyotoa katika mada ndefu mlezi wa uhafidhina nchini hivi sasa, mkurugenzi mtendaji wa Mfuko wa Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku katika kongamano la kumbukumbu ya miaka 10 ya kifo cha Mwalimu, mwaka 2009). Alisema kwa jumla 'tumepoteza utu wetu, Uafrika wetu na Utanzania wetu' katika mada yenye kichwa cha somo 'Watu: Hoja Kuhusu Watu' ikapeta bila majibu.

Inaendelea Uk. 18



Baadhi ya wahitimu wa shahada mbalimbali kutoka mojawapo ya vyuo vikuu binafsi nchini.
**PICHA: MTANDAO**

> Hakuna bodi inayoweza kupuuzia utafiti na ripoti ya kina ya tume hiyo kuhusu huduma zake kwani chuo binafsi kina kazi ngumu zaidi ya kujenga imani kwa wananchi, watumiaji kuliko chuo cha serikali...



Rais Mstaafu wa awamu ya tatu Benjamin Mkapa akiongea na wageni waalikwa wakati wa uzinduzi wa safari ya miaka mitano ya Chuo Kikuu cha Mt. Augustino cha Tanzania (SAUT) kuelekea Jubilei ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1998.

> Mabadiliko ya mwelekeo wa maofisa wa serikali (watawala katika mamlaka husika) kuhusu vyuo vikuu ambayo rais mstaafu anayataka hayatofautiani na mabadiliko ambayo Rais Dk. John Magufuli...

JIELIMISHE

## UNESCO YAUTAMBUA MJI WA BABYLON ENEO LA KIHISTORIA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), limeutambua mji wa kale wa Babylon kuwa eneo la kihistoria.

Nchi ya Iraq imekuwa ikishinikiza tangu mwaka 1983 mji huo wa kale wa miaka 4,000 ujumuishwe katika orodha ya kifahari ya Umoja wa Mataifa (UN).

Mji huo ulijulikana kwa bustani zake za kuning'inia, ambazo zilikuwa kati ya Maajabu Saba ya Dunia ya vitu vya kale duniani.

Katika miaka ya hivi karibuni, eneo hilo limeharibiwa kufuatia ujenzi wa kasri la Saddam Hussein na baadaye kutumiwa kama kambi ya kijeshi na vikosi vya Marekani.

Kamati ya Urithi wa Dunia ya UN ilikutana nchini Azerbaijan kuamua kuhusu maeneo mapya ya kale ambayo yanastahili kutambuliwa ili yapewe tuzo kuwa maeneo au nembo ya kihistoria inayozingatia umuhimu wa binadamu wote na kulindwa na mikataba ya kimataifa.

Ujumbe wa Iraq ulikaribisha hatua hiyo, ukisema kuwa huu ni utambuzi wa mchango wa Babylon katika ustaarabu wa Mesopotamia.

Ikitangaza uamuzi huo, Unesco ilisema: "Hatua hii inaashiria kutambuliwa kwa ubunifu wa hali ya juu wa mji wa Babylon na kuhusishwa kwake na moja ya maajabu saba ya vitu vya kale duniani."

Pia ilionya kuwa maeneo hayo yako katika "hali mbaya" na kwamba yanahitaji kuhifadhiwa haraka iwezekanavyo.

### NI MAENEO YAPI MAPYA YA KIHISTORIA DUNIANI?

Hayo ni pamoja na Babylon, Iraq, maeneo ya kale ya Pharaoh wa Burkina Faso, Paraty and Ilha Grande, Brazil, Hifadhi ya Kitaifa ya Vatnajökull, Iceland na visiwa na bahari ya mbali vinavyomilikiwa na Ufaransa.

Aidha, Urithi wa asili na Utamaduni wa Mkoa wa Ohrid, Albania, muendelezo wa upande wa Ziwa la Kaskazini mwa Macedonia, ambao umekuwa katika orodha ya maeneo ya kihistoria tangu mwaka 1979.

Ofisa Mkuu Mtendaji wa muda kwenye Mfuko wa Dunia wa Makumbusho wenye makao yake jijini New York nchini Marekani, Lisa Ackerman, ameiambia BBC kuwa shirika hilo lisilokuwa la kiserikali limekuwa likifanya kazi na Serikali ya Iraq kwa miaka kuhifadhi uwanja wa Babylon.

Anasema si jambo la kawaida kwa wanaharakati kushawishi kwa miongo kadhaa mji huo wa kale kutambuliwa kama eneo la kihistoria duniani.

### 'KUHARIBIWA VIBAYA'

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, rais wa zamani wa Iraq, Saddam Hussein, aliharibu sehemu kubwa ya makaburi ya kihistoria na kujenga nyumba zingine zilizofanana na zile za zamani.

Baada ya vita vya ghuba, pia alijijengea kasri la kisasa upande wa pili la eneo hilo.

Mwaka 2005, Makavazi ya kitaifa ya Uingereza yalionya kuwa vikosi vya muungano vinavyoongozwa na Marekani vinasababisha uharibifu mkubwa katika mji huo wa kale.

John Curtis, ambaye ni mshirikishi wa makavazi hayo kitengo cha Mashariki ya Kati wakati huo, alionya katika ripoti yake kwamba magunia ya kubeba mchanga yamejazwa mabaki ya akiolojia ambayo inakadiriwa kuwa na miaka 2,600 na kubakisha mawe yaliyoharibiwa eneo hilo liliposhambuliwa.

Pia alipata ushahidi wa mafuta kuvuja katika mitaro ya inchi 12, ambayo ilichimbwa katika migodi ya madini hayo.

Ni sawa na "kujenga kambi ya kijeshi karibu na eneo hilo la kihistoria," alisema wakati huo.

Miaka minne baadaye, Unesco ilisema kuwa "Matumizi wa Babylon kama kambi ya kijeshi ni uvamizi mbaya wa eneo linalotambuliwa kimataifa kama eneo la vito vya kale."

**BBC**



Mji wa Babylon ambao umekuwapo kwa miaka takriban 4,000.
**PICHA: MTANDAO**

# Angalizo la Mkapa litasaidia vyuo vik

Inatoka Uk. 17

Juhudi za wahafidhina kubadili mwelekeo wa nchi kurudi katika Ujamaa na Kujitegemea ni pamoja na hoja ya miaka mingi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo Mwalimu aliikataa kata kata wakati wa maisha yake, ya kubadili mfumo wa kufundishia sekondari, vyuo na vyuo vikuu kutoka Kiingereza na kuwa Kiswahili.

Mwalimu alielewa madhara ya mabadiliko kama hayo lakini wahafidhina walikataa hoja hiyo, na wamejaribu awamu zote zilizofuata kufikia malengo yao.

Hivyo kuondoa vyuo vikuu binafsi au kuvipunguza visiweze kuhoji sera za serikali, viwe viambata tu vya vyuo vikuu vya serikali ni muhimu kwa mkakati huo wa Kiswahili kufaulu; hata siku moja shule na vyuo binafsi havitakikubali Kiswahili.

Kuelekea mwisho wa awamu ya nne wahafidhina, ambao wanasikilizwa sana serikalini lakini kunakuwa na vitahadhari vya hapa na pale ambavyo watawala wanakumbuka hivyo wasitekeleze 'ushauri nasaha' wa wahafidhina, waliweka mkakati wa 'chenga ya mwili' na kufunga bao.

Lakini serikali iliyoingia madarakani ikaona lilikuwa ni bao la kuotea, na bila kusema lolote, wakapuuzia sheria zilizopitishwa kwa haraka haraka bungeni Septemba 2015 kuhusu lugha, licha ya kuwa sheria nyingine za eneo hilo zilibaki na zimetekelezwa, zikiwemo sheria zinazogusa takwimu, mafuta na gesi, na moja au mbili nyingine.

Ni wakati Bunge la Bajeti limemalizika, wagombea wakuu wameshatajwa, halafu muswada muhimu uende bungeni kinyemela, upitishwe na wabunge takriban 50, yaani mradi tu ile 'quorum' ya kikao imetimia.

Muswada huo kuhusu elimu uliainisha kuwa elimu ya msingi itaishia miaka sita, halafu sekondari itaendelea kuanzia mwaka wa saba hadi kumi (miaka minne kama kawaida), na baada ya hapo ni elimu ya vyuo vya ngazi tofauti, ikiwa ni pamoja na matayarisho ya elimu ya chuo kikuu, n.k.

Dhamira ya mpango huo haikuwa kuboresha elimu au kufanya sekondari iwe rahisi kwa wanafunzi wote bali

## JE, WAJUA?



Meghan Williams (kushoto) na mumewe Chris, wakiwa na ngamia wanaowafuga. **PICHA: MTANDAO**

# Kwanini matumizi ya maziwa ya ngamia yanaongezeka duniani?

MAZIWA ya ngamia, yametumika na binadamu kwa zaidi ya miaka 6000, na mahitaji yake yanaonekana kuongezeka katika miaka ya hivi karibuni duniani, licha ya gharama yake kubwa.

Mara nyingi maziwa ya ngamia hutumiwa na jamii za wafugaji na wahamiaji katika ukanda wa Afrika Mashariki na pembezoni.

Jamii za Wasomali, Wa-Borana Wa-Rendile na hata Wa-Turkana zinazopatikana katika maeneo hayo hutumia maziwa ya ngamia kwa kiasi kikubwa kutokana na faida zake kama vile kusafisha mwili na kuboresha afya ya watoto wanapokua.

Kadhalika kuna baadhi ambao wanaamini kuwa maziwa hayo husaidia kumfanya mtu kuwa hodari, mchangamfu na kuchagiza nguvu za kiume, licha ya kwamba haya hayajathibitishwa rasmi kisayansi.

Ni kutokana na faida kama hizi ambazo zimechangia wengi duniani kutafuta na kuanza kutumia maziwa ya ngamia.

**FAIDA ZA MAZIWA YA NGAMIA**

Maziwa ya ngamia yanazidi zaidi maziwa na ng'ombe kwa vitamini C, vitamini B, madini ya iron, calcium, magnesium na potassium.

Yanatajwa kuwa na uwezo kupunguza uzio dhidi ya baadhi ya vyakula unaojitokeza kwa misimu.

Pia hupunguza utegemezi wa insulin na dawa za kutibu kisukari kwani imebainika kwamba, kunywa maziwa ya ngamia huchangia kupunguzwa kwa dozi ya insulin kwa wagonjwa wa kisukari cha aina ya kwanza.

Vilevile hushinikiza kinga mwilini kwa mujibu wa utafiti uliochapishwa katika jarida la utafiti wa bidhaa za maziwa. Utafiti huo umefichua kwamba kuna viwango vikubwa vya protini katika maziwa ya ngamia na baadhi yake vina dawa inayoua vidudu mwilini.

Aidha, hushinikiza ukuaji kutokana na protini nyingi iliomo kwenye maziwa ya ngamia tofauti na maziwa na ng'ombe na mbuzi. Hivyo hushinikiza ukuaji mzuri wa mifupa na ufanyaji kazi wa mifumo ndani ya mwili.

Vilevile maziwa ya ngamia yana uwezo wa kusawazisha viwango vya cholesterol mwilini.

Lakini madini mengi ya chuma au iron ndani ya maziwa hayo pia husaidia kuzuia upungufu wa damu mwilini.

**JE UNAWEZA KUNYWA MAZIWA YA NGAMIA?**

Katika eneo la Mashariki ya Kati ni kinywaji muhimu cha kitamaduni. Kilisaidia waarabu wa kuhamahama wa jamii ya Bedouin kwa karne nyingi.

Marekani, India, China na Urusi ni mataifa yanayotajwa kuwa masoko makuu ya maziwa hayo kwa mujibu wa wataalamu.

Licha ya kwamba maziwa haya hutumika sana katika mataifa ya Kaskazini na Mashariki mwa Afrika na eneo la Mashariki ya Kati, ripoti ya mwaka 2016 ya Serikali ya Australia inatabiri kwamba

"Miaka mitano kuelekea 2021 kunatarajiwa kushuhudiwa ongezeko la uzalishaji maziwa ya ngamia nchini humo."

Soko la maziwa ya ngamia linazidi kuwa kubwa kutokana na ongezeko la mahitaji ndani na hata nje ya nchi hiyo.

**USHUHUDA**

Meghan Williams na mumewe Chris walianzisha ufugaji wa ngamia mnamo 2014 wakiwa na ngamia watatu ambao iliwabidi wawafunze kukamuliwa maziwa.

Miaka mitano baadaye, biashara yao - The Camel Milk Co Australia imeshamiri maradufu na sasa wana ngamia 300, kati yao 60 wakitumika kwa kukamuliwa maziwa.

"Mara nyingi huwa tunafuatwa na wateja wa kimataifa na masoko yao. Jambo moja tunalojivunia Australia dhidi ya mataifa mengine duniani ni kwamba ngamia wetu hawana magonjwa," anasema Meghan.

Ngamia alitumika Australia, mara ya kwanza katika miaka ya 1840 kusaidia kwenye suala la usafiri kwa sehemu kubwa ya nchi hiyo.

Inakisiwa kwamba kuna ngamia milioni 1.2 jangwani, baadhi wakiwa ni wa asili ya kiarabu, walio na nundu moja mgongoni na ndio wanaotumika kukamuliwa maziwa. BBC

## UTAFITI

### MAUAJI YA BILA KUKUSUDIA YALETA VIFO ZAIDI YA MIZOZO

TAKRIBAN watu 464,000 kote duniani waliuawa bila kukusudia mwaka 2017, idadi iliyopita kwa mbali ile ya watu 89,000 walioуawa kwenye mizozo na vita katika kipindi kama hicho.

Hiyo ni kwa mujibu wa utafiti uliofanyika dunia nzima kuhusu mauaji ya bila kukusudia mwaka 2019 na kuchapishwa wiki iliyopita na Ofisi ya Umoja wa Mataifa Inayoshughulikia Dawa na Uhalifu (UNODC). "Utafiti wa dunia nzima kuhusu mauaji ya bila kukusudia unaweka wazi suala la mauaji kwa misingi ya kijinsia, yanayotokana na magenge ya uhalifu na changamoto zingine ili kusaidia kupunguza viwango vya mauaji bila kukusudia," anasema Mkurugenzi Mtendaji wa UNODC, Yury Fedotov.

Fedotov anabainisha kwamba nchi zimeahidi viwango vya chini vya maendeleo endelevu kupunguza kila aina ya ghasia na vifo vitokanavyo na ghasia ifikapo mwaka 2030.

Utafiti huo unaonyesha idadi ya watu waliokumbwa na mauti yaliyotokana na mauaji ya kutokusudia iliongezeka katika robo ya kwanza ya karne kutoka watu 395,542 mwaka 1992 hadi 464,000 mwaka 2017.

Hata hivyo, sababu kuwa idadi ya watu duniani imeongezeka kwa kasi kuliko ile ya visa vya mauaji yasiyo ya kukusudia, imeshuka taratibu.

**UHALIFU ULIOPANGWA HUCHANGIA 19% YA MAUAJI YASIYO YA KUKUSUDIA**

Uhalifu uliopangwa pekee ulichangia hadi asilimia 19 ya mauaji yote ya bila kukusudia mwaka 2017.

Tangu mwanzo wa karne ya 21, uhalifu uliopangwa ulisababisha vifo vya watu wengi sawa na vifo vinavyotokea kwenye mizozo kote duniani kwa jumla.

Sawa na mizozo, uhalifu uliopangwa huathiri mataifa, maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuhujumu sheria.

**VIWANGO VYATOFAUTIANA**

Viwango vya mwaka 2017 vya dunia vya mauaji ya bila kukusudia ni tofauti kimaeneo.

Viwango katika mataifa ya Amerika vya (asilimia 17.2) vilikuwa vya juu kurekodiwa eneo hilo tangu kumbukumbu zianze kuwekwa 1990. Viwango vya Afrika (asilimia 13.0) vilikuwa pia vya juu huku vile vya Asia, Ulaya na Oceania vikiwa chini (asilimia 2.3, asilimia 3.0 na asilimia 2.8 kwa kufuatana).

Licha ya viwango ya mauaji ya bila kukusudia kusalia kuwa vya juu katika mataifa ya Amerika, mambo ni tofauti katika kanda hiyo na pia kati ya nchi.

Huko Amerika ya Kati nchi yenye viwango vya juu zaidi vya (asilimia 62.1) ina viwango zaidi ya mara saba ya vile vya nchi iliyo na viwango vya chini zaidi. Kwa Marekani Kusini, nchi yenye viwango vya juu zaidi vya mauaji yasiyo ya kukusudia vya asilimia 56.8, ilikuwa na viwango mara 16 zaidi ya nchi yenye viwango vya chini zaidi.

**WAATHIRIWA WENGI ZAIDI NI WANAUME,**

...Wanawake mara nyingi huuliwa na familia au wapenzi.

Kote duniani asilimia 81 ya waathiriwa wa mauaji yasiyo ya kutarajia vilivyorekodiwa mwaka 2017 walikuwa ni wanaume na watoto wa kiume. Aidha, zaidi ya asilimia 90 ya washukiwa katika visa hivyo walikuwa ni wanaume kwa mujibu wa makadirio.

Hata hivyo, utafiti unaonyesha kuwa tofauti kwa misingi ya jinsia kati ya waathiriwa inabadilika kulingana na umri.

Katika maeneo yote, uwezekano wa wavulana kuwa waathiriwa wa mauaji yasiyo ya kukusudia huongezeka kwa umri, licha ya visa hivyo kutokea katika umri tofauti.

# kuu binafsi nchini

kufuta hatua ya mabadiliko kutoka shule ya msingi kwenda sekondari, hivyo kubakiza mazingira yale yale ya kufundisha kwa Kiswahili.

Huwezi kusema rais mstaafu Jakaya Kikwete alikubaliana na mpango huo kwa kina lakini siasa ni kuwaruhusu watu wajieleze na kujikusanya ili kiongozi asilaumiwe kwa kuwanyamazisha, lakini alikuwa anajua kuwa ni mrithi wake atakayekuwa na jukumu la kutekeleza sera hiyo. Akikubali, hewala!

> Hivyo kuondoa vyuo vikuu binafsi au kuvipunguza visiweze kuhoji sera za serikali, viwe viambata tu vya vyuo vikuu vya serikali ni muhimu kwa mkakati...



## UCHAMBUZI WA KITABU;

# No Mud, No Lotus: The ART of Transforming Suffering by Thich Nhat Hanh (Sanaa ya kubadili Mateso kuwa ushindi na furaha)

KATIKA maisha watu wengi wanateseka kwa sababu ya kutojua namna vitu vilivyo, vinavyokuwa na namna ya kukabiliana navyo.

Hapa ndipo chimbuko la mateso kwa watu wengi duniani lilipo.

Kama si mateso ya mwili moja kwa moja, basi ni mateso ya kifikra ambayo huwa hayaachi kuwaandama mpaka pale siku ambapo watajua kweli ilipo na kukubali, kisha kuchukua hatua ya kufuata au kubadilika.

Mwandishi wa kitabu hiki kaelezea kwa mapana namna ya kujiweka huru katika maisha pale unapojua uwepo wa kitu na kukikabili kama njia ya kubadili mateso kuwa ushindi na furaha.

Ukijua mateso yanasababishwa na nini na ukawa na uwepo wa akili (mindfulness) kuwa maisha yana mateso, basi utakuwa umejua ukweli mmoja wa dhahabu (noble truth) utakaokutoa katika lindi la kuendelea kuteseka kwa kukosa maarifa (Ujinga).

Furaha ni somo ambalo linaweza kuelezeka zaidi kwa mtu mmoja hata mwingine kwa jinsi aonavyo.

Wakati wapenzi wawili walopanga kwenda katika matembezi kuzungumza juu ya maisha yao ya baadaye, mvua inyeshapo wanaweza kukereka sana na hata wakapoteza furaha.


Wakati huo huo mkulima wa kule Dodoma, Mbeya, Rukwa au Morogoro kwake ni furaha kubwa sana, sababu mvua ndilo lilokuwa ombi lake.

Kadri ambavyo katika maisha unajitahidi kukimbia uhalisia ulivyo, ndivyo ambavyo unajitengenezea mateso na hatari kubwa zaidi.

Hapa tumeona watu waloingia kufanya tabia hatarishi kama kunywa pombe na hata wengine kuvuta sigara pale walipokuwa wakiukwepa uhalisia wa maisha ulivyo, kumewaletea uraibu na matatizo makubwa.

Furaha si hali inayodumu, ni kama vile sarafu inaweza kugeukia upande wowote na upande huo ni mateso na mateso unapoyakubali ndivyo inavyokuwa rahisi sana kuirudisha furaha na maisha yakaendelea vizuri zaidi. Shida ni kuwa watu wengi hawakubaliani na upande wa mateso kama ni sehemu pia ya furaha ukikubali kuwa yapo.

Kama utakuwa mdadisi mzuri sana wa mazingira utakubaliana kabisa kwamba 'ua' ni matokeo ya vitu ambavyo si sehemu ya ua. Kivipi ? Mwanga wa jua, mawingu, ardhi ni




mazingira ambayo yanafanya mmea utokee na kisha ua liwepo.

Licha kuwa si sehemu ya ua lakini kukosekana kwa mwanga wa jua, mawingu au ardhi hakuna matokeo ya mmea. Hivi ndivyo ilivyo kwa furaha kuwa mateso kuwapo ndio chimbuko la furaha.

Tunapokuwa mbali na miili yetu, ndipo tunapokosa kujua mambo yanayotuzunguka na kwa kufanya hivi akili zetu huwa zinakuwa hazitulii na kwa kuwa hazitulii basi ni rahisi sana kufanya mambo ambayo yatazidisha mateso katika maisha yetu.

Wakati mwingine watu wanaendelea kuwa katika mateso makubwa sababu ya kumbukumbu ambazo wamezipitia huko nyuma.

Huenda ni kufanyiwa unyama, kukataliwa, kuondokewa na wapendwa wao, ajali na mengine mengi yanayofanana nayo. Kinachoongeza maumivu zaidi kwa mnyama aliyechomwa mkuki ni ule mkuki kuchoma tena mara ya pili hapo hapo.

Nini maana yake? Katika maisha watu wanajiongezea mateso zaidi pale wanaporuhusu tafsiri ya kitu hicho, pale wanapoweka hisia zao na hata vile hofu wanazozijenga hapo.

Hapa inakuwa kama mkuki wa pili katika kidonda ambacho maumivu yake ni zaidi ya mkuki wa kwanza.

**NJIA**

Njia bora ya kulitatua tatizo ni kuliona katika uhalisia wake kama lilivyo. Wengi wanapata mateso zaidi sababu hawaoni tatizo kama lilivyo.

Jifunze kuachilia yaliyopita na uanze kuishi sasa. Huwezi kubadili yaliyopita, mbali na kuweza kujifunza somo kwa yaliyokwishatokea.

Unahitaji kuwa na hali ya mapumziko katika maisha yako ili upate muda wa kufahamu mengi yanayoendelea katika maisha yako kwa ukaribu zaidi.

Maana pale unapokosa muda wa kupumzika, kuna vitu unaweza ukawa ukiendelea kuvifanya kwa makosa bila kujua.

Kila siku jifunze kufanya katika ubora, kufanya matendo ya upendo na furaha ambayo yatatia thamani kwa maisha ya watu na njia hii ni bora sana kulisha furaha yako kwa hatua za juu zaidi kila siku katika maisha.

Unahitaji ujue kufanya tahajudi na mojawapo ni kujipa utulivu mkubwa na ukae uandike maono yako makubwa na kuangalia ulipofikia.

Maana umekuwa unakimbizana sana na maisha kiasi kwamba umekosa hata muda wa kujisikiliza unataka ufike wapi, na wapi uendako !

Na mwisho inatia moyo sana pale ambapo katika mateso tunayopitia kuna watu kama hawa wasemao 'nipo kwa ajili yako, najua unapitia magumu lakini nina furaha kuwa utashinda.'

Mateso yanapokuwa na mwitikio wa umoja na kuwa tayari kushughulika nayo huwa ni faraja na matumaini makubwa zaidi. Yaelewe maisha katika pande zake zote mbili kuwa furaha na mateso ni sehemu ya maisha makamilifu.

***Mchambuzi wa kitabu, ni Dk. Raymond Nusura Mgeni-2019***
***+255 676 559 211***
***raymondpoet@yahoo.com***




Ili kufanikiwa katika maisha mtu anahitaji kusonga mbele bila kuangalia ya nyuma.
**PICHA: MTANDAO**



# WADAU SABATO KASIKA

## Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa ameiomba serikali kuweka mazingira yenye uwiano sawa wa utoaji wa elimu kwa vyuo vikuu vya umma na vya binafsi ili kuepusha dhana potofu kuwa vyuo vya umma vinathaminiwa zaidi. Wadau wanasemaje?



**DOREEN TUPA (MWANAFUNZI CHUO KIKUU SAUT MWANZA)**

NAUNGA mkono hoja aliyosema Rais mstaafu wa awamu ya tatu Benjamin Mkapa juu ya serikali kuweka mazingira yenye uwiano sawa kwa vyuo vya umma na binafsi, kwa kuwa itasaidia vyuo binafsi kuonekana vina ubora pia kwa sababu mara nyingi wanafunzi wanaona vyuo vya binafsi haviwezi kutoa elimu iliyo bora ikilinganishwa na vya serikali. Lakini hilo si kweli, kwani vina uwezo wa kutoa elimu bora tena yenye kumjenga mwanafunzi katika maisha yake kiujumla. Ni vyema serikali iweke mazingira sawa hata kwenye ukarabati wa vyuo vikuu vyote badala ya kukazania vya serikali tu. Ukiangalia vyuo binafsi havina hosteli nzuri kama za vyuo vya umma, kwa hiyo hii inaleta dhana potofu kwa watu kuwa vyuo binafsi havithaminiwi. Vilevile kwenye miundombinu ya barabara ukiangalia serikali inatengeneza barabara nzuri kwenye vyuo vya umma ili kuweka mazingira bora kwa wanafunzi kufika mapema na kuwa na muda mzuri wa kujisomea, lakini vyuo binafsi serikali haijaboresha miundombinu ya barabara ili kuwasaidia wanafunzi. Hii sasa inaleta dhana potofu kwa watu kuwa vyuo binafsi havithaminiwi na serikali. Ningependa kuishauri serikali kuweka mazingira bora katika vyuo vya umma na vya binafsi kwa ajili ya kuboresha elimu nchini ili kuwasaidia wanafunzi wote na kudumisha ushirikiano kati ya vyuo binafsi na vya umma.




**BENJAMIN NKONYA (KATIBU MKUU WA CHAMA CHA WAMILIKI NA MAMENEJA WA SHULE NA VYUO BINAFSI (TAMONGSCO)**

HILI suala lina changamoto nyingi ambazo kimsingi zinahitaji kufanyiwa kazi au kutatuliwa haraka kwa manufaa ya elimu ya Tanzania, lakini vinginevyo changamoto zitazidi. Kwanza ikumbukwe kuwa wanafunzi wanaosoma katika vyuo binafsi na vya serikali ni watoto wa walipakodi. Kwa nini serikali inazuia ufadhili kwa walio kwenye vyuo binafsi? Vyuo huandaa watu kuingia katika soko la ajira (udaktari, uhandisi, uhakimu, uhasibu n.k.). Iweje mzazi alazimike kumlipia mtu ambaye atafaidisha mwajiri? Watu wote wanaoingia vyuo vikuu wana umri wa zaidi ya miaka 18 (sio watoto). Iweje mtu asiye mtoto agharamiwe na mzazi wake wakati sheria inamtambua kuwa ni mtu mzima? Uyeyuko wa sera hukatisha tamaa sana uwekezaji. Hii sera ya kugharamia wanafunzi bila kujali umiliki wa vyuo ulichochea sana ongezeko ka vyuo vikuu. Kuiondoa tena kutakatisha tamaa sana wawekezaji. Ushauri wangu ni kwamba serikali itambue kwamba vyuo vikuu binafsi vina mchango mkubwa sana katika kuongeza udahili na kupunguza mzigo wa gharama za uwekezaji kwa serikali. Serikali ijifunze kutoka Uholanzi, ambayo inagharamia elimu bila kujali mmiliki, na ubora wa elimu uko juu sana wakati gharama ya elimu iko chini sana. Hata hapa kwetu hayo yanaweza kufanyika kwa mafanikio ya hali ya juu, kwani lengo ni kuandaa wataalam wa baadaye wa taifa hili.



**AMOS KASELA (MKAZI WA JIJINI MWANZA)**

RAI ya Rais mstaafu Benjamin Mkapa aliyoitoa kwamba serikali iangalie uwezekano wa kuweka mazingira yenye uwiano sawa katika utoaji wa elimu katika vyuo vikuu hapa nchini ili kuondoa dhana kwamba vyuo vya serikali nchini vinapata upendeleo ni rai ambayo inahitaji mjadala wa kina kutoka kwa wadau wa sekta ya elimu. Kwa upande wangu napenda kutoa maoni kwamba ninakubaliana na dhana hiyo kuwa vyuo vya serikali yawezekana vinapata upendeleo fulani kutoka kwa serikali japokuwa suala hilo halipo wazi sana. Ikumbukwe kuwa mazingira ya kufundishia katika vyuo vikuu hapa nchini yanaratibiwa na kuangaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu (Tanzania Commission for Universities (TCU). Tume hii kazi yake kubwa ni kuchunguza na kuthibitisha uhalali wa utoaji wa elimu vyuoni kwa kuangalia hasa viwango vilivyokubaliwa. Taasisi nyingine inayohusika na uthibiti wa utoaji wa elimu katika vyuo vikuu hapa nchini ni Baraza la Uthibiti ya Vyuo vya Elimu na Ufundi yaani (National Accreditation Council of Technical Education (NACTE). Baraza hili linahusika na kutoa ithibati na kusimamia utoaji wa elimu katika vyuo vya kati hasa katika ngazi ya astashahada na stashahada. Hapa tunaona waziwazi kuwa uwepo wa TCU na NACTE ni jitihada za makusudi za kuleta uwiano ulio sawa kati ya vyuo vikuu Tanzania, vile vinavyosimamiwa na serikali kwa asilimia 100 na vya binafsi kama taasisi za dini ambavyo serikali ina hisa katika uendeshaji wake. Hivyo basi uwiano sawa katika utoaji elimu katika vyuo vikuu kwa sehemu kubwa upo japo marekebisho bado yanahitajika kuondoa tofauti ndogondogo zilizopo. Nigusie kidogo tu kwamba mwanafunzi anayedahiliwa chuo cha serikali anapata mkopo wa masomo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.



**DOMONICA BALAMA (MWALIMU GENESIS SCHOOL DAR ES SALAAM)**

KWANZA kabisa naamini serikali inathamini mchango mkubwa wa vyuo binafsi na ina mchango wake mkubwa tu katika uendeshaji vyuo hivyo. Sasa kutoa uwiano sawa si jambo rahisi. Ikumbukwe hivyo vinatengeneza faida (Business oriented) ukilinganisha na vyuo umma, ambavyo havitengenezi faida (non profitable). La msingi ni kuhitaji marekebisho na si uwiano sawa. Ni muhimu kutambua kuwa uwiano ulio sawa kati ya vyuo vikuu Tanzania huwa unathibitiwa katika udahili. Serikali huwa mara nyingine inasitisha utoaji ruzuku kwa ajili ya kusaidia uendeshaji na uendelezaji wa taasisi zake. Vilevile wakati mwingine huwa inasitisha utoaji ruzuku na kuhimiza taasisi kujiendesha zenyewe kupitia mapato ya ndani. Ninaamini kwamba katika suala la kudhibiti ubora wa elimu kwenye vyuo hakuna upendeleo, na kama unakumbuka, miaka ya hivi karibuni baadhi ya vyuo vikuu vilivyobainika kutokuwa na ubora na hadhi ya kutoa elimu vilifutwa na vingine kufungiwa. Kwa hiyo niseme tu kwamba Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa ametoa maoni na ushauri wake huo kwamba serikali iweke mazingira yenye uwiano sawa wa utoaji wa elimu kwa vyuo vikuu vya umma na vya binafsi ili kuepusha dhana potofu kuwa vyuo vya umma vinathaminiwa zaidi. Lakini mimi kwa maoni yangu ni kwamba uwiano upo ila hiyo ni dhana tu.



**JOHN PIUS (MHITIMU WA CHUO KIKUU HURIA, DAR ES SALAAM)**

JAMBO hili linahitaji mjadala mpana kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi, kwa sababu siyo mara ya kwanza kumsikia akizungumzia changamoto za elimu nchini. Kama utakumbuka, amewahi kuzungumzia jambo hili wakati wa shughuli za kumuingiza kazini mkuu mpya wa Chuo Kikuu cha Dodoma, na kwenye hotuba yake alisema anashangazwa na matokeo mabaya yanayoshuhudiwa kila mwaka kutoka katika shule za serikali ikilinganishwa na shule binafsi. Akashauri kwamba umefika wakati sasa mfumo wa elimu kutazamwa upya ikiwa ni pamoja na kuangalia changamoto zinazoikabili sekta hiyo ili kubaini wapi kuna dosari katika kuboresha elimu inayotolewa kwa shule za serikali. Alikiri kwamba hana uhakika kuwa elimu ya Tanzania iko chini zaidi katika nchi wanachama za jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini hata hivyo, akashauri kuwapo kwa mjadala shirikishi wa kitaifa bila kujali kada ya raia. Sasa amekuja na hili la kuiomba serikali kuweka mazingira yenye uwiano sawa wa utoaji wa elimu kwa vyuo vikuu vya umma na vya binafsi ili kuepusha dhana potofu kuwa vyuo vya umma vinathaminiwa zaidi. Binafsi sioni tatizo kama kweli kuna kasoro, ambazo zinaweza kufanyiwa kazi, kwa lengo la kutafuta uwiano. Hata hivyo sijafuatilia na kubaini uwepo wa dhana kwamba vyuo vikuu vya umma vinathaminiwa kuliko vya binafsi.



# Waomba kuboreshewa miundombinu ya barabara

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WADAU wa usafirishaji mkoani Songwe wameiomba serikali kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha miundombinu ya barabara ikiwamo kuboresha alama za barabarani ili kuhakikisha usalama wa abiria na wasafirishaji.

Ombi hilo lilitolewa juzi na wadau wa usafirishaji mkoani humo wakati wakizungumza na Nipashe kuhusu uwapo wa alama za barabarani kunavyoweza kupunguza wimbi la ajali.

Walisema ili kuepuka ajali za mara kwa mara barabarani, miongoni mwa njia za kuzipunguza ni kuongeza alama za barabara kwenye maeneo hatarishi na sehemu za makazi ya watu.

Mmoja wa wadau, Leopard Mwanyika, alisema serikali imejitahidi kutoa elimu ya kuepukana na ajali kwa madereva na abiria, suala la kuweka alama za barabarani katika barabara ya Mbeya- Tunduma bado linahitaji.

Pia aliomba kuimarisha doria nyakati za usiku ili kuwahakikishia abiria usalama wao baada ya mabasi kuruhusiwa kusafiri saa 24.

"Uamuzi wa serikali kuruhusu mabasi kusafiri saa 24 lazima uende sambamba na uboreshwaji wa miundombinu ya barabara ambazo kwa sasa matumizi yake yataongezeka maradufu ikilinganishwa na hapo awali," alisema Mwanyika.

Alishauri pia wamiliki wa vyombo vya moto kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vyao kabla ya kusafirisha abiria ili kuepuka ajali na madereva kutii sheria na alama za barabarani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, alisema serikali inatambua changamoto za alama za barabarani na kuwa miongoni mwa sababu zinazochochea ajali.

Alisema serikali inaendelea kutatua changamoto hiyo na kwa kiasi kikubwa imefanikiwa kuweka alama za barabarani ikiwamo sehemu za vivuko na maeneo korofi.

**Uamuzi wa serikali kuruhusu mabasi kusafiri saa 24 lazima uende sambamba na uboreshwaji wa miundombinu ya barabara ambazo kwa sasa matumizi yake yataongezeka maradufu ikilinganishwa na hapo awali.**

# Unicef yatoa mil. 200/- mafunzo elimu ya awali

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

ZAIDI ya Sh. milioni 200 zimetolewa na Shirika la Kimataifa la Kuhudumia Watoto Duniani (Unicef) kwa ajili ya kuendesha mafunzo kwa walimu 400 wanaofundisha elimu ya awali kwa watoto wanaosoma shule za serikali mkoani Songwe.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, David Kafulila, wakati wa kufungua mafunzo ya siku tano kwa walimu kutoka halmashauri za Ileje, Momba na Tunduma, ambayo yalifanyika kwenye Chuo cha Ualimu Mpuguso, kilichopo katika Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya.

Kafulila alisema Unicef imetoa kiasi hicho kwa lengo la kukabiliana na wimbi la wanafunzi wanaomaliza darasa la saba wakiwa hawajui kuhesabu, kusoma wala kuandika.

Alisema mpango huo utasaidia kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa walimu kuhakikisha wanafunzi wanajua kusoma, kuandika na kuhesabu kuanzia elimu ya awali.

**Nimejifunza mbinu mbalimbali za kuwafundisha watoto wenye uelewa mdogo darasani, kiu yangu ni kuhakikisha watoto ninaowafundisha wote wanajua kusoma, kuhesabu na kuandika.**

"Mkoa wa Songwe ni miongoni mwa mikoa ambayo bado haifanyi vizuri kitaaluma kwa sababu hiyo Unicef wamewekeza kwenye elimu kwa kuboresha mazingira kuanzia miundombinu, vifaa vya walimu na wanafunzi na mradi huu wa sasa utajikita kutoa elimu kwa walimu namna ya kukabiliana na wanafunzi wasiojua kusoma wala kuandika," alisema Kafulila.

Alisema fedha zilizotolewa na Unicef zitakuwa kichocheo katika kuhakikisha mikoa ya Nyanda za Juu Kusini zinafanya vizuri kielimu kwa kutengeneza vizuri misingi ya awali ambayo inawaandaa watoto kujua Kusoma, Kuhesabu na Kuandika (KKK).

Ofisa Elimu Mkoa wa Songwe, Juma Kaponda, alisema mpango huo utatekelezwa katika awamu mbili na kila shule itatoa mwalimu mmoja kwa ajili ya kupata mafunzo.

Alisema awamu ya kwanza imehusisha walimu 205, huku akisisitiza kuwa endapo walimu wote katika shule moja watahitajika lazima wapate semina hiyo.

Baadhi ya washiriki walieleza matarajio yao baada ya kupata mafunzo hayo na kuahidi kuchapa kazi kwa bidii watakaporejea kwenye vituo vyao vya kazi.

Miongoni mwa walimu hao, Getrude Mwansele, alisema ni mara yake ya pili kushiriki mafunzo hayo na ameyafurahia kwa sababu yamekuwa yakimjengea uwezo wa namna ya kuwafundisha watoto.

"Nimejifunza mbinu mbalimbali za kuwafundisha watoto wenye uelewa mdogo darasani, kiu yangu ni kuhakikisha watoto ninaowafundisha wote wanajua kusoma, kuhesabu na kuandika," alisema Getrude.

Mafunzo hayo yanaendeshwa kwenye mikoa ya Mbeya, Njombe na Songwe, yanalenga kujenga msingi mzuri kuanzia ngazi ya awali.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (katikati), akipewa maelekezo ya mchoro wa ramani ya mradi wa jengo la ghorofa sita la wodi ya wazazi ambalo litagharimu kiasi cha Sh. bilioni saba katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waziri afurahia upanuzi jengo la mama/mtoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ameeleza kuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa mradi wa upanuzi wa jengo la mama na mtoto linalojengwa katika Hospitali ya Rufani ya Mbeya (MZRH).

Akizungumza hivi karibuni mkoani Mbeya, Waziri Ummy alisema ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa mradi huo na ukikamilika utakuwa ni msaada kwa wajawazito na watoto wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa ghorofa sita mpaka kukamilika kwake na imedhamiria kuboresha na kuiwezesha sekta ya afya nchini.

Vile vile, alisema kukamilika kwa jengo hilo la kisasa kutaongeza huduma mbalimbali zinazohitajika kwa wajawazito na watoto wachanga ikiwamo za upasuaji ndani ya muda mfupi.

"Mradi huu unatarajia kugharimu kiasi cha Sh. bilioni saba, kwa sasa serikali imetoa Sh. bilioni nne kwa mfumo wa 'force account' kwa ajili ya kuanza ujenzi wa ghorofa sita tunatarajia jengo hilo kukamilika ndani ya miezi 18, tumewaomba kuongeza kasi ikiwezekana isifike miezi hiyo," alisema Waziri Ummy.

Alisema baada ya kukamilika kwa jengo hilo, kutasaidia kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga kwa kuwa miundombinu ya utoaji huduma itakuwa bora na kisasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya, Dk. Goodlove Mbwanji, aliishukuru serikali kwa kuwajali wajawazito na kuongeza kuwa kukamilika kwa ujenzi huo kutakuwa neema kwa wanaohitaji huduma ya uzazi kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema jengo hilo litakuwa na jumla ya vitanda 200, vyumba vya uangalizi maalum (ICU) na vyumba vinne kwa ajili ya uangalizi maalum kwa watoto wachanga (NICU) na wataalamu wa kutosha.





# RPC Muroto awaonya walinzi binafsi uhalifu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WALINZI wa kampuni binafsi nchini wametakiwa kuacha kushiriki vitendo vya kihalifu na kuepuka kula vyakula ovyo kutoka kwa watu wasiowajua wakiwa kwenye maeneo ya kazi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, alisema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo kwa walinzi wa kampuni binafsi za ulinzi mkoani hapa.

"Kwanza askari anatakiwa kujenga uaminifu katika maeneo ya kazi, kuepuka tamaa na vitendo vya kihalifu wakati wowote na unapokuwa lindoni epuka kupokea vyakula ovyo ovyo kwa sababu hujui adui ni yupi," alisema.

**Askari anapokuwa kwenye lindo, anatakiwa kuhakikisha anajilinda na silaha aliyo nayo, mali pamoja na maisha ya anaowalinda.**

Kamanda huyo alisema mafunzo hayo yatawasaidia askari hao kujua mbinu zaidi za kiulinzi pamoja na kujifunza ulinzi shirikishi katika jamii.

Alisema askari anapokuwa kwenye lindo, anatakiwa kuhakikisha anajilinda na silaha aliyo nayo, mali pamoja na maisha ya anaowalinda.

Pia alisema askari anatakiwa kujua kazi anayoifanya na eneo analolinda pamoja na mali zilizopo na asikubali kuingia mikataba ya kulinda mali zingine nje ya kazi ya kampuni iliyomwajiri.

Aidha, aliwaomba wamiliki wa kampuni binafsi kuhakikisha wanawapatia zawadi kama motisha walinzi wanaofanya kazi vizuri katika maeneo yao.

Mwenyekiti wa Sekta Binafsi ya Ulinzi (TSIA) Kanda ya Kati, Lukanus Kayombo, alisema mafunzo hayo ni utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Siro, kwenye kikao cha pamoja kilichofanyika Mei 21, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Alisema katika kikao hicho walikubaliana kuwa walinzi wote wa kampuni binafsi wapatiwe mafunzo maalumu bila kujali kama walipitia majeshi mengine kabla ya kuajiriwa.

Kayombo alibainisha kuwa kwa wale waliopitia mafunzo ya kijeshi katika vyombo vya ulinzi vya majeshi mengine, watapata mafunzo hayo kwa muda wa mwezi mmoja ila kwa wale ambao hajawahi kupata mafunzo hayo watajifunza kwa miezi mitatu.

Kayombo alisema katika awamu hiyo ya kwanza, askari 316 kutoka kampuni 24 kati ya 60 mkoa wa Dodoma watapata mafunzo.

Hata hivyo, alisema lengo kuu la askari hao kupatiwa mafunzo ni kuongeza weledi kazini pamoja na kupatiwa mbinu za kazi.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, SACP Gilles Muroto, akizungumza wakati wa kufungua mafunzo ya kampuni za sekta binafsi za ulinzi mkoani humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wenye ulemavu watengewa fungu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetenga bajeti kwa ajili ya mfuko wa watu wenye ulemavu ili kuwasaidia kujikwamua kiuchumi katika shughuli mbalimbali wanazofanya.

Aidha, serikali inatarajia kufanya mapitio ya Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010, ili kuendana na haki sawa za msingi kwa watu wenye ulemavu.

Hayo yalisemwa na mwakilishi kutoka ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Kazi na Ajira kitengo cha walemavu, Herieth Mpili, katika kongamano la lugha ya alama lililofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dodoma.

Mpili alisema mfuko huo umetengwa kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 ili kuwawezesha kiuchumi watu wenye ulemavu kulingana na shughuli za maendeleo wanazofanya ikiwamo kuwahamasisha kuchangamkia fursa za maendeleo.

"Serikali inawajali sana watu wa kundi hilo ndiyo maana unaona iko mstari wa mbele kuhakikisha inawashirikisha katika shughuli za ujenzi wa taifa watu wa kundi hilo," alisema Mpili.

Alisema kutokana na hilo wataendelea kusimamia kundi hilo kuhakikisha linapata huduma ya mikopo ya asilimia mbili inayotolewa katika halmashauri mbalimbali nchini.

Mpili alisema watu wenye ulemavu wanapaswa kuchangamkia fursa za mikopo zinazotolewa katika maeneo mbalimbali nchini kwa sababu ni haki yao kuipata.

Alifafanua kuwa watu wa kundi hilo wana haki za msingi kama walivyo watu wengine, hivyo wanachotakiwa ni kujitokeza kwa wingi katika fursa wanazoona zinawafaa kujiinua kiuchumi.

Pia alisema serikali inatarajia kuunda baraza jipya la watu wenye ulemavu kwa ajili ya kuishauri serikali katika masuala mbalimbali yanayohusu walemavu.

Alisema baraza hilo ni chombo ambacho kitawasaidia watu wa aina hiyo kuwasilisha hoja zao za msingi kupitia viongozi ambao watachaguliwa kuunda baraza hilo.

# Sido yatoa somo kwa wajasiriamali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido) mkoani Dodoma limewataka wajasiriamali kutunza rasilimali walizo nazo na kuziboresha ili kutoa ushindani katika soko la biashara.

Meneja wa Sido Mkoa wa Dodoma, Sempeho Manongi, alisema hayo juzi wakati akielezea ushindani wa biashara uliopo sasa hasa kipindi hiki nchi iko katika soko la pamoja na nchi za Afrika Mashariki.

Manongi alisema wajasiriamali wanapaswa kuboresha bidhaa walizo nazo kulingana na mafunzo wanayopewa na Sido ili kupiga hatua na kuingia katika ushindani wa masoko makubwa ya biashara.

Alisema mjasiriamali anapaswa kuzingatia mafunzo anayopewa ikiwamo kuyafanyia kazi ili kusonga mbele katika biashara anayofanya.

"Naomba wajasiriamali mzingatie mafunzo mnayopewa na Sido. Tunahitaji kuona mnaleta ushindani katika maonyesho ya kitaifa na kimataifa," alisema Manongi.

Alisema kinachotakiwa kwa sasa ni kuona kila vikundi vinashiriki katika mafunzo yanayotolewa na Sido ili kujiongezea ujuzi katika bidhaa wanazotengeneza jambo ambalo litawasaidia kuongeza thamani ya kile wanachofanya.

"Sido imekuwa mstari wa mbele kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuongeza kuwa vikundi vinapaswa kujitokeza kushiriki ili kuboresha zaidi kazi wanazozifanya," alisema Manongi.

Alisema bila kufanya hivyo hawawezi kubadilisha kiwango cha uzalishaji ikiwamo kushindwa kujiongezea kipato kutokana na kwamba jamii inahitaji na kufuata bidhaa iliyobora na yenye viwango vya juu.

Meneja huyo pia alisisitiza wajasiriamali kuongeza ufanisi katika eneo wanalohitaji kufanyia kazi ili kuwasaidia kuimarisha kile wanachohitaji kwenye biashara zao.

Hata hivyo, alisema kuwa lengo la Sido ni kuona wajasiriamali wanasonga mbele na kuingia katika maonyesho makubwa ya biashara ya kimataifa.

**Sido imekuwa mstari wa mbele kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuongeza kuwa vikundi vinapaswa kujitokeza kushiriki ili kuboresha zaidi kazi wanazozifanya.**

# SMZ yajiandaa kusafirisha mahujaji

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imeanza mazungumzo yatakayowezesha Zanzibar kujitegemea katika safari za ibada ya hija huko Makka, Saud Arabia.

Waziri wa Katiba na Sheria, Juma Khamis Maalim, alisema hayo wakati akiwaaga mahujaji katika msikiti wa Noor Mohamed, wakiwa katika maandalizi ya mwisho ya safari ya Ibada ya Hija.

Alisema Zanzibar inataka kuandaa safari za mahujaji kwenda Makka yenyewe kwa ajili ya kuepuka mivutano na migogoro inayojitokeza mara kwa mara kwa mahujaji.

Alisema katika nyakati tofauti kumejitokeza hitilafu za maandalizi ya safari hizo na kuwafanya mahujaji kutoka Zanzibar kushindwa kutekeleza ibada zao kikamilifu.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo katika mchakato ambao utatuwezesha kufanya maandalizi ya safari za ibada ya hija bila ya kuwategemea watu wengine au taasisi," alisema.

Pia, Maalim aliwatakia mahujaji hao kila la kheri katika safari yao ya ibada ya hija na kuwataka kufuata maelekezo ya viongozi wa kundi la msafara wa mahujaji.

Naye Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Wakfu na Mali ya Amana inayoshughulikia safari za mahujaji Makka, Abdalla Talib, alisema tayari maandalizi ya kuanzishwa kwa mfuko wa hija yamekamilika baada ya kuzinduliwa na Rais wa Zanzibar.

Alisema kuwapo kwa mfuko wa hija kwa kiasi kikubwa kutasaidia kuratibu safari na maandalizi kwa mahujaji kwa mafanikio makubwa.

"Nataka niwajulishe mahujaji wote kwamba tayari mfuko wa hija umezinduliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ambao miongoni mwa majukumu yake ni kuratibu safari za hija," alisema.

Jumla ya mahujaji 170 wanatarajiwa kuondoka nchini wiki ijayo kuelekea Makka kwa ajili ya ibada ya hija ambayo ni miongoni mwa nguzo tano za dini ya Kiislamu kwa mtu mwenye uwezo.

**Nataka niwajulishe mahujaji wote kwamba tayari mfuko wa hija umezinduliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ambao miongoni mwa majukumu yake ni kuratibu safari za hija.**

# Tamwa yataka upelelezi haraka utumikishaji kingono

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

KUFUATIA kukamatwa kwa mfanyabiashara Salome John, anayedaiwa kuwatumikisha kingono wasichana sita huko Kizimkazi Unguja, Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), Ofisi ya Zanzibar imelitaka Jeshi la Polisi kufanya upelelezi wake haraka iwezekanavyo ili sheria ichukue mkondo wake na pia kupunguza vitendo hivyo viovu vinavyowadhalilisha wanawake na watoto wa kike.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu kadhia hiyo, Mkurugenzi Tamwa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema kuwa kitendo cha kuwatumikisha wasichana kingono ni uvunjifu wa Sheria ya Adhabu namba 6 ya mwaka 2018.

**Sehemu ya 13 ya sheria hiyo ni kuhusu makosa ya kimaadili; kifungu namba 117 kinachoelezea 'kuwezesha ukahaba' na kifungu na 118 kuhusu kuwezesha ngono haramu.**

Alieleza kuwa kuna ongezeko la wasichana wanaoingia nchini na kufanya kazi kinyume cha matarajio yao ya awali ikiwamo kufanyishwa kazi kwenye saluni za kuchua na kutumikishwa kingono.

"Sehemu ya 13 ya sheria hiyo ni kuhusu makosa ya kimaadili; kifungu namba 117 kinachoelezea 'kuwezesha ukahaba' na kifungu na 118 kuhusu kuwezesha ngono haramu," alisema.

Alieleza kuwa sheria hiyo inasema kuwa mtu huyo atakuwa anatenda kosa la uwezeshaji ukahaba na atapewa adhabu ya kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka 10 na atatozwa faini isiyopungua Sh. milioni tano, lakini isiyozidi Sh. milioni 10 au adhabu zote.

Vile vile, alisema sheria hiyo ya adhabu imeeleza vizuri kuhusu makosa dhidi ya maadili pamoja na adhabu zake, hivyo ana imani kuwa Jeshi la Polisi litafanya kazi yake vizuri ili kumtia hatiani mtuhumiwa hasa kwa sababu waliofanyiwa vitendo hivyo (wasichana sita), wako tayari kutoa ushahidi.

Alisema Tamwa inaamini kuwa hatua mahususi ikichukuliwa dhidi ya mtuhumiwa siyo tu itaweza kumsimamisha yeye binafsi, lakini pia wengine wanaofanyabiashara kama hiyo na wale wote wanaotaka kujaribu.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara ya DCB, Godfrey Ndalahwa (kulia), akikabidhi zawadi ya seti ya television kwa mmoja wa wafanyakazi wa benki hiyo, Elizabeth Ntulu, baada ya kuibuka mmoja wa washindi wa kampeni ya akaunti ya muda maalumu ya 'DCB Lamba Kwanza' jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

# 'Wapewe elimu udhalilishaji kijinsia'

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Kusini Unguja limesema elimu ya udhalilishaji wa kijinsia inahitajika ili wanafunzi kuepuka na ukatili wa kijinsia ambao hujitokeza wakati wanapokuwa katika masomo.

Hayo yalisemwa na kiongozi wa Dawati la Polisi Mkoa wa Kusini Unguja, Ali Mohamed Othman, wakati alipozungumza na wanafunzi wa Shule ya Kiboke, Wilaya ya Kati Unguja, katika ziara ya kutoa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia.

Alisema wanafunzi wengi bado hawafahamu aina ya ukatili wa kijinsia na njia za kukabiliana na matukio hayo wakati yanapojitokeza.

"Ukatili wa kijinsia sio kubakwa tu au kulawitiwa...hata adhabu za kupindukia zinazotolewa na walimu zinatakiwa kukemewa vikali," alisema.

Vile vile, aliwataka wazazi nao kufuatilia nyendo za watoto wao wakati wote wanapokuwa shule na wanaporudi ili kuhakikisha wapo salama na aina zote za udhalilishaji wa kijinsia.

"Hatuwezi kufanikiwa katika mapambano ya udhalilishaji wa kijinsia kama wazazi tutakuwa mbali na watoto wetu katika kuangalia harakati zao za kila siku za maisha," alisema.

Mkuu wa dawati hilo kutoka Jeshi la Polisi alisema tayari wameanza kufanya mawasiliano na wazazi wa wanafunzi waliofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

"Tutawaita wazazi wa wanafunzi waliofanyiwa ukatili wa kijinsia ili kujuwa nani wahusika wa matukio hayo na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria," alisema.

Mwalimu wa Shule ya Kiboje, Ali Iddi, alisema wamefurahishwa na uamuzi wa Jeshi la Polisi kutoa elimu ya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanafunzi wa shule ambayo imeibua wanafunzi wanaofanyiwa ukatili huo.

"Elimu ya udhalilishaji wa kijinsia imeibua mambo makubwa ya kuwapo kwa wanafunzi wanaofanyiwa ukatili wa kijinsia ikiwamo watoto wa kiume kulawitiwa," alisema.

# Mawakala utalii wa Korea kusini kuja Tanzania

**Na Beatrice Philemon**

JUMLA ya mawakala wa utalii 20 kutoka Korea Kusini wanatarajia kutembelea Tanzania mwezi Oktoba mwaka huu, ili kuona vivutio vya utalii, pia kushiriki mafunzo ya wakala wa utalii.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji mstaafu Thomas Mihayo na kufafanua:

"Tukiwa Korea Kusini ujumbe kutoka Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ulifanikiwa kukutana na wadau mbalimbali wakuu wa utalii wa nchi hiyo akiwamo Byeong -Sam Kim, Katibu Mkuu wa Chama cha Mawakala wa Utalii wa Korea ya Kusini."

**Kim alionyesha utayari wake wa kushirikiana na TTB na katika kufanikisha suala hilo, na aliahidi ataongoza ujumbe wa mawakala wa utalii 20 kutoka Korea Kusini watakaokuja nchinii.**

Katika kikao hicho TTB na KTA waliweza kufanya mazungumzo yaliyolenga kuhamasisha suala la ushirikiano baina ya mawakala wa utalii wa Tanzania na Korea ya Kusini.

Alisema Kim alionyesha utayari wake wa kushirikiana na TTB na katika kufanikisha suala hilo, na aliahidi ataongoza ujumbe wa mawakala wa utalii 20 kutoka Korea Kusini watakaokuja nchinii.

Vile vile wamefanikiwa kukutana na wadau wa sekta ya utalii nchini humo na mikutano hiyo iliandaliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania nchini humo.

Kim alieleza kwamba kwa mwaka 2018 idadi ya watalii milioni 26 kutoka Korea Kusini walitembelea nchi mbalimbali duniani.

Aidha, alishauri ili TTB iweze kufanikiwa katika mikakati yake ya kukamata soko la Korea ya Kusini, ni muhimu kuwaunganisha wafanyabiashara ya utalii wa Tanzania na wa Korea ya Kusini.

Wakati huo huo, ujumbe kutoka TTB pamoja na maofisa kutoka ubalozi wa Tanzania nchini Korea ya Kusini waliweza kukutana na Rahel Gebre, Meneja Mkuu wa Shirika la Ndege la Ethiopia nchini Korea ya Kusini, mkutano huo ulilenga kuweka mikakati ya ushirikiano kati ya TTB na ofisi ya Ethiopian Airlines nchini Korea Kusini katika kutangaza utalii wa Tanzania nchini Korea Kusini, hasa katika kurahisisha suala la usafiri wa anga kwa watalii kutoka nchi hiyo.

Pia ujumbe kutoka TTB ulikutana na Kampuni ya Uwakala wa Utalii ya Shoestring travels ambayo imebobea katika utalii wa upandaji mlima duniani.

Kwa mujibu wa Jaji Mihayo, Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Youngbok Jang, alisema kampuni yake ipo tayari kushirikiana na TTB katika kutangaza Mlima Kilimanjaro na kuhamasisha watalii kutoka Korea kupanda mlima huo pamoja na kutangaza milima mingine ya Tanzania.



Miti iliyokatwa katika safu ya Milima ya Livingstone mkoani Ruvuma ambapo inaonyesha namna gani athari za shughuli za kibinadamu zinavyoharibu ekolojia ya Ziwa Nyasa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# NEMC yawaonya waharibifu wa mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** MBINGA

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limewataka wananchi katika Wilaya ya Mbinga na Nyasa kuacha mara moja tabia ya kukata miti ovyo kwenye safu ya milima ya Livingstone hali inayochangia uharibifu wa ikolojia ya Ziwa Nyasa.

Akizungumza katika ziara yake ya kutembelea Kanda ya Kusini ya Baraza hilo mkoani Ruvuma, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema ziara yake imelenga kujionea changamoto za kimazingira katika wilaya za Mbinga na Nyasa ambazo zinapelekea ekolojia ya Ziwa Nyasa kuharibika.

"Ukataji miti unachangia ardhi kuwa tupu na kupelekea udongo kusombwa na maji kipindi cha mvua ambapo udongo wote unakwenda ziwani hali itakayosababisha miaka michache ijayo ziwa kujaa matope na hata kupotea," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema elimu ni muhimu kutolewa kwa wananchi juu ya athari za kukata miti katika maeneo ya milimani ambapo ndio kuna vyanzo vya maji hali inayosababisha mmomonyoko wa udongo kipindi cha mvua na kupelekea udongo kujaa katika ziwa.

"Athari za kukata miti inapelekea ardhi kuwa na mmomonyoko mvua zinaponyesha rutuba ya udongo inapote hata kusababisha uzalishaji katika sekta ya kilimo kupungua, hivyo ili kuepukana na athari kama hizi tunawajibika kutunza mazingira," alisema.

Alitolewa mfano Mto Luhuhu ambapo maji yake bado yamekuwa na rangi ya udongo hata kipindi hiki cha kiangazi hali inayodhihirisha shughuli za kibinadamu zimeathiri vyanzo vya maji katika mto huo na kufanya maji yanayoingia Ziwa Nyasa kuwa na matope hali inayosababisha ziwa kujaa matope taratibu.

"Hali hii ikiendelea tunaweza kulipoteza Ziwa Nyasa hivyo juhudi za makusudi katika utunzaji wa vyanzo vya maji unahitaji na jukumu hili ni la kila mwananchi kuhakikisha shughuli anayofanya haisababishi mazingira kuathirika," alisema.

Aidha, Dk. Gwamaka alisema baraza linawataka wananchi kutunza mazingira ikiwamo safu ya milima ya Livingstone ambayo ni sehemu ya vyanzo vya maji vinavyolifanya Ziwa Nyasa kuendelea kuwapo hivyo ni muhimu kulindwa na kila mwananchi awe mlinzi kwa mwenzie katika suala la utunzaji wa mazingira.

"Nimepita katika baadhi ya vijiji ndani ya Wilaya ya Mbiga na kukuta mapori mengi yamekatwa miti, hivyo niwatake viongozi wa vijiji maofisa mazingira na wadau wengine wa mazingira kuhakikisha wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo tengefu ili yaendelee kulindwa," alisema Dk. Gwamaka.

# Madiwani waazimia asilimia 25 kwa mkaa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, wameazimia kutenga asilimia 25 wanayokusanya kutoka vijiji vya mradi wa mkaa endelevu kila mwaka na kuzitoa ili kuanzisha suala la usimamizi shirikishi wa misitu (USM) katika vijiji vyao.

Madiwani hao walisema hayo jana wakati wakikamilisha kikao cha mrejesho wa shughuli za mradi wa kuleta mageuzi katika sekta ya mkaa Tanzania (TTCS) maarufu kama mkaa endelevu, ambapo walisema vijiji vyote vya halmashauri hiyo vitambue na kuainisha maeneo yao ya misitu ili vifanyiwe mpango wa usimamizi huku waheshimiwa madiwani wakisaidia kusimamia hilo katika kata zao.

Walisema wataalamu wao wa misitu katika ngazi zote ni vema wakashirikiana katika mikutano ya vijiji, huku serikali za vijiji zikipewa mafunzo na kuelimishwa kutokuwa na utaratibu wa kubadilisha maeneo ya misitu kuwa mashamba bila utaratibu. Aidha, walisema halmashauri ya wilaya hiyo iweke bajeti ya kutengeneza mpango wa matumizi bora ya ardhi katika wilaya na mpango huo uanze angalau kwa vijiji vitano kwa mwaka.

Hata hivyo walimtaka Mratibu wa Mradi wa TTCS wilayani humo ahakikishe taarifa zinafika kwenye vikao vyao vya robo mwaka hususan taarifa zinazohusu uendelevu wa matumizi wa maliasili kwenye vijiji vya mradi na vijiji vingine ili viwe na mwenendo mzima wa vijiji kama sheria na kanuni zinavyotaka.

Hivyo walimtaka Mratibu wa Mradi wa TTCS Mwanasheria na wataalamu wa MJUMITA wamalizie rasimu kwa kupitia kwenye vijiji husika ili wapate maoni na wahakikishe taarifa hizo katika vikao vya robo mwaka zinapatikana.

ITV
JARIDA LA WANAWAKE: SAA 1:00 USIKU
LEO BLANDINA SEMBU ATAKUWA NA DOREENA MNUNGULIMSHONAJI WA KAVA ZA HOSPITALINI NA MASHULENI AKIMILIKI KIWANDA KIKUBWA CHA USHONAJI.

## Congo yathibitisha ebola mji wa Goma

**GOMA, DRC**

WIZARA ya Afya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imethibitisha mlipuko wa ebola kwenye mji wa Goma, ikiwa ni mara ya kwanza kwa maradhi hayo kuufikia mji huo wenye zaidi ya wakazi milioni moja tangu yalipozuka takribani mwaka mmoja uliopita.

Kwa muda mrefu maofisa wa afya wamekuwa na wasiwasi kuwa maradhi hayo yangeingia mji wa Goma ambao unapakana na Rwanda.

Wizara ya afya imesema mwanaume mmoja ambaye alifika kwenye hospitali ya mkoa Jumapili alihamishiwa haraka kwenye kituo cha matibabu ya ugonjwa huo.

Mamlaka za Congo zimesema zimewafuatilia abiria wote waliosafiri kwenye basi lililomsafirisha mgonjwa huyo kwenda Goma akitokea mji wa Butembo ambao ni moja ya miji iliyoathiriwa vibaya na maradhi ya ebola.

Virusi vya ebola vimewaua zaidi ya watu 1,600 nchini Congo na wengine wawili katika mpaka wa nchi hiyo na Uganda.

**DW**

## Watu wanane wafariki baada ya ghorofa kuporomoka India

**NEW DELHI, India**

MAOFISA nchini India wamesema watu wanane wamefariki dunia baada ya jengo la ghorofa kuporomoka kutokana na mvua kubwa kunyesha katika eneo la milimani kaskazini ya India.

Waokoaji bado wanaendelea kuwatafuta manusura wakiwamo wanajeshi kadhaa ambao hawajulikani waliko tangu tukio hilo lilipotokea Jumapili.

Wanajeshi kadhaa ni miongoni mwa watu 31 waliokolewa tangu jengo hilo lilipoanguka kwenye mji wa Solan kiasi cha kilometa 310 Kaskazini mwa mji mkuu New Delhi.

Mafuriko yaliyosababishwa na mvua za masika yameathiri zaidi ya watu milioni 4.5 Kaskazini na Mashariki ya India na kuwaacha maelfu ya watu bila makazi.

Tangu Jumatano iliyopita watu 51 wamefariki dunia kwenye matukio yaliyosababishwa na mvua katika majimbo saba kote nchini India.

**DW**

# Trump ashutumiwa kwa ubaguzi wa rangi

**Washington, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameshutumiwa kwa ubaguzi wa rangi baada ya kuandika ujumbe kwenye twitter akiwashambulia wabunge wanawake wa chama cha Democratic.

Amedai kuwa wanawake hao "wamewasili kutoka mataifa ambayo serikali zake ni majanga matupu", kabla ya kupendekeza "warudi walikotoka".

Baada ya hapo alisema kuwa Spika Nancy Pelosi "atafurahi sana kuwashughulikia kwa haraka mipango ya safari ya bure".

Haya ni baada ya wiki moja, Pelosi kukabiliana kwa maneno na "kundi hilo", la wabunge wasio watu weupe wa mrengo wa kushoto wa chama cha Democratic.

Kati ya wabunge hao wanne, watatu, Alexandria Ocasio-Cortez, Rashida Tlaib na Ayanna Pressley walizaliwa na kulelewa Marekani, huku wanne Ilhan Omar, alihamia Marekani alipokuwa mtoto.

Ocasio Cortez alizaliwa mjini Bronx, New York, kiasi cha maili 12 kutoka hospitali ya Queens alikozaliwa Trump mwenyewe.

Katika msururu wa ujumbe kwenye twitter, Trump amewashutumu wabunge hao kwa kumshutumu yeye na Marekani kwa 'ukali'.

Aliandika: "Inavutia kuona wabunge wa Democratic 'wanaotaka maendeleo' ambao waliwasili kutoka nchi ambazo serikali zake ni majanga matupu, zilizo mbaya zaidi, zilizo na kiwango kikubwa cha rushwa, na zisizojiweza kokote duniani (iwapo ni serikali zilizokuwa zinafanya kazi) sasa wakizungumza kwa ukali wakiwaambia watu wa Marekani, taifa kubwa na lenye nguvu duniani, namna tunavyostahili kuiendesha serikali yetu.

"Kwanini wasirudi kusaidia kuyarekebisha mataifa yaliyosambaratika na yaliogubikwa kwa uhalifu wanakotoka. Halafu warudi watuonyeshe namna inavyostahili kushughulikiwa.

"Maeneo hayo yanahitaji usaidizi wenu sana, mngeondoka haraka sana. Nina hakika Nancy Pelosi atafurahi sana kuwashughulikia mipango ya safari ya bure!"

***BBC***



Rashida Tlaib (katikati), akiwa na Alexandria Ocasio-Cortez (kushoto) na Ayanna Pressley (kulia). **PICHA: BBC**

## Mchungaji akamatwa 'kumkashfu' Museveni

**KAMPALA, Uganda**

MCHUNGAJI Joseph Kabuleta, amekamatwa kwa tuhuma za kumkashfu Rais wa Uganda, Yoweri Museveni.

Kabuleta, alikamatwa Ijumaa jioni mjini Kampala na maofisa wa usalama ambao hawakuwa na sare rasmi.

Maofisa hao, pia hawakuwa na gari rasmi la kazi na wakati wa kumkamata mchungaji huyo hawakuona sababu yoyote ya kuchukua hatua hiyo.

Kabla ya kukamatwa kwake, Kabuleta alikuwa akiendesha kampeni kali katika mitandao ya kijamii akikosoa utawala uliopo madarakani na familia ya Rais.

Katika waraka wa hivi karibuni kwa jina "Mafia Empire and the Transition", ambao ulichapishwa katika mtandao wa kijamii wa Facebook Julai 8, Kabuleta alielekeza lawama zake hususan kwa mtoto wa kiume wa Rais Museveni na mshauri wa ngazi ya juu wa operesheni maalum, Luteni Jenerali Muhoozi Kainerugaba.

Alisema mpango mzuri ni kuhakikisha Jenerali Muhoozi hamrithi baba yake kama Rais.

"Tayari Jenerali Muhoozi amekuwa akitumwa kumwakilisha baba yake kwa mikutano ya kimataifa na pia kukutana na mabalozi na viongozi wengine wa ngazi za juu na kuelezea katika mtandao wake wa kuhusu ziara hizo," sehemu ya ujumbe wa Kabuleta ulisema.

Aliongeza kuwa: "Huenda baba yake ana mpango wa kustaafu kimpango baada ya kuchakachua uchaguzi wa mwaka 2021 na kuchukua jukumu la kumshauri mtoto wake, huku akiendelea kuendesha biashara ya kampuni ya familia inayofahamika kama Uganda.

"Au pengine mageuzi yakifanyika ndani ya chama cha NRM na taifa lianze mfumo wa utawala wa kibunge ambapo chama kilicho na wabunge wengi kinachukua urais."

"Mpango wowote walionao, lakini nahisi mambo huenda yakabadilika. Himaya ya Mafia imeanza kuporomoko na Uganda itarejea mikononi mwa Waganda."

Muda mfupi baada ya Kabuleta kukamatwa msemaji wa polisi mjini Kampala, Patrick Onyango, alinukuliwa na gazeti la New Vision, hana habari kuhusu "kukamatwa kwake" na kwamba atavitaarifu vyombo vya habari akipata maelezo kamili.

Baadaye Msemaji wa Idara ya Upelelezi wa jinai, Charles Twine, alithibitisha kuwa Kabuleta amekamatwa na kwamba anazuiliwa na polisi.

"Amekamatwa na kushtakiwa kwa kukiuka sheria ya mawasiliano na kwa sasa anazuiliwa," Twine aliliambia gazeti hilo.

Hatua ya kumkamata Kabuleta imezua mjadala, huku wengi wakilaani kitendo hicho.

***BBC***

HABARI KITAIFA

# Makazi holela yaiamsha ARU

**Na Romana Mallya**

MAKAZI holela kwenye miji mbalimbali imekisababishia Chuo Kikuu Ardhi (ARU) kuongeza masomo ili wanafunzi wamalizapo waisaidie serikali kasi ya urasimishaji makazi.

Mhadhiri wa chuo hicho, Paul Kitosi, aliyasema hayo jana katika maonyesho ya vyuo vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

"Changamoto ya makazi ilipotokea tulibadili mitaala kwa kuongeza masomo ili wanafunzi wamalizapo waisaidie serikali kasi ya urasimishaji makazi," alisema.

Alisema kwa sasa kuna upangaji wa miji unaoendelea kwa kasi maeneo mbalimbali kutokana na wataalamu wanaowazalisha chuoni hapo.

"Miradi ya urasimishaji inayoendelea ni baada ya wataalamu kutoka chuoni kwetu, kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa kama Benki ya Dunia (WB), wamekuwa wakifanya utafiti na kupata matokeo yake na kushauri sera, nini kifanyike kwenye makazi holela," alisema.

Pia alisema katika maeneo ambayo hayajajengwa wamefanya utafiti kuona namna ya kuipanga miji kwa gharama ndogo.

Kuhusu utafiti ambao umefanywa chuoni hapo ili kuisaidia serikali kwenye eneo hilo, Kitosi alisema kuna unaoendelea sasa ambao wanafanya kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali kwenye miji midogo kuangalia jinsi gani inaweza kupangwa ili isiharibike kama mingine.

Aliitaja miji ambayo wanaifanyia utafiti ni Geita, Malinyi na Ifakara.

Pia kupitia wanafunzi wa chuo wanapofika mwaka wa nne hufanya utafiti wa makazi holela, ajali barabarani, ujenzi wa nyumba bei nafuu, maeneo ya wazi, usafiri wa umma na mafuriko ambao huwasaidia wanapoanza kazi.

Kitosi alitaja miji mitatu ambayo ina makazi holela Dar es Salaam, Mbeya na Arusha na ambayo makazi yake yamepangika ni Tanga na Dodoma.

"Mipango kabambe imeshatengenezwa kwenye miji hiyo. Kwa upande wa manispaa zipo ambazo zimepangwa, lakini zipo ambazo zina changamoto kubwa ya makazi holela," alieleza na kuendelea:

"Ukizungumzia maeneo kama Iringa, Morogoro, wamejitahidi kwa kiasi kikubwa kupanga yale maeneo ambayo hayajajengwa."

Alisema athari za moja kwa moja miji isipopangwa ni kusababisha foleni, mafuriko kwenye makazi ya watu mvua zinaponyesha na huduma kama afya na elimu hupatikana mbali.



Mwezeshaji wa semina ya kuwajengea uwezo wanawake kushiriki katika uongozi, Dk. Katanta Simwanza, akitoa mafunzo kwa wawezeshaji kuhusu kukuza ushiriki wa wanawake katika siasa iliyoandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo (WiLDAF) na kufadhiliwa na Shirika la UN Women. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# NAS yachangia mil. 50/- ujenzi hospitali Kilolo

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya utoaji huduma za anga viwanja vya ndege, NAS Dar Airco (NAS), imechangia Sh. milioni 50 katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa.

Mradi wa hospitali hiyo ambao upo katika hatua za mwisho kukamilika, unajumuisha pia ujenzi wa nyumba za watumishi wa hospitali hiyo kwa thamani ya Sh. bilioni 4.7.

Fedha hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, Aloyce Kwezi, alisema kampuni hiyo ilikuwa na uhuru wa kuchagua mradi wowote nchini na kuuwezesha, lakini imeona ni vyema kuchangia ukamilishwaji wa hospitali hiyo.

"Kampuni ya NAS imekuwa mstari wa mbele katika kurejesha kwa jamii. Imekuwa ikichangia miradi mbalimbali ya afya na elimu. Naomba nikiri kuwa huu ni mwanzo mzuri wa uhusiano wetu na kampuni hii," alisema Kwezi.

Meneja Mkuu wa Kampuni hiyo, Miguel Serra, alisema imeajiri watu 385 na asilimia 99 ni wazawa.

Serra alisema NAS Dar imejikita nchini kwa kufanya kazi ya kuhifadhi mizigo ya abiria katika viwanja vitatu vikubwa ambavyo ni Dar es Salaam, Kilimanjaro na Dodoma.

"Tangu tumeanza kutoa huduma Tanzania mwaka 2016, tumesaidia kwa kiwango kikubwa kuinua sekta ya anga nchini, kadiri biashara inavyozidi kukua ndivyo tunavyoendelea kuchangia huduma za kijamii," alisema.

Alisema kwa kushirikiana na Kilolo wanatarajia kutimiza wajibu wao kusaidia jitihada za serikali za kutoa huduma bora za afya.

"Kwa sasa tupo katika zaidi ya viwanja vya ndege 40 mashariki ya kati, Asia na Afrika, NAS inatoa huduma ya kuchukua na kuhifadhi mizigo kwa ndege saba ambazo ni miongoni mwa ndege bora zaidi duniani," alisema.

Alisema kwa Afrika Mashariki kampuni hiyo inafanya kazi katika viwanja vya ndege 12 katika nchi sita zilizopo ukanda huo.

# 'Mapambano rushwa yaipaisha serikali'

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema juhudi za serikali za kupambana na rushwa, kudhibiti upotevu wa mapato, matumizi ya fedha za serikali na kusimamia uwajibikaji kwa watumishi wa umma ni sababu zilizowezesha Ofisi ya Rais pamoja na ya Waziri Mkuu kuaminika zaidi.

Ameyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na viongozi wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), akiwa katika ziara yake ya kikazi mkoani Kigoma. Alisisitiza kuwa vita dhidi ya rushwa ni endelevu.

Waziri Mkuu alisema Serikali ya Awamu ya Tano imepiga hatua kubwa katika vita dhidi ya rushwa ambapo kwa Afrika Tanzania inaongoza kwa mujibu wa ripoti ya Taasisi ya Transparency International iliyotolewa hivi karibuni.

Ripoti hiyo mpya iliyotolewa Julai 11, mwaka huu, inaonyesha kwamba kwa sasa Tanzania inaongoza katika nchi 35 za Afrika baada ya kupungua kwa vitendo vya rushwa katika sekta nyingi, ambapo Ofisi ya Rais na Ofisi ya Waziri Mkuu zimeonekana kuaminika zaidi.

Kadhalika, Waziri Mkuu aliwatahadharisha watumishi wa umma kwamba serikali haitomvumilia mtumishi atakayebainika anayejihusisha na vitendo vya rushwa, na aliwataka wahakikishe kuwa wanatekeleza majukumu yao ya kuwatumikia wananchi bila ubaguzi.

Waziri Mkuu alisema serikali imejipanga vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa, hivyo aliwataka wananchi wasisite wakati wote kutoa taarifa kwa vyombo husika pale watakapobaini uwapo wa watumishi wanaojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa.

"Watumishi wa umma wanatakiwa kutambua kwamba jukumu lao kubwa ni kuwatumikia wananchi kwa kuzingatia maadili na kanuni za utumishi wa umma zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni na si vinginevyo. Serikali hii kamwe haitowaonea haya au kuwafumbia macho watumishi wa ovyo."

Kadhalika, alisema kuwa suala la kuwaondoa kazini watumishi wazembe, wasiotimiza wajibu wao ipasavyo pamoja na wale wasiozingatia maadili ya utumishi wa umma ni endelevu kwa sababu serikali inahitaji watumishi wa umma wenye heshima na nidhamu ya kazi.

Alisema suala la kuwapokea, kuwasikiliza na kuwahudumia wananchi katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma kwa wananchi zikiwamo ofisi za serikali kuanzia ngazi ya kijiji hadi taifa ni miongoni mwa vipaumbele vya serikali ya awamu ya tano, hivyo watumishi wa umma wanapaswa kuzingatia jambo hilo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA,** Viwanja Vinauzwa Kibaha Visiga, ukubwa ni mita 20 kwa 20 bei ni millioni moja tuu(1,000,000/=) unaweza kulipa kwa awamu ndani ya miezi mitatu. Huduma zote zipo. Mawasiliano: 0714 090008 au 0767 090008

**PLOT NA NYUMBA VINAUZWA**

Ploti na nyumba vinauzwa mtoni kijichi wilaya ya temeke. Ploti ni mbili kwa moja ni nzuri na kubwa saana kwa matumizi yote ya kibiashara na makazi. Mawasiliano: 0688 640101

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**
**Usimamizi wa mirathi 38/2019**

**Ombi la MOSES MWAKIBINGA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu ZENA HUSSEIN MSUYA**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA - TANZANIA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 13/6//2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

215324002

### KUPOTEA KWA PASSORT/HATI YA KUSAFIRIA



Daina Abel Mwakanyamale anatangaza kupotea kwa Passport/hati ya kusafiria yenye namba TAE 130786 ilitolewa na idara ya Uhamiajia Dar es Salaam mwaka 2019.

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi taarifa:**
**DAR/OST/RB/131475/2019**

115323202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO UKONGA MJINI**
**WILAYA YA ILALA**

**SHAURI LA MADAI YA NO. 200 YA 2019**

**ANNE PRIVER KUNDI.....................MDAI**

**DHIDI YA**

**HAPINESS JOHN MAHEMBA................MDAIWA**

**KUITWA SHAURINI**

Mdai amefungua kesi madai hapa mahakamani na shauri limepangwa kusikilizwa tarehe 18/07/2019 siku ya alhamisi saa 2:30 asubuhi.

Hivyo mdaiwa unatakiwa ufike bila ya kukosa mahakama siku hiyo na endapo hutahudhuria siku hiyo iliyopangwa na mahakama shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

115323102

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ANTHONY PAUL MAKULA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba MC 393 BRF aina ya SANLG yenye chassis namba **LBRSPJB58H9013715,** yenye engine namba **17913256.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.

Taarifa ya Polisi.
**KAH/RB/TR/566/2019.**

215323801

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 18/07/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMANNE tarehe 16/07/2019 kampuni ya **SUMMMER COMMUNICATION** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **KYELA** kuelekea **UBALUKU** kupitia UYOLE. Gari hilo lenye namba za usajili:

   **T552 DKN/ T960 CMC**

2. Gari lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu-mita 17.5
   Upana-mita 3.5
   Kimo- mita 4.7

3. Njia itakayotumika **KYELA** hadi **UBALUKU** kupitia UYOLE.Gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 oni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215323302

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**
**RM. CIVIL CASE NO: 29 OF 2017**

**ALLI CHAMANI ..........................................PLAINTIFF**
**VERSUS**
**ANITHA COSTANTINE...........................1ST DEFENDANT**
**ASHURA KAJUNA...........................2ST DEFENDANT**

**Notice to show cause why execution should not issue**
**(O. XXI, r. 20(1) of the Civil Procedure Code)**

**To. ANITHA COSTANTINE**
Whereas the* Applicant has made application to this Court for the Judgment debtor to be committed to prison in the above suit, this is to give you notice that you are to appear before this Court on the 14th day of AUGUST, 2019, to show cause why application for the judgment debtor to be detained as a civil prisoner should not be granted.

**GIVEN under my HAND and the SEAL of the court,**
**this 11th day of JULY, 2019.**

XXXXXX

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**
**RM. CIVIL CASE NO:29 OF 2017**

**ALLI CHAMANI ................................. PLAINTIFF**
**VERSUS**
**ANITHA COSTANTINE.................................1ST DEFENDANT**
**ASHURA KAJUNA......................................2ST DEFENDANT**

**Notice to show cause why execution should not issue**
**(O. XXI, r. 20(1) of the Civil Procedure Code)**

**To. ASHURA KAJUNA.**
Whereas the* Applicant has made application to this Court for the Judgment debtor to be committed to prison in the above suit, this is to give you notice that you are to appear before this Court on the 14th day of AUGUST, 2019, to show cause why application for the judgment debtor to be detained as a civil prisoner should not be granted.

**GIVEN under my HAND and the SEAL of the court,**
**this 11th day of JULY, 2019.**

XXXXXX

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz ,

au

piga simu: 0767 223311

Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza
Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0767 223 311

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SENEGAL
## KUMKOSA KOULIBALY FAINALI

**CAIRO, Misri**

SENEGAL imejivuta hatua moja kuukaribia ubingwa wa Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), kwa kupata ushindi wao kwenye nusu fainali juzi Jumapili, lakini itakuwa bila beki wake muhimu, Kalidou Koulibaly katika fainali ya michuano hiyo itakayochezwa Ijumaa.

Beki huyo ambaye anatajwa kama mmoja wa mabeki bora wanaotikisa kwenye soka la Ulaya kwa sasa, alionywa mara mbili katika mechi tatu, wakati wakipata ushindi wa ba 1-0 dhidi ya Tunisia juzi na hivyo ataukosa mchezo wa fainali.

"Ni aibu kwamba tutakuwa bila Kalidou, yeye ni nguzo kwa timu, mchezaji ambaye amekuwa muhimu zaidi kwetu. Tutacheza pia kwa ajili yake," alisema kiungo Pape Alioune Ndiaye akiwaambia waandishi wa habari.

Koulibaly, ambaye anawachezea miamba wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Napoli, alionekana kumchezea rafu, Ferjani Sassi na kuonywa na mwamuzi.

Naye Kocha wa Senegal, Aliou Cisse, mara baada ya mchezo huo alisema kwamba, ulikuwa ni wa aina yake na walipata nafasi ya kutinga fainali katika dakika za majeruhi.

"Mchezo ulikuwa ni mgumu mno, sasa imebakia nafasi kwenye fainali, naamini chochote kinaweza kutokea," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Ndio furaha ya mpira wa miguu, ni mchezo wa hisia. Hatuwezi kuwa kwenye nafasi nzuri kila wakati."

Hii itakuwa ni fainali ya pili kwa Cisse, ambaye alikuwa nahodha wa Senegal walipotinga fainali ya michuano hiyo mwaka 2002 na walipoteza kwa mikwaju ya changamoto ya penalti.

"Ni fahari kutinga fainali. Imekuwa ni miaka 17 tangu tulipofuzu kwa michuano hiyo, tangu kizazi chetu cha mwaka 2002," alisema Cisse.

# ROHR: ALGERIA WALISTAHILI USHINDI

**CAIRO, Misri**

KOCHA wa Nigeria, Gernot Rohr, amesema Algeria walistahili ushindi wa nusu fainali baada ya bao la Riyad Mahrez kuwapeleka fainali ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa mara ya kwanza baada ya miaka 29.

Winga wa Manchester City, Mahrez alifunga bao hilo la ushindi kutoka umbali wa yadi 20 katika dakika za mwisho jijini Cairo na kupata ushindi wa mabao 2-1, baada ya Nigeria, Odion Ighalo kusawazisha wakati William Troost-Ekong alipojifunga na kuwapa Algeria bao la uongozi.

"Tulipigana hadi dakika ya mwisho. Algeria walicheza vizuri zaidi kipindi cha kwanza kuliko sisi, lakini tulirudi katika kipindi cha pili na tukaruhusu bao la dakika ya mwisho," alisema Rohr.

"Nafikiri wachezaji walitaka kwenda muda wa ziada na waliamini Algeria wangekuwa wamechoka na kwamba wangeweza kushinda dakika za muda wa ziada."

"Nawapongeza wachezaji kwa kupigana kwa ustadi dhidi ya timu nzuri. Walishinda katika dakika ya mwisho na walistahili," aliongeza kusema.

"Algeria ni timu yenye wachezaji wazuri na wapiganaji waliojipanga, hivyo kwangu mimi naona nimepoteza mbele ya timu bora kabisa."



# Belmadi anataka Afrika iwaamini wazawa

**CAIRO, Misri**

KOCHA wa Algeria, Djamel Belmadi, ana matumaini kwamba fainali ya Afcon ya Ijumaa hii dhidi ya Senegal itazishawishi nchini nyingi za Afrika kuwaamini makocha wazawa.

Timu zote mbili zina makocha wazawa ambao wapo kwenye umri wa miaka 40, huku mchezaji huyo wa zamani wa Algeria, Belmadi akiwaongoza mbweha hao wa Jangwani na Senegal ikiwa chini ya Aliou Cisse, ambaye aliwachezea Simba hao wa milima ya Teranga wakati walipofika fainali mwaka 2002.

"Ni ujumbe mzuri ambao tumetuma kwenye soka katika nchi zote za Afrika, inavutia," alisema Belmadi akiwaambia waandishi wa habari baada ya timu yake kuifunga Nigeria mabao 2-1 juzi Jumapili.

"Nimemjua Cisse kwa miamba mingi, nimecheza dhidi yake mara nyingi wakati wote tukiwa nchini Ufaransa. Tofauti kati yetu ni kwamba yeye amekuwa na timu kwa miaka minne na mimi nimekuwa na timu kwa mwaka mmoja.

"Kucheza fainali dhidi Senegal, dhidi ya rafiki yangu, inavutia. Natumaini wafanya maamuzi wanatakiwa kufikiria kuhusu hili, na wanaweza kufikiri zaidi kuhusu jambo hili na kuweka imani kwa makocha vijana."

Kuhusu mechi yenyewe, Belmadi amesema timu yake ilitakiwa kufunga zaidi ya bao moja kipindi cha kwanza, lakini walishindwa kutumia vizuri nafasi yake.

"Tulijua kwamba ungekuwa mchezo mgumu kwa sababu ya ubora wa timu zote mbili," alisema.

"Vijana wangu walicheza mchezo wa kuvutia katika kipindi cha kwanza na tulitakiwa kufunga mabao mengi zaidi. Halafu kipindi cha pili, nafikiri tulikuwa na wakati mgumu kwa dakika 15, wakati tukiwa kwenye presha kubwa.

"Tulicheza kwa umakini, lakini tulizidiwa, tulishindwa kuongeza presha zaidi kwa wapizani wetu," alisema.

"Nafikiri wachezaji walionyesha mchezo mzuri, walikuwa imara na tulipigana kwa juhudi kubwa," aliongeza.

## HABARI MICHEZO



# HAZARD

## ACHAGUA JEZI NAMBA 23 MADRID

**MADRID, Hispania**

EDEN Hazard amechagua kuvaa jezi namba 23 akiwa katika timu yake mpya ya Real Madrid, huku akiwa na matumaini ya kufikia mafanikio kama ya magwiji wa ligi ya mapira wa kikapu ya Marekani, NBA, Michael Jordan na LeBron James, kwa mujibu wa gazeti la Marca.

Hazard hatavaa tena jezi namba 10, kwa sababu kwa sasa hiyo inavaliwa na mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or, Luka Modric, hivyo ameamua kuchagua namba nyingine.

Jezi namba 23 hapo Madrid ilitambulika zaidi na kuwa na mafanikio wakati ikivaliwa na David Beckham, lakini sasa nahodha huyo wa Ubelgiji ana matumaini ya kuweka alama yake.

Gwiji wa mpira wa kikapu Jordan aliifanya jezi namba 23 kuwa na umaarufu mkubwa duniani wakati akiichezea timu ya Chicago Bulls.

Kwa hivi karibuni, LeBron alitumia jezi namba 23 wakati akiichezea Cleveland Cavaliers na sasa anaivaa pale Los Angeles Lakers.

Hivyo, Hazard ambaye ni shabiki mkubwa wa mpira wa kikapu anataka kupata mafanikio makubwa akiwa na jezi namba hiyo.

Hazard alikamilisha usajili wa pauni milioni 150 kutoka Chelsea kwenda Madrid, na klabu hiyo ya Hispania imetumia fedha pia kuwasjili nyota wengine kama Ferland Mendy na Luka Jovic kipindi hiki cha majira ya joto.

Aliripoti kwenye mazoezi katika siku yake ya kwanza wiki iliyopita, chini ya kocha Zinedine Zidane.



## DANIEL STURRIDGE ATAKIWA BOLOGNA

**ROME, Italia**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Liverpool, Daniel Sturridge amepewa nafasi ya kuendelea kuonyesha kipaji chake cha kucheza soka la ushindani, baada ya klabu ya Bologna kuripotiwa kwamba inataka kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 yupo huru baada ya kumaliza mkataba wake pale Liverpool na kushindwa kuongezwa.

Kwa mujibu wa gazeti la Sunday Express, miamba hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, wametoa ofa kwa Sturridge.

Bologna imempa ofa Sturridge ya kumlipa mshahara wa pauni chini ya 120,000 kwa wiki ya ule aliokuwa akilipwa pale Liverpool.

Licha ya kushindwa kufikia kiwango cha mahitaji ya mshahara wa mchezaji huyo wa zamani wa England, Bologna bado ina matumaini ya kumpata nyota huyo.

Aston Villa na Rangers pia zimekuwa zikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto, lakini bado hazijatuma ofa zao.

Sturridge alifunga mabao 67 katika mechi 160 alizoichezea Liverpool kwa kipindi cha misimu sita na nusu aliyokaa kwa wekundu hao, akiwa pia ameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

# KLOPP: TUTASAJILI BEKI WA KUSHOTO

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amebainisha kwamba, Liverpool wana nafasi ya kumsajili beki wa kushoto wa kumsaidia Andrew Robertson katika kipindi hiki cha dirisha la majira ya joto.

Nahodha huyo wa Scotland alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwa kikosi hicho msimu wa 2018-19, amefanyiwa operesheni ndogo kwenye mkono wake baada ya kung'atwa na mdudu na kupata maambukizi.

Atarudi kwenye mazoezi ya klabu hiyo na atasafiri na klabu kwenda nchini Marekani ambako wataweka kambi ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu England, lakini Klopp bado amebainisha ana nafasi ya kusajili beki wa kushoto wa kumsaidia nyota wake huyo mwenye umri wa miaka 25.

Liverpool ilimpoteza Alberto Moreno aliyejiunga na Villarreal kwa uhamisho huru kipindi hiki cha majira ya joto, huku Yasser Larouci na Adam Lewis wote wamepewa nafasi ya kuonyesha viwango vyao kipindi hiki cha maandalizi ya msimu mpya na walicheza dhidi ya Tranmere Rovers na Bradford City.

"Tayari nilishasema, tunatakiwa kufikiria kuhusu kila kitu, na mwishoni wa siku pengine hatutafanya chochote, lakini tataona," alisema kocha huyo baada ya mchezo wa kirafiki wa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Valley Parade.

"Kama unavyoweza kufikiria, tutatakiwa kuangalia vitu vingi vinavyotuzunguka sisi. Bila shaka tumempoteza beki wa kushoto (Moreno), na leo umewaona vijana (Larouci) na (Lewis), huku James (Milner) amecheza mara nyingi."

Katika safu ya kiungo, Klopp ameamua kumwachia jukumu hilo Adam Lallana na ameelezea kuwa yeye ndiye atakayeongeza safu hiyo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO ANUKIA KUTUA BUNDESLIGA

●●● Ni kutokana na Mreno huyo kuanza kujifunza lugha ya Kijerumani...

**MILAN, Italia**

JOSE Mourinho amefungua mlango wa kuchukua nafasi ya ukocha kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, baada ya kocha huyo wa zamani wa Manchester United kubainisha kwamba, kwa sasa akiwa hana kazi anasoma lugha ya kijerumani.

Raia huyo wa Ureno alifukuzwa kazi pale United Desemba mwaka jana bada ya kufungwa na wapizani wao wa soka la England, Liverpool kwenye Uwanja wa Anfield. Mourinho, amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi kufundisha kipindi hiki cha majira ya joto, huku klabu za Benfica, Lyon na Newcastle zikitajwa kumwania.

Lakini sasa kuna uwezekano mkubwa wa kutua Ujerumani na ligi hiyo ya Bundesliga inaweza kuwa sehemu atakayofundisha kocha huyo mwenye umri wa miaka 56, kwani kwa sasa anajifunza kuielewa zaidi lugha ya nchi hiyo.

"Kwa sasa nasoma lugha ya kijerumani," amesema Mourinho katika mahojiano yake na gazeti la michezo la Italia, Gazzetta dello Sport.

"Bundesliga? Sasa, nasoma lugha ya kijerumani kwa sababu siijui. Nazungumza kiingereza, kihispania, kireno na kiitaliano." Mourinho, ambaye kwa sasa anafanya kazi kama mchambuzi wa soka kwenye televisheni, na amezungumzia njaa yake ya kurudi kwenye soka.

Alipoulizwa kama kwa sasa yupo njiani kurudi kwenye utawala wa kufundisha soka, Mourinho aliiambia Sky Sports: "Nina njaa ya kurudi kwenye soka, lakini nitasubiri katika klabu sahihi, na kwa muda muafaka.

"Na kwa wakati nilionao, nafanya vitu ambavyo napenda kuvifanya. Napenda kufanya kazi, lakini napenda michezo mingine na hii ni nafasi nzuri kufurahia mambo nje ya soka."

Mourinho hadi sasa amefanya kazi katika nchi za Ureno, Hispania, Italia na England na amebainisha kwamba bado ana mawasiliano na klabu zake ambazo amewahi kuzifundisha.

Inter Milan, ambayo Mourinho aliipa mafanikio makubwa msimu wa mwaka 2009-10, msimu huu watakuwa chini ya kocha wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte.

Na Mourinho anaamini kwamba klabu yake hiyo ya zamani itashinda taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, chini ya Conte na kumaliza utawala wa muda mrefu wa Juventus.

## KWA UFUPI

**UNITED, MAGUIRE SAFI**
MANCHESTER United imekubali kuilipa Leicester City pauni milioni 80 kwa ajili ya kumnasa, Harry Maguire ambaye atakuwa ndiye beki ghali zaidi kusajiliwa. United italipa pauni milioni 60 kwa beki huyo wa kati aliyetarajia kufanyiwa vipimo vya afya jana na itamalizia pauni milioni 20 katika awamu ya pili. ***(Sun)***

**ATLETICO MAMBO MAGUMU**
ATLETICO Madrid inatajwa kuwa haina ushahidi wowote wa kuwasaidia kuandaa mashataka dhidi ya Barcelona kuhusu makubaliano waliyoingia na mshambuliaji wa Mfaransa, Antoine Griezmann (28), kwa haraka zaidi, amesema Rais wa Barca, Josep Maria Bartomeu. ***(Goal)***

**DUNK KUMRITHI MAGUIRE**
LEICESTER City inajiandaa kumsajili beki wa Brighton na Timu ya Taifa ya England, Lewis Dunk, mwenye umri wa miaka 27 kwa dau la pauni milioni 45 ili kuziba nafasi itakayoachwa na Harry Maguire ambaye anajiunga na Manchester United. ***(Sun)***

**COUTINHO KITAELEWEKA**
KIUNGO wa Barcelona, Philippe Coutinho (27), anakaribia kukamilisha mchakato wake wa kurejea katika klabu yake ya zamani ya Liverpool kwa kusaini mkataba wa miaka miwili ambao utaifanya Reds kuweza kumnunua Mbrazil huyo baadaye kwa dau la pauni milioni 88. ***(Calciomercato - in Italian)***

**CELTIC WAIGOMEA ARSENAL**
MABOSI wa Celtic wameikacha ofa mpya ya Arsenal ambao wanahitaji saini ya beki wake wa kushoto ambaye ni raia wa Scotland, Kieran Tierney (22), baada ya kuwa si ya thamani ya pauni milioni 25. ***(Sky Sports)***

**CITY YAMWAMINI SANE**
MANCHESTER City inaamini kuwa Leroy Sane ataikacha ofa itakayowasilishwa rasmi na mabingwa wa Bundesliga, Bayern Munich ambao wanatajwa kuhitaji saini ya winga huyo Mjerumani mwenye umri wa miaka 23. ***(Mirror)***

**ALVES AGOMBEWA ENGLAND**
TOTTENHAM na Arsenal zimeingia kwenye vita ya kuwania saini ya beki wa Timu ya TAifa ya Brazil, Dani Alves (36), ambaye kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kuondoka kwa vigogo wa Ufaransa, Paris St-Germain. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**AC MILAN, ROMA VITANI**
AC Milan imeungana na klabu nyingine ya Italia, Roma kusaka saini ya kiungo wa Fulham na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Jean Michael Seri, ambaye ana umri wa miaka 27. ***(Express)***

**MBRAZIL SOKONI EPL**
MSHAMBULIAJI anayewindwa na Arsenal na Everton, ambaye ni nyota wa klabu ya Gremio na Timu ya Taifa ya Brazil, amesema kuwa amepokea ofa lakini hataki kutaja ni klabu gani zinamhitaji ili kuondoa maswali. ***(Mirror)***

**KLOPP KUSAJILI BEKI**
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema kuwa klabu yake itaangalia uwezekano wa kusajili beki wa kushoto ili kujaza nafasi ya nyota wa Timu ya Taifa ya Scotland, Andrew Robertson (25), katika kipindi hiki cha dirisha la usajili la majira ya joto. ***(ESPN)***

**BRUCE KUINGIA MTEGONI**
KAZI ya kuifundisha Newcastle United itakuwa ni moja ya changamoto kubwa ambayo Steve Bruce hajawahi kukutana nayo tangu aanze kufundisha mpira wa miguu kwa muda wa miaka 21 kama ataamua kuondoka Sheffield Wednesday na kujiunga na klabu hiyo ya St James' Park, amesema winga wa zamani wa Magpies, Chris Waddle. ***(Newcastle Chronicle)***

**KANE KUTOLEWA MKOPO**
KIUNGO raia wa England wa Liverpool, Herbie Kane, anatarajia kukamilisha mchakato wa kujiunga kwa mkopo na klabu inayoshiriki mashindano ya Championship wakati wowote wiki hii. Brentford, Charlton Athletic na Hull City zote zimetajwa kumwania chipukizi huyo mwenye umri wa miaka 20 na ambaye msimu uliopita aliitumikia Doncaster Rovers. ***(Goal)***

# MATAWI YANGA KUKUTANA KESHO KUPANGA MIPANGO

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI viongozi wa Matawi ya Yanga wanatarajia kukutana kesho ili kupanga mikakati kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mwinyi Zahera, anatarajiwa kurejea siku yoyote kuanzia leo, imeelezwa.

Yanga itafungua pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa mwaka 2019/20 kwa kucheza dhidi ya Ruvu Shooting ya Mlandizi, Pwani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema kuwa tayari muda wa likizo ambao aliopewa, umemalizika na anarejea kwa lengo la kukiimarisha kikosi chake.

Mwakalebela alisema kuwa licha ya kikosi chao kuanza mazoezi bila ya kuwapo kwa kocha huyo, alitoa maelekezo na mipango ambayo inatekelezwa ili kuwafanya wachezaji wawe na viwango bora.

"Siku yoyote kuanzia leo tunategemea kocha wetu mkuu (Zahera) atawasili nchini na ataelekea Morogoro ilipo timu ili aweze kuendelea na majukumu yake ," alisema Mwakalebela.

Aliongeza kwamba wanaamini timu yao itafanya vema zaidi msimu ujao kutokana na mipango na mikakati imara ambayo wameiandaa.

"Ili kuweka mambo yote sawa sawa, Julai 17 (kesho)mwaka huuwa tutakuwa na mkutano na viongozi wa Matawi yote ya Yanga Dar es Salaam, tunaamini kila anayestahili kushiriki kwenye maandalizi, atatekeleza majukumu yake sawa sawa," Mwakalebela.

Aliongeza kuwa maandalizi ya kuelekea Tamasha la Siku ya Mwananchi itakayofanyika Agosti 4 mwaka huu, yako katika hatua za mwisho na wanawaomba mashabiki na wanachama kuhudhuria kuona wachezaji wao wapya waliosajiliwa.

Yanga pia itashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Simba ambayo msimu uliopita ilifika hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).




Meneja Mwandamizi wa Chapa ya Coca-Cola Tanzania, Kabula Nshimo (kushoto), akitambulishwa na mshereheshaji rasmi wa mashindano makubwa ya kuibua vipaji ya kuibua vipaji kwa ukanda wa Afrika Mashariki (East Africa's Got Talent), Anne Kansime, katika hafla ya kuwatambulisha majaji wa shindano hilo iliyofanyika katika makao makuu ya Coca-Cola jijini Nairobi hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kennedy: Ndoto zangu zimetimia

**Na Shufaa Lyimo**

BEKI mpya wa mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Kennedy Juma, amesema kuwa ndoto yake aliyokuwa akiiota kwa muda mrefu kuichezea klabu hiyo imekamilika.

Kennedy, beki wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), amejiunga na Simba akitokea Singida United ya mkoani Singida, klabu ambayo aliitumikia tangu ikiwa Ligi Daraja la Pili.

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuelekea Afrika Kusini kuweka kambi ya wiki mbili kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao, mchezaji huyo alisema alikuwa anatamani kuichezea Simba na amefurahi kuona amepata nafasi hiyo kipindi hiki. Kennedy alisema kuwa baada ya kufuatwa na viongozi wa Simba, haikuchukua muda kwake kukubali ofa kwa sababu aliamini anajiunga na klabu aliyokuwa akitamani kwa muda mrefu.

**"Ile ndoto yangu ya kucheza katika klabu kubwa kama Simba imekamilika, naahidi kushirikiana na wachezaji wenzangu na kuhakikisha tunatetea ubingwa wa Ligi Kuu," alisema Kennedy.**

Alisema kuwa licha ya msimu ujao wa Ligi Kuu Bara kuonekana utakuwa na changamoto mbalimbali, yeye amejipanga kupambana kwa uwezo wake wote ili awape furaha na burudani mashabiki na wanachama wa klabu hiyo.

"Mashabiki na viongozi wangu sitawaangusha, nitafanya kile kilichonileta Simba, kikubwa ni nidhamu na kumsikiliza mwalimu kwa umakini anapokuwa anatufundisha," Kennedy aliongeza.

# Mdee, Koinange majaji wapya EAGT

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya kupata mshindi wa East Africa Got Talent yamefika hatua ya mbele zaidi baada ya majaji wake kutangazwa rasmi jana kwenye ofisi ya Coca Cola jijini Nairobi, Kenya.

Jopo la majaji hao linamjumuisha Jeff Koinange, ambaye ni maarufu zaidi katika vyombo vya habari nchini Kenya akiwa amewahi kufanya kazi katika vyombo mbalimbali vya habari duniani.

Jaji mwingine ni Gaetano Kagwa, mwigizaji wa Uganda na mtangazaji ambaye amejizolea umaarufu mkubwa zaidi katika eneo hilo ambaye pia anatangaza katika kituo cha Capital FM, akiongoza kipindi cha Tusker Project Fame na alikuwa mshiriki wa Big Brother Africa.

Jaji mwingine ni msanii, Vanessa Mdee, mtunzi wa nyimbo na Mtanzania wa kwanza MTV VJ, mwenyeji wa Epic Bongo Star Search na pia alishiriki kwenye shoo ya runinga ya Coke Studio Africa 2019 kati ya nyota wengine wa muziki wa Afrika.

Pia yumo Makeda Mahadeo aliyebobea katika vyombo vya habari nchini Rwanda na DJ wa kwanza wa kike nchini Rwanda.

Majaji watakuwa na jukumu muhimu katika kuidhinisha washiriki ambao watakiwa kuendelea kwa hatua inayofuata mwishoni mwa kila hatua na kutoa maoni au kukosoa juu ya waliyoshuhudia jukwaani. Washiriki wataondolewa ikiwa hawapati kura nyingi kutoka kwa majaji wanne.

Hii ni shoo ambayo itakuwa kinyumbani zaidi kufuatana na soko ambapo itatangazwa katika nchi nne za Afrika Mashariki ikiwemo Kenya, Tanzania, Uganda na Rwanda. Vyombo vya habari vishiriki vitakuwa ni Citizen TV, Clouds Tv, NBS na RTV.

Kampuni ya Coca-Cola pia itakuwa na jukumu la kutoa huduma mbalimbali zikiwamo ushauri wa ushiriki wa fursa katika kanda nne zilizoshiriki.

"Mfumo wa Coca-Cola unaamini kusaidia sekta ya ubunifu nchini na kutoa jukwaa ambapo watu wanaweza kuonyesha na kuendeleza vipaji vyao katika kanda. Tunaamini kwamba majaji waliochaguliwa wana uwezo wa kuchagua vipaji bora kwa wasikilizaji wetu wa Afrika Mashariki, ili waweze kufahamu na kufurahia shoo, "alisema Beatrice Nyamari, Meneja Mwandamizi wa Mawasiliano wa Coca-Cola Kanda ya Biashara Kusini na Mashariki mwa Afrika (SEABU).

"Afrika ya Mashariki ina vipaji vya kuonyesha ambavyo vinatoa fursa kwa Waafrika Mashariki kuonyesha talanta zao na kampuni yetu inaamini katika kutoa majukwaa ya watu kustawi, tunafurahi sana kuwa sehemu ya shoo,"alisema Sitoyo Lopokoiyit, Afisa Mkuu wa Huduma za Fedha wa Safaricom.


Jukwaa hilo litaonyesha vipaji mbalimbali kutoka kwa watu wote wa umri tofauti wa Afrika Mashariki, na litajumuisha vipaji vinavyotokana na kuimba, kucheza, maigizo na aina nyingine nyingi za vipaji.

"Sisi tunafarijika kuleta msisimko huu wa kidunia nyumbani. Tunaamini kuwa jukwaa hili litaamua wafuatiliaji wa kimataifa kwa vipaji vya kipekee vya Afrika Mashariki, "alisema Joseph Kusaga, Mkurugenzi Mtendaji wa Clouds Media International na mmiliki wa Franchise.

Kila mshiriki anahitaji kupokea idhini tatu kutoka kwa majaji kwenda kwenye duru ijayo.

Mshindi wa shindano hilo ambalo kuanzia Agosti mwaka huu litaanza kuonyeshwa na itakuwa na vipindi 10, pamoja na nusu fainali na fainali, atapata zawadi ya Dola za Marekani 50,000 (sawa za zaidi ya Sh. milioni 110).

Michezo
Jumanne Julai 16, 2019
Nipashe



## Mourinho anukia kutua Bundesliga

HABARI UK 30

# JUMA KASEJA AFUNGUKA KUREJESHWA TAIFA STARS



**Kipa huyo wa zamani wa Simba aelezea kilichosababisha kupata uteuzi huo...**

**Na Mwandishi Wetu**

KIPA mkongwe na mzoefu katika mashindano ya kimataifa nchini, Juma Kaseja, amerejeshwa katika kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars) ambacho kitajiandaa kuikaribisha Harambee Stars ya Kenya kwenye mchezo wa kuwania kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), imefahamika.

Taifa Stars itaikaribisha Harambee Stars Julai 28, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Taifa, na timu hizo zitarudiana Agosti 2 mwaka huu jijini Nairobi, Kenya.

Kaseja amekuwa nje ya kikosi cha Taifa Stars kwa zaidi ya miaka 10, lakini mwaka jana alirudi kulitumikia taifa kupitia Timu ya Taifa ya Ufukweni, ambayo ilishiriki mashindano ya Afrika kwa mara ya kwanza.

Mbali na Kaseja, wachezaji wengine walioitwa katika kikosi hicho ambao walikuwa nje kwa muda mrefu ni kiungo tegemeo wa Azam FC, Salum Aboubakary "Sure Boy" na Hassan Dilunga wa Simba.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaseja, alisema kuwa anamshukuru Mungu kwa uteuzi huo kwa sababu hakuna aliye juu yake. "Allah mkubwa tu," alisema kwa kifupi Kaseja ambaye katika jezi zake za mazoezi anajiita "Copper " akimaanisha yeye ni shaba na kueleza kuwa kiwango chake daima hakishuki. Taarifa kutoka Rwanda zinasema kuwa Kaseja, ambaye timu yake ya KMC imeyaaga mashindano ya Kombe la Kagame, alionyesha kiwango cha juu wakati walipoikabili Rayon Sport na kupata ushindi wa bao 1-0, huku pia akikaa langoni walipocheza dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), na kufungwa goli 1-0.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema kuwa kikosi hicho cha wachezaji 26 kilichoitwa na Kocha Mkuu mpya, Etienne Ndayiragije, kitaingia kambini Julai 21, mwaka huu, kwa ajili ya kuanza kujiandaa na mechi hizo mbili za michuano ya CHAN.

Ndimbo alikitaja kikosi kamili kilichoitwa kujiandaa na mchezo huo kuwa ni pamoja na Aishi Manula (Simba), Kaseja, Metacha Mnata, Paul Godfrey (Yanga), Boniface Maganga (KMC), Gadiel Michael (Simba), Paul Ngalema (Namungo FC), David Mwantika (Azam FC), Idd Mobi (Polisi Tanzania), Kelvin Yondani (Yanga), Erasto Nyoni, Jonas Mkude (Simba), Abdulazi Makame (Yanga) na Mudhathir Yahya wa Azam.

Wachezaji wengine ni Ibrahim Ajib kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba, Salim Aiyee (KMC), Salum Abobakar, Masoud Abdallah (Azam FC), John Bocco (Simba), Ayoub Lyanga (Coastal Union), Kelvin John (U 17), Feisal Salum "Fei Toto" (Yanga), Frank Domayo (Azam FC), Hassan Dilunga (Simba), Iddy Naldo (Azam FC) na Shaban Chilunda wa Azam FC.

Katika timu hiyo, Ndayiragije ambaye amerithi mikoba ya Mnigeria Emmanuel Amunike, atasaidiana na Juma Mgunda kutoka Coastal Union na Suleiman "Veron" Matola wa Polisi Tanzania.

## Aussems atamba watarejea imara

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kikitua salama Afrika Kusini kwa ajili ya kuanza maandalizi ya msimu mpya, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Aussems, amesema kuwa anaamini wachezaji wake watarejea nchini kuanza kutetea taji lao wakiwa na "makali ya hali ya juu".

Hata hivyo Aussems alisema kuwa programu yake haitahusisha wachezaji wote kwa muda wote, kwa sababu baadhi ya nyota watakaoitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars) watalazimika kurejea mapema ili kujiandaa kucheza dhidi ya Kenya, katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Akizungumza na gazeti hili muda mfupi kabla ya kuanza safari jana, Aussems, alisema kuwa anaamini kambi hiyo itazaa "matunda" na watarejea nchini wakiwa imara na tayari kufanya vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Aussems alisema kuwa wachezaji wote waliosajiliwa na mabingwa hao watakuwapo katika wiki ya kwanza ya mazoezi na wakiwa nchini humo, wanatarajia kucheza mechi tatu za kirafiki.

"Leo (jana) tunaondoka na baadhi ya wachezaji, tukifika huko tutaanza mazoezi, ila Jumatano nitakuwa na wachezaji wote 26, lakini ikifika Julai 24, wachezaji watakaoitwa katika Timu ya Taifa watalazimika kurejea, hatuoni kama tutakuwa kwenye maandalizi kamili," alilalamika Aussems.

Aliongeza kuwa baada ya kufanya mazoezi ya wiki mbili, kikosi chake kitarejea nchini tayari kusubiri mechi ya Simba Day ambayo mwaka huu huenda ikawa na mabadiliko kutokana na kuwapo kwa mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika. Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, aliliambia gazeti hili kuwa, tayari kuna makubaliano yamefanyika kati yao na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kuhusu muda ambao wachezaji wao watatakiwa kuripoti kwenye kambi ya Stars.

"Tunalazimika kukubaliana na hali hii, kwa sababu ya kuweka mbele maslahi ya Taifa, " Magori alisema kwa kifupi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >